Kikao cha Ishirini na Mbili - Tarehe 16 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

Maswali na Majibu

Nam. 60

Kutembelewa Vikundi vya Uzalishaji vya Wanawake

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Wanawake wengi katika ukanda wa bahari ya Mashariki Kisiwani Pemba tayari wameanza kutekeleza ule mpango wa Serikali wa kujiongezea kipato na kupunguza umaskini (MKUZA) kwa kujishughulisha na ufugaji wa mazao ya bahari kama vile samaki na kaa. Kwa kuwa mambo haya yanahitaji utaalam katika suala zima la ufugaji na ulishaji wa mifugo hiyo.

Je, Serikali angalau imeshawahi kutembelea vikundi vya wanawake hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi- Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 60, naomba kutoa maelezo machache.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, kwamba wanawake wengi waishio katika ukanda wa bahari ya Mashariki Kisiwani Pemba wameanza kutekeleza mpango wa serikali wa kujiongezea kipato na kupunguza umaskini (MKUZA) kwa kujishughulisha na ufugaji wa mazao ya baharini kama vile samaki na kaa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia wataalamu wake pamoja na viongozi mbali mbali imewatembelea wafugaji wa samaki, kaa na mazao mengine ya baharini na kuwapatia ushauri wa kitaalamu. Hivi sasa katika Kisiwa cha Pemba kuna jumla ya vikundi 93 vinavyojishughulisha na ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo ambavyo vinajumuisha wanawake na wanaume.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile suala la ufugaji wa mazao ya baharini kama vile samaki, kaa, chaza na majongoo linahitaji utaalamu. Serikali kupitia Idara ya Mazao ya Baharini imekuwa na utaratibu wa kuvitembelea vikundi hivi vya ufugaji kila mwezi Unguja na Pemba kwa lengo la kuangalia maendeleo ya ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini katika vikundi hivyo. Pia, kutoa taaluma kwa wanavikundi juu ya njia bora ya kuendeleza ufugaji wenye tija pamoja na kusikiliza changamoto mbali mbali za ufugaji wa samaki kwa vikundi hivyo na kuzitafutia ufumbuzi.Aidha, katika kipindi cha Julai hadi mwezi Aprili, 2014, jumla ya vikundi 76 vya ufugaji wa mazao ya baharini Kisiwani Pemba vimetembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalam nikiwemo mimi mwenyewe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa bidii na juhudi zake katika kuwatumikia wananchi. Kwa kweli Mhe. Naibu Waziri, ni miongoni mwa Manaibu Waziri wachache sana kupatikana katika serikali zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara tukiwemo sisi. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Wawi analotoka Waziri Mohammed Aboud Mohammed, naomba nimuulize swali moja dogo sana la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo ya Vitongoji Umangani, Furaha, Uwandani pamoja na hapa sehemu za Matungu wameshajiika sana katika kufuga samaki na kaa na kwa kuwa kaa tulionao katika visiwa hivi ni wale wa zamani ambao uzazi wao huchukua muda mrefu sana, ndio wakapata kuzaa na kukua na kupata faida.

(a) Je, kwa sababu wenzetu Wachina wana kaa wa *hybrid* na vile vile wana vyakula vinavyoweza kuwakuza kaa wale wakakua kwa muda mfupi. Je, ni lini Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein itatuletea wataalamu kutoka China kuweza kuja kutusaidia utaalam wa ufugaji kaa pale Vitongoji, Wawi, Kibokoni, Udusini, Umangani, ili akinamama waweze kupata kaa wengi kwa muda mfupi.

(b) Kwa sababu soko la kaa hapa watu hawajahamasika sana hasa huku vijijini kujua umuhimu wa kaa katika suala zima la mwili wao, na kwa hivyo, hawapendi kula kaa. Sasa soko la kaa linakuwa ni dogo sana hasa kule vijijini.Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuweza kuwapatia soko wafugaji wa samaki na kaa pale ambapo uzalishaji umekuwa mkubwa. Ni utaratibu gani umeandaliwa na serikali ili kupata soko.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, serikali tarehe 8 mwezi wa 4 imetia mkataba na *WHO* ili kujenga vituo mbali mbali vya kuzalisha samaki pamoja na mambo mengine hayo ya kaa na vile vile kuongeza bei ya mwani. Hivyo, huo ni utaratibu wa serikali wa sasa kuwaongezea soko, lakini pia, tumeanza kuwapeleka wafugaji wa samaki na kaa China na kwengineko, lakini kama hili lako hakuna mtu ambaye amepelekwa, tutafanya utaratibu katika duru ya pili itakayokwenda tuweze kukupelekea angalau mtu mmoja nae katika vikundi hivi ili aweze kuwafundisha wenzake katika uzalishaji mzuri wa kaa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili suala la soko naomba nilichukue ili niwasiliane na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili kuweza kuona jinsi gani wananchi wetu watapatiwa soko la kudumu na lenye manufaa zaidi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanatutia moyo, lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza.Kwa kuwa lengo la serikali ni kuwaendeleza wanavikundi wafugaji wa mazao ya baharini kama vile ufugaji wa samaki, kaa, chaza na kadhalika. Je, ni vikundi vingapi Unguja na Pemba ambavyo vimeweza kupatiwa mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili waweze kuendeleza ufugaji huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa swali lake ni la takwimu sana, kwa Zanzibar sasa hivi nitakosa kutoa takwimu halisi ya vikundi hivyo. Naomba nikujibu kwa maandishi, lakini kwa Pemba mpaka sasa ni vikundi 38 katika ukanda huo wa Mashariki vimeweza kusaidiwa na kupeleka watu wake nje ya nchi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza katika wizara hii. Kwa kuwa miongoni mwa wananchi walioshajiika sana katika ufugaji wa samaki ni wananchi wa Jimbo la Chambani wanaoishi Mashariki ya Chambani na kwa kuwa kuna mabwawa yasiyopungua saba, hawa vijana wamejikusanya kike na kiume kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

Je, Mhe. Naibu Waziri, ni mara ngapi umewatembelea wafugaji wa samaki katika Shehia hii ya Chambani na ni ushauri gani ambao uliutoa kwao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, katika Shehia ya Chambani nimetembelea mara mbili, lakini pia, katika Shehia ya Chambani kuna kikundi Mlekipi ambacho kimesaidiwa shilingi hamsini elfu, Kwa dada kichimba imesaidiwa shilingi laki tatu, majembe matano, mapauro na mafunzo ya nje mtu mmoja.

Nam. 71

Wizara ya Kilimo kuwapatia Mbolea bure Wakulima wa Mpunga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, lini Wizara ya Kilimo na Maliasili itatoa mbolea bure kwa wananchi wanyonge hasa wale wanaopanda mpunga kutokana na hali yao ya kimaisha kuwa duni hasa wanapotumia nguvu zao katika kulipia matrekta wakati wa kulipa kuchimbiwa mashamba yao.

(a) Je, kuwalipisha wakulima hao mbolea ni kuwaendeleza au ni kuwaumiza.

(b) Kwa vile wakulima wengi hulima mpunga mwaka mara moja. Je, Wizara itakuwa tayari kuwafikiria wakulima na kama haiko tayari naomba itoe sababu zake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Lengo la serikali la kuanzisha mpango wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo ni kuona kwamba kila mkulima ananufaika kwa kupata fursa ya kupata pembejeo kwa bei wanayomudu baada ya serikali kuchukua zaidi ya asilimia 86 ya gharama za pembejeo hizi na wakulima kuchangia asilimia 14 tu. Kufanya hivyo ni kuwaendeleza wakulima, sio kuwaumiza.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na mpango wa kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo kwa njia ya ruzuku kwa bei zilizopangwa hadi itakapoona kuna ongezeko la uzalishaji na wakulima wanapata tija na mapato ambayo yatawawezesha kununua pembejeo za kilimo kwa mujibu wa bei za soko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala la kilimo utekelezaji wake unakwenda na ratiba kulingana na maendeleo ya mazao. Wakulima wengi hata katika kutembelea Kamati wanacholalamikia wakiwemo na wananchi wa Jimbo la Muyuni kwamba mbolea kutokufika kwa wakati.

Je, hatua hii ya mbolea kutokufika kwa wakati ni kumuokoa au kumkandamiza mkulima.

La pili, kwa kuwa mpunga huota magugu, kulikuwa kuna dawa, chupa ikiuzwa shilingi elfu kumi na sasa hivi chupa hiyo inauzwa shilingi elfu ishirini. Je, ni nini kilichosababisha kupanda kwa haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mbolea inafika kwa wakati, lakini ni sababu ambayo inayosababishwa saa nyengine wakati tunapotoa tenda. Tatizo hili safari hii kwa mujibu lilivyotokea ni kwamba pesa za kuchukulia mbolea hazikuja kwa wakati. Hii ndio sababu kubwa iliyofanya kuchelewa kwa mbolea. Hadi leo mbolea ile haijafika. Fedha zilichelewa kuingizwa na kulima tunajua tunalima kwa msimu, ndio sababu iliyocheleweshwa wakati wa kuingizwa fedha kuzipata kwa wakati na mbolea imechelewa kufika kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, hili la dawa nalo ni suala ambalo lilijitokeza hivyo hivyo. Katika kilimo chetu safari hii tulichelewa kupata pesa za ruzuku kuanzia kulima mpaka kuagizia pembejeo. Wakati tulipoanza kulima matrekta tulichelewa kutiliwa pesa kwa ruzuku, wananchi wakaanza kulima kwa matrekta yao wenyewe binafsi.Suala la dawa alikuja mfadhili ambaye alituletea dawa na dawa ile iliuzwa kwa bei ya shilingi elfu ishirini, ndio maana wananchi wakaamua kununua dawa ile kwa bei hiyo na ilipoletwa dawa ya mara ya pili ya ruzuku ya serikali wakati wananchi wengi tayari wameshanunua ile dawa ya mfadhili. Kwa hivyo, dawa ile haikuuzwa kwa kuwakomoa wananchi hata siku moja. Hizo ruzuku inategemea na bei yenyewe inavyokuwa katika soko.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba asilimia 14 tu ndio wanayochangia wakulima na asilimia 86 inachukua serikali, lakini dawa iliyoletwa mara ya pili ikauzwa shilingi elfu ishirini, sio kwamba ile ruzuku imeondoka, ruzuku iko pale pale.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengi hutegemea kilimo na kwa kuwa kuna kupata na kukosa katika kilimo hicho.

Je, Mhe. Naibu Waziri, una mpango gani wa kuwasaidia wananchi wale ambao hawakufaidika na mavuno hayo ili angalau kuwapatia mbegu za kuwasaidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, tunajua siku zote kweli unapolima unategemea upate japo mbegu ya kuweka na katika kilimo tunahakikisha wakati wa kulima kuna kupata na kukosa. Sasa bado mkulima yeyote ambaye analima hakupata hata ile mbegu, lakini mbegu tunayoiuza inatolewa kwa bei ya ruzuku

nayo kilo shilingi mia mbili. Bado kwa sasa hakuna mkulima, kusema ukweli ambaye anakosa mbegu. Mbegu ipo wanasaidiwa.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mbolea ndio sababu kuu ya kuongeza uzalishaji wa mazao, lakini tulipokwenda kwenye Kamati tulipata malalamiko mengi kuhusu mbolea. Je, katika msimu huu wa vuli wamejipanga vipi kuhusu mbolea.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema kwamba yalitokea malalamiko ya mbolea kwa sababu ya kuchelewa kuingiziwa fedha za kuweza kuagizia mbolea, lakini kwa msimu huu namhakikishia Mhe. Mwakilishi, kwamba mbolea hii tuliyokuwa tumeiagizia kwa msimu huu uliopita tayari ipo tumeshalipa 10% na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda, tutamaliza ile 3% na msimu huu kutakuwa hakuna tatizo la mbolea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kabla ya kujibiwa swali langu, naomba uniruhusu dakika moja tu kumpongeza Mhe. Naibu Waziri, kwa umakini wake alipokuwa akimsaidia Mhe. Waziri, akipangua hoja vile vile.Vile vile, naomba Mhe. Naibu Spika, pindipo Mhe. Waziri, akimpigia simu, naomba ampe pole kwa majukumu yaliyomkuta vile vile kama ni kweli. Baada ya maelezo hayo naomba swali langu Nam. 69 lipate jawabu.

Nam. 69

Taarifa ya Wizara ya Miundombinu Kuhamisha Afisi zake

Hivi karibuni Ofisi za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zilihamishwa kutoka eneo la karibu na bandari ambapo ndipo kwenye majukumu yake mengi ikiwemo bandari ambako ni kituo kikuu cha kuingiza fedha, hali hiyo imewapa usumbufu wananchi wanaohitaji huduma mbali mbali kwa maendeleo ya nchi. Kuna taarifa kuwa Ofisi hizo zipo Kisauni na wananchi wengi hawajui Wizara hiyo ilikohamia.

a) Je, Wizara hiyo iliwatangazia wananchi wakati inahamisha Ofisi zake bandarini kwenda Kisauni.
b) Kuhamisha Ofisi na kupeleka umbali ulioko ni kweli kuwatendea haki wananchi wanaohitaji huduma za wizara kwa ukaribu.
c) Je, wizara itakubaliana na mimi kuwa wizara hiyo, ndio kawaida yake kuwatesa wananchi au kuwanyanyapaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, jengo lililokuwa la Makao Makuu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano lilidata ghafla na kusababisha kuta za nyumba kuachana na kupata maharibiko makubwa na baadhi ya sehemu za nyumba hiyo zilibomoka na kuanguka. Hali iliyopeleka kuhatarisha maisha ya wafanyakazi waliokuwa wakilitumia jengo na majirani wanaoishi karibu na nyumba hiyo. Hali hii ilisababisha baadhi ya wafanyakazi kuumia na kulazwa Hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulihami jengo hilo ili lisilete madhara makubwa zaidi kwa wafanyakazi na majirani wanaoishi katika maeneo husika, wizara iliwasiliana na Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa lengo la kuja kulikagua na kutoa mapendekezo ambapo mamlaka hiyo iliiagiza wizara kulifanyia matengenezo ya haraka jengo hilo. Aidha, pia Mamlaka ya Mji Mkongwe ilishauri wizara kama inaweza kuhama katika jengo hili ili wasiendelee kukaa kwani idadi kubwa ya wafanyakazi wanaweza kusababisha athari za kuendelea kubomoka.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ya jengo lile lilivyokuwa uongozi wa wizara uliamua kuhama katika jengo hilo na watendaji wake waligawanyika katika sehemu tatu ambapo viongozi wa wizara, yaani Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu walipata hifadhi katika jengo la Shirika la Meli. Huku Naibu Katibu Mkuu na baadhi ya watendaji wakihamia katika jengo liliokuwa Bohari Kuu la serikali na Idara ya Mipango ilihamia katika nyumba za wizara kule Kisauni.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii ya Afisi za wizara kuwa katika sehemu tatu ilipelekea usumbufu mkubwa katika utekelezaji wa kazi za kila siku kutokana na mgawanyiko huo wa wafanyakazi. Uongozi wa wizara kwa nia njema iliamua kuhamia katika majengo yaliopo Kisauni Zanzibar kwani majengo hayo ni mali ya wizara na katika maeneo hayo wizara hailipi kodi na wafanyakazi wake wote, wapo katika eneo moja, hali iliyopelekea urahisi wa utekelezaji wa kazi. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara iliwatangazia wananchi wote wa Unguja na Pemba kupitia redio na televisheni kuwa itahamia Kisauni kwa barua Nam. *MOIC/H. 10/1/VOL 111/31* ya tarehe 3/11/2013 kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji za Zanzibar. Tangazo ambalo lilitolewa kama wizara ilivyoomba. Aidha, Makatibu wote wa wizara za SMZ walijuulishwa juu ya uamuzi huo kwa kuhama katika eneo hilo kwa barua Nam. *MOIC/N 10/1/VOL. 111/38* ya tarehe 28/11/2013;

b) Kuhama katika eneo hilo ni haki na hakuna tatizo lolote kwa wananchi wanaohitaji huduma za wizara yetu, kwani watu na wageni mbali mbali wamekuwa wakifika huko Kisauni bila ya usumbufu wowote na kupatiwa huduma kwa vizuri. Hata Wajumbe wako waliofika katika eneo hili ni mashahidi wa hayo; na

c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano haina kawaida ya kuwasumbua wananchi kila anayestahiki kupata huduma hizo atapatiwa bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, swali nililiilouliza mimi ninafikiri Mhe. Naibu Waziri, hakunifahamu mimi. Hili jengo la mara ya pili, sio la mwanzo, lile la mwanzo sote tunajua kuwa ni bovu tokea kwa Mhe. Waziri Machano Othman Said.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la pili walihamia, sio la mwanzo Mhe. Naibu Waziri. Hapo mulipokaa mara ya pili ndio jengo lilivyokusudia Mhe. Naibu Spika. Kwa heshima na taadhima naomba munifahamishe jengo lile la mara ya pili, sio la mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, majibu kama umemfahamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, makao makuu ya wizara yaliyokuwa ni hayo jengo la kwanza. Jengo la pili, lilikuwa ni jengo la Shirika la meli na tumesema kwamba katika jengo hilo la Shirika la meli hatukupata kukaa uongozi mzima wa wizara. Waliopata nafasi ya kukaa mule ilikuwa ni Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu.Naibu Katibu Mkuu na baadhi ya watendaji wakurugenzi wengine walikuwa wanakaa katika Bohari, lakini Idara yetu ya Mipango na Uendeshaji ilikuwa inakaa Kisauni. Kwa hivyo, wizara yetu ilikuwa imegawanyika vipande vitatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, anapozungumza jengo la pili, maana yake hili jengo la Shirika la meli. Sisi tulikuwa tumeazimwa vyumba vitatu ambavyo anatumia Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Kwa hivyo, tumetoka pale kwa sababu sio kwetu, tumekwenda kwenye eneo letu la Kisauni ambalo wizara nzima tunakaa pamoja hivi sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi ndiye mwenye swali. Nimemfahamu sana Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa anajibu swali langu. Swali serikali ndio wananchi na wananchi ndio serikali, kuna sababu gani ya msingi kwenda kuhamia kule jengo na pana jengo hivi sasa pale lililokuwa la Ubalozi wa Oman, kwa nini musihamie pale na wananchi ndio serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hamuoni kwamba ndio munakimbia wananchi makusudi hivi. Leo mwananchi atoke bandari aende Kisauni, nauli ya daladala hana, tunawafanyia haki wananchi hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Mjumbe, asihamishe goli, maana anahamisha magoli. Swali lake aseme alichokusudia ni nini, maana amezungumza swali la kwanza, kwa nini mumehamisha jengo. Tumemwambia sababu jengo lililokuwepo halitoshi kwa kukaa sote, tumekaa Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Waziri jengo moja. Naibu Katibu na Wakurugenzi wapo katika jengo la pili, Kurugenzi nyengine ipo jengo la tatu. Tukaona kwamba hivi sio hapa, tulikuwa tumeazimwa, wenyewe wanapahitaji, tumetafuta jengo la kutuchukua sote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa swali lake la pili, kwamba kwa nini musitumie jengo la Ubalozi wa Oman. Huu ni utaratibu wa serikali, wizara nyengine imeelekezwa kwenda kukaa hapo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa la tatu, anasema kwamba watu wanasumbuka na wananchi wanashuka wananchi, sio kwamba wananchi wetu lazima watumie bandari na hapo mashamba pia wapo, ndio hao hao Wazanzibari, sio lazima kwamba wawekewe mjini tu. Huko mashamba tulikokwenda Kisauni pia wapo, Wazanzibari ambao wanahitaji huduma za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, sio lazima kwamba mambo yote yabakie mjini.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilihisi labda alikuwa anatafuta utaratibu. Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimsifu Mhe.Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri yenye ufasaha. Katika majibu yake amesema kwamba wizara iliwatangazia wananchi kuhusu kuhamia Afisi zile za Kisauni, lakini swali langu ni kwamba Afisi zile za Kisauni zipo maeneo mbali na mjini, lakini Afisi zile katika majibu yake ameeleza kwamba zitakuwa ni za muda mfupi na ina mpango wa kurudia katika Afisi yake ya zamani. Je, itaendelea kwa muda gani kuhamia pale au itarudi katika Afisi yake ya jengo la zamani ambao linaendelea kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara hatuna nia wala hatuna mpango wa kutaka kurudi katika jengo la zamani. Hatuna nia wala sababu ya kurudi huko kwa sababu jengo lile sio mali zetu. Jengo lile la *Wakfu.* Kwa hivyo, tunaposema tunarudi kule, maana yake twende tukalipe kodi. Tunaacha sehemu ambayo hatulipi kodi, twende tukalipe kodi, maana yake haya matumizi mabaya ya raslimali ya nchi zetu. Kwa hivyo, sisi mipango yetu ni kuimarisha pale tulipopawe pazuri zaidi, wananchi wakija wazidi kufurahi zaidi katika huduma tunazozitoa.

Mhe. Mwenyekiti: Maelekezo au muongozo.

MUONGOZO

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nitumie fursa kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia hii fursa hii ya kuweza kupata muongozi wako.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imefanywa na visiwa viwili vikubwa, yaani Unguja na Pemba. Usafiri pekee ambao tunaumudu, watu tulio wengi ambao tunaudumu ni usafiri wa meli na meli pekee ambayo ni uhakika na kufanya safari zake Unguja na Pemba ni meli ya *MV. Sealink* inayomilikiwa na mfanyabiashara makini, mahiri na anayetujali Wazanzibari Bwana Said Salim Bakheressa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba michango iliyochangiwa na baadhi ya Waheshimiwa hapa juzi, ilimvunja moyo Bwana Said Salim Bakheressa na kusitisha ziara za meli zake baina ya visiwa hivi vya Unguja na Pemba, jambo ambalo sisi Wazanzibari tulio na maisha ya chini huku yalitushtusha mno, taarifa hizo tuliona kama radi iliyotupasukia mbele yetu bila ya kufanya wingu.

Mhe. Mwenyekiti, hii inayokuja ni Ramadhani, wajasiriamali wengi kutoka katika Kisiwa cha Pemba huja Unguja na biashara zao, wakulima wengi huja na mazao yao ili waweze kumudu kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na kujiongezea kipato. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuendelea kuzuia Said Salim Bakheressa meli yake ya *MV. Sealink,* sio tu kwamba kutatuzorotesha kimaisha, lakini hata kufanya vizuri ibada ya mfungo wa mwezi wa Ramadhani. Sasa katika hili, naomba muongozo wako ili serikali katika hili inatueleza nini serikali kuhusiana na suala zima la mfanyabiashara huyu anayetuonea huruma, lakini akakasirishwa na mambo haya? Munatwambiaje serikali kuhusu hili? Ataendelea au tunawaomba nyinyi serikali mumnasihi, mumliwaze na mumuombe aendeleze hizi safari zake ili walipa kodi tuweze kuishi vizuri katika nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, katika jambo ambalo Mhe. Mjumbe, alikuwa amelizungumza tayari serikali ilikwisha kujipanga na tulikuwa tunasubiri kipindi hichi cha maswali na majibu kimalizike na kiti kwa kutumia Kanuni ya 158 kitoe fursa kwa Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ili aweze kutoa kauli ya serikali juu ya kadhia hiyo ambayo ilikuwa umeizungumza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, bila ya kupoteza muda, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, ili atoe Kauli ya Serikali katika jambo hilo Mhe. Naibu Waziri, karibu.(*Makofi*)

KAULI YA SERIKALI

Kuhusu Meli ya Sea Link kusitisha safari zake kwa Visiwa vya Unguja na Pemba

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Naibu Waziri, ili tuweze kufahamu kile ambacho kimeulizwa. Naomba masikio yetu tumpe Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Waziri, tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa maelezo machache yanayohusiana na kadhia nzima ya suala la usafiri kati ya Unguja na Pemba. Kulingana na kipindi kinachotukabili cha kwenda katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo hayo, naomba pia uniruhusu nitumie nafasi hii kutoa maelezo kidogo ili kuweza kusawazisha yale maelezo ambayo yalikuwa yamezagaa mitaani pamoja na zile kauli ambazo zilikuwa zikisemwa kuhusiana na chombo ambacho kimeulizwa.

Mhe. Mwenyekiti, meli ya *Azam Sealink,* ni meli ambayo imetengenezwa nchini Ugiriki. Imetengenezwa mwaka 2011. Jina lake la asili inaitwa "*Protoporos V*". Kwa maana kwamba ilikuwa na *Sister ship* yake ambayo ni *Protoporos six.* Meli hii ilikuwa ikifanya safari zake za kawaida za kubeba abiria na magari, yaani mzigo kutoka katika Kisiwa cha *Evbia* kwenda katika Ugiriki kuu. Meli hii imekuwa *designed* kuchukua abiria na mizigo kwa utaratibu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, katika mwaka 2012, Kampuni ya *Azam Marine* ilifanye nia ya kutaka kununua meli hii. Kiutaratibu kwa mujibu wa maelekezo sheria Nam. 5 ya Usafiri Baharini inaelekeza kwamba kabla ya kununua chombo cha baharini, mmiliki anapaswa kushirikiana na mamlaka kwenda kukithibitisha chombo hicho.Wakati wa mmiliki alipokuja serikalini akaondoka na maafisa wetu kwenda nao Ugiriki kwenda kukagua chombo hicho, walikaa kwa muda wa wiki moja na kuthibitisha meli hiyo. Baada ya kuangaliwa meli ile ilipandishwa chelezoni nchini Ugiriki na kufanyiwa kipimo cha uzani ambacho wataalamu *inclining experiment* siku ya tarehe 13/05/2011 katika mji wa Malpos Volos.

Mhe. Mwenyekiti, kipimo hichi cha uzani kilifanywa na mtaalamu wa ujenzi wa meli, yaani *Naval Acted* ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ya nchi ya Ugiriki. Jina la mtaalamu anayeitwa Nikosozous Zapos. Vipimo vya meli hii vya awali urefu ilikuwa na urefu wa mita 99.65 ambapo baadhi ya *document* imeandikwa kwamba urefu wa 100. Lakini utaratibu huu kwa watu wote wa hesabu wanajua *point* ikiuka sita, saba unaweza ukaifanya kuwa ni moja. Kwa hivyo, kama kutatokea tofauti ya pahali paliandikwa mita 99.65, pengine pakisomeka mita 100, kitaalamu hakuna kosa. Upana, meli hii ilikuwa na upana wa mita 16.50. Kina cha chini, yaani *deep* ilikuwa na urefu wa mita 3.8, ndio *deep* ya kwenda chini na *draft* yake ni mita 2.75. Meli hii iliuzwa kwa Kampuni ya *Azam*

Marine tarehe 22/06/2012. Alinunua baada ya kuridhishwa na maafisa wa *ZMA* kwa mujibu wa sheria kwamba meli hii inaakisi kuja kufanya kazi nchini kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hofu kubwa iliyokuwa ikisemwa hapa ni kwamba meli hii imebadilishwa maumbile yake, imeongezwa idadi ya magari, imeongezwa idadi ya abiria, malengo ya serikali si mazuri, tunaruhusu mambo haya kiholela. Jambo hili si kweli. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu meli hii *modification* iliyofanyika, ilikuwa mwanzo ukiingia ndani ya meli uwasili wake, mkono kulia na mkono kushoto wa meli upande wa chini kulikuwa kuna *ramps, ramps* zile zimefutwa zimeekwa ngazi na upanda wa *ramp* umepunguzwa. Yale maeneo yote yaliyopunguzwa upana wa *ramp* vimeongezwa viti vya kukaa abiria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya *ramp*, kulikuwa kuna magari yanapoingia yanakaa *line*s mbili mbili, *line* moja ya kila upande imefutwa, vimeongezwa viti vya kukaa abiria. Juu kuna *decks* tatu, *same decks* zote zimerefushwa, mbili kuongeza viti vya kukaa abiria. Pamoja na vitu vile vya asili, mpango wake umepangwa vyengine ili kuweza ku-*squeeze* kuongeza abiria, lakini meli hii uwezo wake wa kitaalamu uzito, ulikuwa ujumla ni tani 607 kabla ya kufanya mabadiliko yale, yaani ilikuwa inachukua abiria 700 na magari 206. Baada ya kufanyika mabadiliko hayo tuliyoyasema meli hii sasa hivi inachukua abiria 1500 na inachukua mizigo, kwa maana kwamba magari 110.

Mhe. Mwenyekiti, idadi ya abiria 1,500 ukichukuwa tani juu yake ni sawa sawa na tani 150, kwa maana kwamba kila mtu ukimpa kilo 100 na magari haya tani yake sasa hivi uzito ni 315. Kwa hivyo, hivi sasa meli ile inachukua mzigo wa tani 420, kabla ilikuwa inachukua uzito wa tani 607. Kwa hivyo, mtu anaposema kwamba meli hii imeongezwa uzito inapakia mzigo mkubwa, mtu huyo sio mkweli anapotosha watu. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tunatambua hivi sasa dunia ni kijiji, kuna mabadiliko mengi yanayopatikana kupitia kwenye mtandao. Ni kweli kulikuwa kuna *document* hii ambayo imetolewa kwenye mtandao. *Document* hii ukienda katika utaratibu wa *AIS,* uki-*google* sasa hivi unaipata, ambapo *document* hii inaonesha uwasili wake na mabadiliko baada ya kufanyiwa *modification*. Kwa hivyo, kuja na *document* hii, haimaanishi kwamba wewe umekuja na *genuine document* ya kuikanusha serikali tunaposema kwamba mabadiliko yaliyofanywa kwenye meli hayakwenda kinyume na sheria. *Document* hii ni kuonesha tu uwasili wa meli na mabadiliko yake vipi yamefanyika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaikubali hii *document,* imo kwenye mtandao inayoelezea uwasili wa meli na mabadiliko yake, lakini ukiangalia taratibu za kupasisha meli ziko wazi kwamba unaweza kuwa na *State Booklet* yako ya asili, unapomaliza kufanya *inclining experiment* yule *Nather Archeture* amepewa mamlaka kisheria kutengeneza *State Booklet* nyengine. Kwa hivyo, *State Booklet* ya awali sio ambayo imepasishiwa, imepasishwa meli hii baada ya kuwa na *State Booklet* ya pili baada ya kufanyiwa *inclining experiment*. Kwa hivyo, unapokuja na *document* kama hii yenye kusimama katika *State Booklet* ya awalimu, taarifa za humu zimepitwa na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi, baada ya kupata majanga yale mwaka 2013 mapema tu, tulikuja na mabadiliko ya sheria, mabadiliko yale yameeleza wazi kwamba hakuna meli yoyote ya kubeba abiria itakayoruhusiwa kubeba abiria Zanzibar baada ya kufanyiwa mabadiliko, lakini jambo la msingi ni lazima tukumbuke kwamba mabadiliko yaliyozungumzwa kisheria yako wazi. Katika mabadiliko yale ya sheria tuliyoyafanya tuliongeza kifungu nambari 17(a).

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nikinukuu. Baada ya kufanya mabadiliko yale, tuliongeza kifungu Nam. 17(a) (1), kinachosomeka kama ninavyosoma, kinasema;

> "*No ship having more than 15 years for age, from the date its commission shall come to the registration and license for the purpose to carry passengers in Zanzibar*".

Kifungu Nam. 17(2);

> "*Any landcraft vessel which is not purposely built for carrying passengers from the fist construction shall not be registered or licensed for purpose of carrying passengers and cargo in Zanzibar*".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu Nam. 17(3), naomba ninukuu, maana hapa ndio kwenye msingi wa ninalotaka kulisema;

> *"No ship shall be registered in Zanzibar or licensed for purpose of carrying passengers in Zanzibar, if such ship has been modified for its original construction. For the purpose of this section, modification shall been, any modification to the ship structure from alteration of the main dimensions such as lank, bath, date or installing generators, transmitters, generators, crane, wallet of similar things".*

Mhe. Mwenyekiti, *modification* iliyokusudiwa hapa iko wazi kwamba umezungumzwa urefu, upana, kina, ama *generators* za awali za kuendeshea, yaani mfumo wa umeme wa asili wa meli husika.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia *document* hii ambayo ndio *document* ya asili iliyotafutwa kwenye mtandao, vipimo vilivyokuwemo humu vya urefu na *document* hii ambayo imepasishwa meli vipimo vilivyokuwemo humu viko sawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye *document* ya awali inasema kwamba urefu wake ni mita 96.65 katika *document* hii iko sawa sawa 96.65, urefu wa *beam* huku inazungumza 16. 5 na huku urefu wa *beam* unazungumza 16. 5, *date* 3.8 na huku inazungumza 3.8, *draft* huku inazungumza 2.75 na huku *draft* inazungumza 2.75. Kwa hivyo, hoja ya kusema mabadiliko haya yanai-*nalify* meli hii kwamba haistahiki kuchukua abiria, nayo pia hayana msingi. Mabadiliko yote hayo yaliyofanywa yameendana kwa mujibu wa sheria, hakuna hata kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, tena kwa meli zote zilizosajiliwa Zanzibar kama kuna meli ambayo serikali ilichukua jitihada na tahadhari kubwa katika usafirishaji wake ni meli hii.Ilichukua miezi mitatu kufanya mazungumzo ya kila hatua, serikali na mmiliki wa meli tukawa tunazungumza kitu kimoja. Pia, kwa kutambua kwamba hili ni jambo jipya na jambo geni kabisa katika usafiri wetu wa Zanzibar, mfumo wa roro serikali pia hatukukubali ku-*issure license* ya abiria wote 1,500 *at one*. Meli hii iliruhusiwa kuchukua watu 700 kwa kipindi cha miezi 9, baada ya kuona *Sealink* yake *buoyancy* yake, *central of gravity, there are other things*, serikali ikaruhusu kutoka abiria 1,200. Ikatembea kwa kipindi kisichopungua miezi sita, serikali ikawa imeridhika, ndio maana tukaongeza idadi ikafika 1,450.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, serikali tunaposema kwamba meli hii ina uwezo wa kuchukua abiria 1,500 ambao wako kihalali, meli inaruhusika kihalali haijazidishwa mzigo, kauli yetu hiyo ni kauli ya ukweli na haina chembe ya kupotosha. Sisi kama wizara na kama serikali hatutomvumilia mtu yeyote kutumia nafasi yake, utajiri wake au vyombo vyake kutaka kuwaangamiza wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia, hatutotumia ushawishi wa mtu yeyote kuona tunamkandamiza mwananchi mwengine anayetoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar. Tunatambua kuna ushindani wa biashara, ushindani huu uwe ni ushindani wa biashara tu na wala ushindani huu usitumike katika kuwapotosha wananchi katika huduma wanazozitaka. Nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu mno, tunaunga mkono, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi na Wazanzibar kwa ujumla, tumeridhika na maelezo ya serikali. Kwa hivyo, nawaomba Wawakilishi wote katika Baraza hili la Wawakilishi, waunge mkono haya maelezo na tumuombe Mfanyabiashara wetu Said Saleh Bakharesa aendelee kutoa huduma katika visiwa hivi kwa vyombo vyake vyote na sisi tunamuunga mkono. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambua uzito wa jambo lenyewe na kwa kutambua kipindi tunachokabiliana nacho cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, sisi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tumefanya jitihada za ziada kumtafuta mmiliki wa meli hii na kuweza kuzungumza na yeye. Jambo la shukrani mmiliki yule ni muungwana, msikivu na ametambua umuhimu wa safari zake na umuhimu wa huduma anazotoa kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, basi ameiruhusu meli yake kuendelea na utaratibu wa safari kwenda Pemba na kuanzia leo Jumatatu *route* ya Pemba ipo kama kawaida. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri, kutokana na kauli ya serikali ambayo tayari umeitoa na Mhe. Mjumbe, ambaye ulikuwa umetaka kupata muongozo juu ya suala hili, huu ndio muongozo wenyewe na tukiendelea Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuchukua fursa hii kuwatangazieni kwamba kwa siku ya leo tuna wageni ambao ni wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ni wanafunzi kutoka Skuli ya Fujoni, wanafunzi hao idadi yao ni 20 na walimu watatu. Nawaomba wasimame wanafunzi wa Skuli ya Fujoni katika Jimbo la Kitope, ili waweze kusalimiana na Waheshimiwa Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, vile vile, tulikuwa tuna wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Tunguu na wao nawaomba wasimame ili waonekane. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2014/2015
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa waraka wangu huu, lakini kabla sijaanza, naomba kutoa indhari kwamba nitakachokizungumza hapa ni muhtasari wa kitabu cha bajeti yangu. Naomba bajeti yangu yaliyoandikwa yote yajitokeze kwenye *Hansard*, ili kuweka *Hansard* na maelezo sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati, ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kwanza kumshukuru Mola Mtukufu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo nikiwa na afya na uzima ili kutoa hotuba yangu. Hiki ni kikao cha nne cha bajeti tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Moh'd Shein, kwa jinsi alivyokuwa karibu sana na Wizara yangu kwa kutupa miongozo na maelekezo ambayo yamechangia sana katika kuiendeleza sekta ya elimu. Vile vile, napenda kutoa Shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad (Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar) na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi (Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar) kwa michango yao ya mawazo na kuweza kutushauri wizara yetu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nawe pia nakushukuru na nakupa pongezi zangu za dhati kwa kutuwezesha na kutufikisha hapa tulipofika.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake ya Baraza la Wawakilishi ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kutuongoza vyema na kutushauri ipasavyo. Wajumbe wa Kamati hii waliweza kuichambua na kuijadili hotuba ya bajeti ya wizara yangu kwa undani kabisa na mwishowe kuipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, namshukuru kwa dhati kabisa msaidizi wangu, Mhe. Zahra Ali Hamad, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa juhudi zake, mashirikiano yake na nidhamu ya hali juu kwangu katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Aidha, napenda kuwapongeza watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa wizara yangu, wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi, maafisa wa ngazi mbali mbali za elimu, walimu na wafanyakazi wengine wote kwa kufanya kazi kwa nidhamu, bidii na ushirikiano. Pia, napenda kuzipongeza Taasisi za Elimu, zinazojitegemea, Baraza la Elimu, Bodi za Elimu za Mikoa, Wilaya na Kamati za Skuli kwa utendaji wao wa kazi ambao umechangia sana katika mafanikio ya wizara yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru kwa dhati kabisa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ushirikiano mkubwa iliyotupa katika mwaka 2013/2014. Kwa ujumla upatikanaji wa fedha ulikuwa wa wastani kwani hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014 jumla ya Tsh 1,637,000,000/= za kazi za maendeleo kutoka Serikalini zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 31.0 ya makadirio. Kwa upande wa kazi za kawaida, jumla ya Tsh 67,124,582,433/= zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 83.7 ya makadirio. Jadweli Nam. 9(a) na 9 (b) zinatoa uchambuzi zaidi. Ni matumaini yangu kwamba ushirikiano huu utaendelezwa na kudumishwa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imejumuika na wananchi wa Tanzania katika kuadhimisha sherehe za kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Sherehe hizo zilifana sana kwa mambo mbali mbali ya kimaendeleo. Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika ufunguzi wa majengo ya skuli, maonyesho ya kazi mbali mbali za elimu na katika siku ya kilele michezo ya halaiki iliyofanywa na wanafunzi ilichangia katika kuifanya sherehe hiyo ifane kwa kiwango cha juu.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida yangu, kabla ya kuelezea utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi cha mwaka 2013/2014. Naomba uniruhusu nieleze kwa ufupi mafanikio yaliyopatikana katika wizara hii kwa kipindi cha mwaka 2013/2014.

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imepata mafanikio kiasi kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita wa 2013/2014. Miongoni mwa mafanikio hayo ni :-

- Ujenzi wa skuli 3 mpya za sekondari za ghorofa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi umekamilika.Skuli hizo zimeanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari 2014. Ujenzi wa skuli za sekondari za Paje Mtule, Tunguu na Dimani unaendelea kwa hatua za mwisho baada ya Wizara kuvunja mkataba na mkandarasi wa awali na kutiliana saini mkataba na wakandarasi wengine watatu. Ujenzi wa skuli za sekondari za Kibuteni na Mkanyageni unaendelea na unatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha;

- Wizara imetilia saini Hati ya Maelewano na Serikali ya Falme ya Oman kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Utamaduni wa Kiislamu katika eneo la Chuo cha Kiislamu, Mazizini. Ujenzi huo umeanza na utakapokamilika utakuwa na msikiti, nyumba ya Imamu, madarasa 6, jengo la maktaba, maabara ya kompyuta na lugha, vyumba vya mikutano na vya semina;

- Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kidato cha Pili, imeongezeka kutoka 56.9 mwaka 2012 na kufikia 59.4 mwaka 2013. Kati ya wanafunzi 19,322, wa skuli za sekondari za Serikali waliofanya mtihani huo mwezi wa Oktoba 2013, wanafunzi 11,483 wamefaulu na kuchaguliwa kuingia kidato cha tatu mwaka 2014;

- Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne imeongezeka kutoka 53.1 mwaka 2012 na kufikia 66.5 mwaka 2013. Jumla ya Wanafunzi 130 walifaulu na kutunukiwa cheti cha daraja la I;

    - Jumla ya waombaji 6 wa nafasi za masomo ya elimu ya juu, wamefanikiwa kupata ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kutoka Serikali ya Oman kupitia programu ya *Oman Academic Fellowship (OAF)* kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na tayari wameshajiunga na vyuo kwa ajili ya masomo ya Shahada ya Uzamili (3) na Shahada ya Uzamivu (3). Pia, wanafunzi wengine 7 wamechaguliwa kwa masomo ya Shahada ya kwanza kupitia mpango huu, kati yao wanafunzi 3 wameondoka nchini hivi karibuni kwenda kuanza masomo ya Shahada katika nyaja ya mafuta na gesi, teknohama na sayansi nchini Marekani;

    - Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimeanzisha kozi ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) katika Lugha ya Kiswahili;

    - Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia inazalisha umeme wa nishati ya jua wa kutosha kwa matumizi yake;

    - Ubalozi mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China na India umetupatia nafasi 24 za mafunzo ya muda mfupi nchini China na India. Wafanyakazi mbali mbali wamefaidika na mafunzo yaliyotolewa katika nchi hizo;

- Jumla ya vitabu 711,050 vya kiada vya elimu ya msingi kwa madarasa ya kwanza hadi la nne vimechapishwa na kusambazwa katika skuli mbali mbali;

- Jumla ya skuli 174 za msingi zimepatiwa kompyuta na vifaa mbali mbali vya teknolojia ya habari na mawasiliano kupitia mradi wa TZ 21, Unguja na Pemba;

- Jumla ya vipando 170 vimenunuliwa na *SACCOS* za Elimu, Unguja (100) na Pemba (70) na kukopeshwa walimu mbali mbali; na

- Mashindano ya Mbio za nyika "*Elimu Cross Country"* yalifanyika kwa mwaka wa pili na kuwashirikisha wanariadha kutoka skuli mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa ufupi mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2013/2014, sasa naomba uniruhusu nieleze kuhusu shughuli mbali mbali zilizotekelezwa katika Idara moja moja na taasisi zinazojitegemea katika mwaka 2013/2014 na matarajio na malengo kwa mwaka 2014/2015.

Idara ya Sera, Mipango na Utafiti:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti ina majukumu ya kuandaa mipango ya maendeleo, kuratibu na kufuatilia rasilimali na misaada ya wahisani, kufanya mapitio ya tathmini ya sera, mipango na miradi mbali mbali inayotekelezwa na Wizara, kuratibu shughuli za utafiti wa kielimu na kusimamia ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa takwimu mbali mbali za kielimu kwa wadau.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2013/14:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ilipanga kutekeleza jumla ya miradi tisa ya maendeleo. Miradi hiyo imetekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali, Wananchi na Washirika wa Maendeleo. Jumla ya Tsh. 35,547,619,000/= zilitengwa kwa utekelezaji wa miradi hiyo. Kati ya fedha hizo Tsh.5,350,000,000/= ni za serikali, Tsh. 8,779,632,000/= ni ruzuku kutoka kwa wahisani mbali mbali wa maendeleo na Tsh. 21,417,987,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Benki ya Dunia.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya Tsh. 1,637,000,000/= za serikali zilitolewa ikiwa ni sawa na asilimia 31.0 ya makadirio. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, jumla ya Tsh. 6,223,274,932/= sawa na asilimia 20.6 ya makadirio zilipatikana. Utekelezaji halisi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mradi wa Upanuzi na Uimarishaji wa Huduma za Maktaba:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa, jumla ya Tsh. 400,000,000/= za SMZ kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Tawi la Maktaba Kuu Pemba. Hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya Tsh. 400,000,000/= za SMZ zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 100.0 ya makadirio. Kazi za ujenzi wa maktaba unaendelea katika ghorofa ya pili.

Mradi wa Uimarishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulikuwa na lengo la kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). Mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 850,000,000/= za SMZ na Tsh.2,240,921,000/= za *BADEA*. Hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya Tsh. 362,000,000/= za SMZ sawa na 43.0 ya makadirio zilipatikana. Aidha, kwa upande wa *BADEA*, Tsh. 250,618,572/= zilipatikana sawa na asilimia 11.2 ya makadirio. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Mkandarasi wa ujenzi, wa mkandarasi umeme na mzabuni wa vifaa vya kompuyta wamelipwa sehemu ya malipo yao; na

ii) Andiko la mradi kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) limeandaliwa na kuwasilishwa Tume ya Mipango Zanzibar.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya wananchi, SMZ, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (*SIDA*), *UNICEF*, *UNESCO*, *GPE* na *USAID*. Mradi ulitengewa jumla ya Tsh.1,000,000,000/= za SMZ na Tsh. 7,212,032,000/= kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 480 kwa kushirikiana na wananchi katika Wilaya tisa za Unguja na Pemba;

ii) Kufanya ukarabati wa majengo katika skuli 12 za msingi;

iii) Kuchonga madawati 10,000 na kuyasambaza katika madarasa mapya yaliyojengwa;

iv) Kuwapatia walimu mafunzo mbali mbali yakiwemo ya matumizi ya lugha ya Kiengereza kwa ajili ya kufundishia, mafunzo juu ya matumizi ya mtaala mpya wa ngazi ya msingi na mafunzo ya kufundisha katika mfumo wa elimu mjumuisho;

v) Kukamilisha ujenzi wa nyumba tatu za walimu; na

vi) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa TZ-21.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya Tsh. 175,000,000/= za SMZ zilipatikana sawa na asilimia 18.0 ya makadirio. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, jumla ya Tsh 2,881,271,948/= sawa na asilimia 40.0 ya makadirio zilipatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Jumla ya madarasa 163(Unguja 69, Pemba 94) ya skuli za msingi yamekamilishwa;

ii) Ukarabati wa majengo katika skuli za msingi za Kitogani, Nungwi, Kijini na Ole umefanyika;

iii) Jumla ya madawati 2,520, viti 346 na meza 344 yamechongwa na kusambazwa katika skuli mbali mbali. Aidha, Benki ya *NMB* ilitoa madawati 100 ambayo yalisambazwa katika skuli za Matetema, Kitope, Kinduni, Kipange na Donge Mtambile; na

iv) Ujenzi wa vyoo, minara na matangi ya maji na sehemu za kunawa mikono katika skuli 13 (Unguja 05 na Pemba 08) umekamilika. Pia, miongozo ya maji, afya na mazingira katika skuli imetafsiriwa kutoka Kiengereza kuwa ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha watumiaji kuwa na uelewa zaidi wa maudhui ya miongozo hiyo na hivyo, kuweza kuitumia ipasavyo.

Aidha, mafunzo juu ya matumizi ya miongozo hiyo yametolewa kwa wakufunzi wakuu (23), wakaguzi wa elimu na maofisa wa elimu ya msingi 50 (27 Unguja, 23 Pemba) na walimu wa skuli za msingi 44 (Unguja 20 na Pemba 24).

Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh 100,000,000/= za SMZ na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kuendeleza ujenzi wa uzio, kuzunguka eneo la Chuo cha Kiislamu Micheweni na kuanza maandalizi ya ujenzi wa uzio katika Chuo cha Kiislamu Mazizini; na

ii) Kuendeleza ukarabati wa majengo ya Chuo cha Kiislamu Micheweni yaliyopo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi tarehe 30 Mei 2014, hakuna fedha za SMZ zilizotolewa na hivyo, hakuna kazi zilizotekelezwa.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 500,000,000/= za SMZ na TSh. 1,529,906,000/= za *AfDB* na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha uandaaji wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wakufunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar na wakufunzi wa mafunzo ya amali;

ii) Kukamilisha mapitio na marekebisho ya mitaala ya mafunzo kwa wanafunzi wa vituo vya Elimu Mbadala;

iii) Kuchagua mshauri elekezi, kuandaa michoro ya ujenzi wa vituo vinne vya elimu mbadala na vituo vitatu vya mafunzo ya amali na kutangaza zabuni za ujenzi;

iv) Kuchagua mshauri elekezi wa kuandaa michoro ya ukarabati na utanuzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Chuo cha Utalii Maruhubi na ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na kutangaza zabuni za ujenzi; na

v) Kulipa sehemu ya fidia ya vipando kwa wananchi wa eneo la Kituo cha Mafunzo ya Kazi za Amali Vitongoji ambao mazao yao yaling'olewa wakati wa ujenzi wa Kituo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Meii 2014, jumla TSh. 92,000,000/= za SMZ zilipatikana sawa na asilimia 15.0 na TSh. 93,321,600/= zilipatikana za *AfDB* sawa na asilimia 6.1 ya makadirio. Utekelezaji ulikuwa hivi ifuatavyo:-

i) Uandaaji wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wakufunzi wa Mafunzo ya Amali umekamilika na taratibu za kutayarisha mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wakufunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar zinaendelea;

ii) Mihutasari ya kutolea mafunzo kwa wanafunzi wa Vituo vya Elimu Mbadala imepitiwa na kurekebishwa. Kazi ya kuandika mihutasari mipya ya masomo 11 imekamilika. Kazi ya kuandika vitabu vya wanafunzi vya masomo 11 pia imekamilika; na

iii) Wizara imetiliana saini mikataba na washauri elekezi wa kusanifu michoro kwa ajili ya ujenzi wa vituo vinne vya elimu mbadala (*Meccon Arch Consult Ltd*), vituo vitatu vya mafunzo ya amali (*New-tech Consulting Group*) na ukarabati na utanuzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Chuo cha Utalii Maruhubi na ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali (*On space Co Ltd*). Kazi za usanifu wa michoro zinaendelea.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 1,000,000,000/= za SMZ na Tsh. 17,647,160,000/= kutoka Benki ya Dunia na Badea na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa skuli za sekondari za Kibuteni na Mkanyageni.

ii) Kukamilisha ujenzi wa madarasa katika skuli nne za sekondari za wananchi;

iii) Kuchonga na kusambaza samani katika skuli za sekondari zilizokamilishwa kujengwa;

iv) Kujenga "*grills"* katika vyumba vya maabara vya skuli mpya za sekondari 16; na

v) Kukamilisha ujenzi wa skuli za Sekondari za Paje Mtule, Dimani na Tunguu na kujenga ukuta kuzunguuka skuli mbili mpya za sekondari kati ya skuli 16 zilizojengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya TSh. 347,000,000/= za SMZ sawa na asilimia 35.0 na Tsh. 1,777,839,236/= za wafadhili sawa na asilimia 10.1 zimepatikana. Utekelezaji ulikuwa ni kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa skuli ya sekondari ya Kibuteni umekamilika kwa asilimia 45 na ule wa Mkanyageni umekamilika kwa asilimia 75.;

ii) Ujenzi wa ghorofa ya pili ya skuli ya sekondari ya Donge unaendelea; na

iii) Ujenzi wa skuli za sekondari za ghorofa za Kiembe-samaki na Faraja (Wilaya Magharibi) umekamilika na skuli hizo zimeanza kutumika. Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Tunguu umekamilika, ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Dimani umefikia asilimia 95 na ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Paje-Mtule umefikia asilimia 98.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umetengewa jumla Tsh. 500,000,000/= za SMZ na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kuanza ujenzi wa dakhalia mpya ya skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja;

ii) Kuipatia skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja vifaa vya karakana; na

iii) Kuendelea na ukarabati wa majengo, kununua vifaa vya kufundishia na vitabu kwa ajili ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, hakuna fedha iliyopatikana na hivyo, hakuna utekelezaji uliofanyika.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 150,000,000/= za SMZ na Tsh. 1,567,600,000/= za *UNICEF* na *GPE*. Malengo ya mradi huu yalikuwa ni :-

i) Kuendelea kutoa mafunzo ya mtaala mpya kwa walimu wa elimu ya maandalizi;

ii) Kukamilisha ujenzi wa skuli za maandalizi za Jongowe na Konde;

iii) Kununua samani kwa skuli za maandalizi za Jongowe, Konde na Tunduni;

iv) Kuandika na kuchapisha moduli ya 4 na 5 kwa ajili ya kutolea mafunzo kwa wakufunzi wa walimu wa maandalizi kwa njia ya TEHAMA; na

v) Kununua vifaa vya kufundishia watoto wa vituo vya Tucheze Tujifunze.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya Tsh. 19,000,000/= sawa na asilimia 13.0 ya fedha zote za SMZ zilitolewa na kutumika. Kwa upande wa washirika wa Maendeleo jumla ya Tsh. 1,056,551,800/= sawa na asilimia 68.0 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa mradi ulikuwa kama ifuatavyo:-

i) Mafunzo ya mtaala wa somo la Kiengereza na Kiarabu yametolewa kwa walimu wa skuli za maandalizi za Serikali Unguja na Pemba;

ii) Ujenzi wa skuli ya maandalizi za Jongowe na Konde umekamilika kwa hatua zote na skuli hizo zimepatiwa samani za madarasani na ofisini;

iii) Uandishi wa moduli ya nne ya kutolea mafunzo ya wakufunzi wa walimu wa maandalizi kwa njia ya TEHAMA unaendelea; na

iv) Taratibu za zabuni za kununua vifaa vya kufundishia watoto wa vituo vya Tucheze Tujifunze zinaendelea.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi kwa Wilaya ya Magharibi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 850,000,000/= za SMZ na Serikali ya China ilikubali kujenga skuli moja ya msingi na ulikuwa na malengo yafuatayo :-

i) Kujenga skuli moja mpya za msingi;

ii) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 20 ya skuli za msingi yaliyoanzishwa na wananchi;na

iii) Kununua samani za skuli za msingi zilizojengwa.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Mei 2014, jumla ya Tsh. 25,000,000/= zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 3.0 ya makadirio. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa madarasa 21 umekamilika katika skuli za Kihinani, Kizimbani, Maungani, Kibweni na Welezo;

ii. Jumla ya madawati 210 na seti za meza na viti 14 zimechongwa na kusambazwa katika madarasa yaliyokamilishwa; na

iii. Ukarabati wa madarasa 04 ya skuli ya msingi ya Mwanakwerekwe “H” umefanyika.

Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara imepanga kutekeleza miradi sita yote ikiwa ni miradi inayoendelea. Kati ya miradi hiyo mmoja utatekelezwa kutokana na bajeti ya SMZ pekee na miradi mitano itatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Jumla ya Tsh. 3,300,000,000/= za SMZ, Tsh. 9,362,128,000/= ambazo ni ruzuku kutoka kwa washirika mbali mbali wa maendeleo na Tsh. 13,490,322,130/= ni mkopo kutoka Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na “*OPEC Fund for International Development*” zitatumika. Jadweli nambari 43 inatoa uchambuzi zaidi Malengo ya miradi mbali mbali itakayotekelezwa katika mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, mradi huu utaendelea kutekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ, *GPE* na *UNICEF*. Malengo ya mradi huu ni:-

i) Kuendelea kutoa mafunzo ya mtaala mpya kwa walimu wa elimu ya maandalizi;

ii) Kukamilisha ujenzi wa skuli za maandalizi za Kajengwa na Chambani na kuchonga samani zake;

iii) Kuwapa mafunzo wakufunzi wa walimu wa skuli za maandalizi kwa njia ya TEHAMA;

iv) Kuandika na kuchapishaji moduli ya 4 na ya 5 kwa ajili ya kutolea mafunzo kwa wakufunzi wa walimu wa maandalizi kwa njia ya TEHAMA; na

v) Kununua vifaa vya kufundishia watoto wa vituo vya Tucheze Tujifunze.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 100,000,000/= za SMZ na Tsh. 1,200,000,000/= za Washirika wa Maendeleo.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa kwa mashirikiano kati ya wananchi,Washirika wa Maendeleo wakiwemo *SIDA, UNICEF, UNESCO, GPE, OPEC Fund, Imperial College of Science and Technology (UK)* na *USAID*. Mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 240 (160 Unguja na 80 Pemba) kwa kushirikiana na wananchi;

ii) Kufanya ukarabati wa skuli 10 za msingi (6, Unguja na 4, Pemba);

iii) Kuchonga madawati 5,000 na kuyasambaza katika madarasa mapya yaliyokamilishwa kujengwa. Pia, kuchonga samani za jengo jipya la maktaba kuu tawi la Pemba;

iv) Kuanza taratibu za zabuni za kumpata mshauri elekezi wa ujenzi wa skuli 10 za msingi za ghorofa na kuandaa michoro ya ujenzi;

v) Kuimarisha miundombinu ya maji, afya na usafi wa mazingira katika skuli;

vi) Kuandika na kuchapisha vitabu vya kiada na miongozo ya walimu kwa masomo ya Kiengereza, Hisabati, *ICT*, Jiografia, Sayansi, Uraia, Historia, Michezo, Mafunzo ya Amali, Dini, Kiarabu na Kiswahili kwa madarasa ya V- VI;

vii) Kuanza kwa majaribio mpango wa upatikanaji wa chakula cha wanafunzi katika skuli 9;

viii) Kukamilisha ujenzi wa nyumba tatu za walimu; na

ix) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa TZ-21.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 1,000,000,000/= za SMZ na Tsh. 11,362,128,000/= za Washirika wa Maendeleo.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na *BADEA*. Kwa mwaka 2014/2015, mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa skuli za sekondari za Kibuteni na Mkanyageni;

ii) Kuchonga na kusambaza samani katika skuli za sekondari za Kibuteni na Mkanyageni. Pia, kununua vifaa vya maabara vya skuli hizo;

iii) Kuendeleza ujenzi wa skuli za sekondari za wananchi za Donge na Miwaleni; na

iv) Kujenga ukuta kuzunguka skuli za sekondari za Lumumba, Mpendae na Chwaka Tumbe.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umetengewa Tsh. 1,200,000,000/= za SMZ na Tsh. 3,411,006,260/= kutoka Badea.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee na utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kuanza ujenzi wa dahalia mpya ya wavulana katika skuli ya sekondari ya ufundi ya Kengeja; na

ii) Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umeme katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 300,000,000/=.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Kwa mwaka 2014/2015. Mradi utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha uandaaji wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wakufunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar na wakufunzi wa mafunzo ya amali;

ii) Kuhariri na kuchapa mitaala, vitabu vya wanafunzi na miongozo ya walimu wa vituo vya Elimu Mbadala;

iii) Kukamilisha taratibu za kupata wakandarasi na kuanza ujenzi wa vituo vitatu vya elimu mbadala na vituo viwili vya mafunzo ya amali;

iv) Kuanza ujenzi wa Vituo vya Elimu ya Amali na Mafunzo ya Kazi za Amali na ukarabati wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Maruhubi na kujenga makao makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;

v) Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani; na

vi) Kulipa sehemu ya fidia ya vipando kwa wananchi wa eneo la Kituo cha Mafunzo ya Kazi za Amali Vitongoji, ambao mazao yao yaling'olewa wakati wa ujenzi wa Kituo.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 700,000,000/= za SMZ na TSh. 6,879,315,870/= za *AfDB*.

Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, mradi huu utatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Serikali ya Oman na utakuwa na lengo la kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Utamaduni wa Kiislamu katika eneo la Chuo cha Kiislamu Mazizini. Ujenzi huu utagharimu Tsh. 13,255,496,100/43 ambazo Mkandarasi Kampuni ya *Exim Construction Ltd* atalipwa moja kwa moja na Serikali ya Oman. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachangia Tsh. 2,022,024,828/88 ikiwa ni gharama ya kodi ya ongezeko la thamani ya malipo ya mkandarasi.

Utafiti:

Mhe. Mwenyekiti, tafiti mbali mbali zimeendelea kufanyika katika kipindi hiki. Utafiti Mkuu wa Nne wa *SACMEQ* wenye lengo la kupima uwezo wa kusoma, kufanya Hisabu na uelewa katika taaluma ya *VVU* na UKIMWI kwa wanafunzi na walimu wa darasa la sita ulifanyika. Jumla ya Skuli 126 za Serikali na binafsi zilishirikishwa katika utafiti huu.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya skuli hizo 79 ni za Unguja na 47 za Pemba. Kila skuli ilitoa sampuli ya wanafunzi 25 na kutimiza jumla ya wanafunzi 3,150, walimu wakuu 126 na walimu wa masomo husika 480 walioshiriki kufanya utafiti huu. Taarifa za utafiti zimeingizwa katika programu maalum ya kompyuta na kuwasilishwa katika Taasisi ya Kimataifa ya Mipango ya Kielimu (*IIEP*) ambayo inaratibu kazi za *SACMEQ* kilichoko Paris.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, wizara ilifanya utafiti wa kutathmini hali ya kisomo cha watu wazima ili kubaini maendeleo na changamoto zinazokikabili kisomo hicho. Taarifa za utafiti huo zimeshafanyiwa uchambuzi na uandishi wa Rasimu ya mwisho ya ripoti ya utafiti huo unaendelea. Wizara pia imo katika hatua za mwisho

kukamilisha ripoti ya Tathmini ya maendeleo ya Miaka kumi (10) ya Elimu kwa Wote (*EFA-End of decade Assessment)*.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, wizara itaendelea na kazi ya uchambuzi wa taarifa za Utafiti Mkuu wa Nne wa *SACMEQ*. Ripoti ya utafiti huo inatarajiwa kukamilika mwezi wa Oktoba 2014. Ripoti itachapishwa rasmi na matokeo ya utafiti huo yatawasilishwa kwa wadau mbali mbali wa elimu wakiwemo walimu wakuu na walimu wa skuli zote za msingi za serikali na binafsi. Lengo kuu ni kuyajadili na kuyafanyia kazi matokeo ya utafiti na mapendekezo yatakayotolewa. Matokeo ya utafiti huu pia yataisaidia serikali katika kuandaa mipango ya kimaendeleo na kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha sekta ya Elimu nchini.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, wizara imepanga kuchapisha ripoti ya utafiti wa hali ya kisomo cha watu wazima na ripoti ya tathmini ya miaka 10 ya elimu kwa wote na kuyawasilisha matokeo ya tafiti hizo kwa wadau mbali mbali. Aidha, matokeo ya tafiti hizo yatawasilishwa *UNESCO* kwa lengo la kutumika katika tathmini ya malengo ya Milenia na Elimu kwa Wote ifikapo 2015.

Ukusanyaji na Uchambuzi wa Taarifa za Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, kazi za ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za elimu zimeendelezwa kwa ufanisi mkubwa. Takwimu zinakusanywa kutoka skuli zote za serikali na binafsi, Vyuo Vikuu, Vituo vya elimu Mbadala na Watu Wazima na vituo vya elimu ya Amali kwa Unguja na Pemba. Takwimu hizi hufanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kwa wadau mbali mbali wa elimu ili kuonesha maendeleo katika sekta ya elimu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi wa TZ-21, jumla ya skuli 248 za msingi za Unguja na Pemba zimepatiwa kompyuta mbili kwa kila skuli pamoja na programu ya kuweka na kuchambua takwimu za elimu (*Database*). Ofisi za takwimu za wilaya na vituo vya walimu pia zimepatiwa kompyuta. Aidha, Divisheni ya Takwimu ya Wizara Unguja imepatiwa "*Server computer*" pamoja na programu. Taratibu za kuipatia nyenzo kama hizo Divisheni ya takwimu ya Pemba zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imewapeleka masomoni watakwimu watano wa Wilaya kuhudhuria mafunzo ya ngazi ya Cheti katika Chuo cha Takwimu cha Dar-es-salaam. Watakwimu hao watakapomaliza mafunzo yao, watashirikiana na Wizara katika kuziimarisha takwimu za elimu katika wilaya zao. Wizara pia imewapatia mafunzo ya muda mfupi maafisa wake wote wa takwimu wa Unguja na Pemba, juu ya matumizi ya programu ya *SPSS* ambayo hutumika katika uchambuzi wa takwimu za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inashirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika kuandaa kitabu cha takwimu (*Statistical Abstract*) ambacho kina uchambuzi wa kina wa taarifa za kielimu za Zanzibar za kipindi cha miaka mitatu (2012 -2014). Taarifa hizo ni muhimu sana kwani zinaonesha hali halisi ya elimu, mafanikio na changamoto zake katika utoaji wa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, wizara itaendelea na kazi ya ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu pamoja na kuziwasilisha kwa wadau mbali mbali wa maendeleo ya elimu. Pia, mfumo mpya wa takwimu kwa ngazi ya msingi na sekondari utakamilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Wizara itaendelea kutoa kitabu cha mwaka cha takwimu za elimu (*Annual Statistical Abstract*), itatoa mafunzo zaidi kwa maafisa wa takwimu wa Wizara, wilaya na kwa watendaji wa vituo vya walimu. Aidha, Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika mbali mbali wa maendeleo ya elimu wa ndani na nje, wakiwemo *SIDA, GPE, USAID, OCGS, NGO's* katika kuimarisha ubora wa takwimu za elimu ili kuweza kupanga mipango sahihi na yenye uhakika kwa maendeleo ya elimu na Taifa kwa jumla.

Maendeleo ya Kisera:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, wizara imeitafsiri Sera ya Elimu 2006 kutoka lugha ya Kiengereza na kuwa ya Kiswahili, ili kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wake kwa wadau mbali mbali wa elimu. Kwa mwaka 2014/15, Wizara itafanya tathmini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu (*ZEDP*) kwa dhamira ya kuandaa mpango mpya wa maendeleo ya elimu kwa miaka ya 2016/2017 – 2019/2020. Wizara pia itachapisha

jumla ya nakala 500 za Sera ya Elimu iliyotafsiriwa na itawasilisha Sera hiyo kwa wadau mbali mbali wa elimu wakiwemo skuli binafsi, ili kujenga uelewa mzuri wa mfumo wa elimu wa Zanzibar.

Ufuatiliaji na Tathmini:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14. Wizara iliendelea na kazi ya ufuatiliaji na tathmini hasa katika miradi ya maendeleo na kuwasilisha taarifa hizo serikalini na kwa Washirika wa Maendeleo. Wizara iliwapeleka maafisa wake watatu Tanzania Bara kupata mafunzo ya muda mfupi ya ufuatiliaji na tathmini. Maafisa hao wanaendelea na kazi zao baada ya kupata mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, wizara itaendelea na ufuatiliaji wa kazi za kawaida na za maendeleo. Aidha, wizara itapeleka maafisa zaidi katika mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini, kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya mpango kazi wa wizara (2012/13 – 2015/16) na kuendesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini kulingana na mfumo huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 2,664,590,000/= kwa Unguja na Tsh 453,626,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii inahusika na masuala yote ya kiutumishi na uendeshaji, kusimamia sheria na Kanuni za kazi pamoja na maslahi ya wafanyakazi. Idara pia inahusika na shughuli za kuratibu safari zote kwa wafanyakazi wote ndani na nje ya nchi, utunzaji wa kumbukumbu za wafanyakazi pamoja na utunzaji wa majengo na ghala za vitabu na vifaa vyengine vya elimu. Idara pia inaratibu mafunzo mbali mbali ya wafanyakazi kulingana na mahitaji ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2014, wizara ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 13,972, kati yao wanawake 8,797 na wanaume ni 5,175. Wafanyakazi 10,185 wapo Unguja (wanawake 6,870 na wanaume 3,314) na Pemba wapo wafanyakazi 3,787 (wanawake ni 1,927 na wanaume 1,860). Kati ya wafanyakazi wote, 12,756 wamo katika kada ya ualimu na 1,216 ni wafanyakazi walio nje ya kada ya ualimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14, jumla ya walimu 235 (110 Unguja na 125 Pemba) waliajiriwa baada ya kupata kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini. Kati yao, walimu 176 ni wa ngazi ya Cheti, 33 wa Stashahada ya Sanaa, 02 Stashahada ya Sayansi, mmoja wa Shahada ya Sayansi na 23 wa Shahada ya Sanaa. Pia, Tume ya Utumishi Serikalini, hivi karibuni imetangaza nafasi za kazi za walimu wa ngazi mbali mbali. Aidha, katika jitihada za kuwaendeleza watumishi wake, wafanyakazi 963 kwa Unguja na 176 kwa Pemba walijiunga na vyuo mbali mbali kwa masomo katika ngazi tofauti kuanzia cheti hadi Shahada ya Uzamivu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/14, jumla ya wafanyakazi 137 walistaafu kazi kwa mujibu wa sheria. Wafanyakazi 20 walitangulia mbele ya haki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, *Amin.* Wafanyakazi 34 walipewa uhamisho wa kuendelea na kazi katika wizara na Taasisi mbali mbali na wengine 26 walichukuwa likizo bila ya malipo kutokana na sababu mbali mbali, watumishi 02 wametoroka kazini na 03 waliacha kazi kwa hiari zao. Pia, Wizara imewasilisha Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma maombi ya kujaza nafasi tupu zilizoachwa wazi na wafanyakazi waliostaafu na waliofariki dunia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwasaidia wafanyakazi kujikwamua kimaisha, Wizara yangu imewadhamini wafanyakazi 670 Unguja na 468 Pemba kupata mikopo ya fedha taslimu, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Mikopo yote ina thamani ya Tshs 1,297,238,000/=. Napenda kuchukua nafasi hii kuushukuru Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Posta, *CRDB*, *Barclays* na *SACCOS* zote kwa kuwapatia watumishi wa Wizara yangu mikopo ya aina mbali mbali. Nawaomba waendelee na kuwaunga mkono wafanya kazi wetu na nawaahidi kutoa ushirikiano mkubwa kufanikisha azma hii.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kuanzia mwezi Julai 2013, imefanya mabadiliko ya viwango vya maposho mbali mbali wanayolipwa Wakuu wa Vyuo vya ualimu, Walimu Wakuu na Wasaidizi, Maafisa wa Elimu wa Mikoa na Wilaya na Wakaguzi wa Elimu baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma. Vile vile, Wizara yangu imewalipa posho la likizo wafanyakazi 1,390 (wa 2012/13). Pia, imefanya marekebisho ya mishahara ya

wafanyakazi 570 waliorudi masomoni na wafanyakazi ambao mishahara yao ilikuwa na makosa. Hivyo, imewalipa wafanyakazi 1,465 wa Unguja na 97 kwa Pemba malimbikizo ya mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu itaendelea kuwaruhusu wafanyakazi kujiendeleza kwa mujibu wa mahitaji ya Wizara, kuwafanyia marekebisho ya mishahara na kuwalipa malimbikizo ya malipo ya mishahara na kuwapatia huduma ya likizo. Pia, Wizara inatarajia kuajiri wafanyakazi 794. Aidha, itaendelea kuwapatia fursa zaidi za masomo walimu na watumishi wengine ili waweze kumudu vyema kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wafanya kazi wake juu ya sheria na Kanuni za utumishi. Wizara pia itawafanyia mafunzo ya maandalizi '*Orientation*' waajiriwa wapya ili waweze kufahamu sheria, Kanuni na taratibu za kazi, mafunzo haya yatatolewa kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma (*IPA*).

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu itaendelea kuboresha '*Database*' ya wafanyakazi, kuandaa mpango wa rasilimali watu na kuwapatia vitendea kazi vya kutosha watendaji ili kuimarisha utendaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, Idara imepangiwa kutumia jumla ya Tshs. 2,613,800,000/= kwa Unguja na Tshs.1,399,958,000/= kwa Pemba, kwa kazi za kawaida.

Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi ina majukumu ya kusimamia utoaji wa elimu iliyo bora kwa ngazi ya maaandalizi na msingi pamoja na uratibu wa elimu ya vyuo vya Kurani na madrasa hapa nchini. Aidha, inasimamia skuli binafsi za maandalizi na msingi ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa na skuli hizo zinafuata mtaala ulioidhinishwa na wizara.

Elimu ya Madrasa na Vyuo vya Kurani:

Mhe. Mwenyekiti, Idara inaratibu shughuli za Madrasa/Vyuo vya Kurani 2,276 Unguja na Pemba. Aidha, zipo jumla ya skuli za maandalizi za madrasa za jamii 84 Unguja na Pemba zinazosimamiwa na kuhudumiwa kupitia '*'Madrasa Early Childhood Programme''* ambazo ufundishaji wake unafuata misingi ya dini ya Kiislam. Maafisa wa Idara, wamezitembelea Madrasa/Vyuo vya Kurani 108 na wahusika walipatiwa miongozo ya ufundishaji wa masomo yanayohusu dini ya Kiislam.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, walimu 60 wa vyuo vya Kurani katika Wilaya ya Kusini na Magharibi Unguja walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za kufundishia na ushiriki wa wanafunzi katika kujifunza.Kwa upande wa Pemba, mafunzo kama hayo yalitolewa katika Wilaya ya Mkoani na Micheweni kwa idadi ile ile ya walimu 60.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, wizara yangu inakusudia kutoa mafunzo kwa walimu 350 wa vyuo vya Kurani na Madrasa Unguja na Pemba. Pia, itaendelea kufanya ziara mbali mbali za kikazi katika vyuo hivyo.

Elimu ya Maandalizi:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, idadi ya skuli za maandalizi zilikuwa ni 279 kati ya hizo 244 za binafsi ambazo zina jumla ya wanafunzi 22,184 na skuli 35 za serikali zenye jumla ya wanafunzi 16,624. Jumla ya wanafunzi wote walioko katika ngazi hii ni 38,808 wakiwemo wanawake 19,154 na wanaume 18,630 ambayo ni sawa na asilimia 37.3 jadweli 12(a) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/14, wizara iliendelea na utaratibu wa kuzisaidia skuli vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kupunguza mzigo kwa wazazi kuchangia ununuzi wa vifaa hivyo. Vifaa hivyo ni pamoja na chaki, madaftari ya mahudhurio ya wanafunzi na manila ambavyo vimetolewa kwa baadhi ya skuli za

Maandalizi na Msingi zilizopo katika mazingira magumu. Wizara pia imetoa mafunzo kwa watendaji 48 wanaohudumia watoto katika skuli za maandalizi juu ya elimu ya afya, maji na usafi wa mazingira ili waweze kuwatunza vyema watoto hao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, wizara imekusudia kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu 250 kwa Unguja na Pemba ili kuwawezesha kuwa wataalamu wa kufundisha madarasa ya maandalizi. Wizara pia imekusudia kuimarisha maeneo ya kuchezea watoto katika skuli 30 za Unguja na Pemba. Pia, Wizara kwa kushirikiana na "*Madrasa Early Childhood Programme"* itawapatia mafunzo ya ualimu walimu 100 wa maandalizi ili watambulike rasmi kuwa walimu wa kufundisha watoto wa maandalizi.

Elimu ya Msingi:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Elimu ya Msingi inatolewa katika jumla ya skuli 359 zikiwemo skuli 270 za serikali na 89 za binafsi. Idadi ya wanafunzi katika ngazi hii imefikia 252,938 sawa na asilimia 102.5 ikilinganishwa na wanafunzi 247,353 sawa na asilimia 124.4 ya mwaka 2012/2013. Jumla ya wanafunzi 35,535 walioandikishwa kuanza darasa la kwanza katika skuli za serikali wamepatiwa nafasi.Miongoni mwa watoto hao 17,365 ni wanawake na 18,170 ni wanaume jadweli Nam. 13 inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi mbali mbali inaendeleza juhudi za kuwajengea wanafunzi mazingira bora, afya na usalama na mustakabali mwema ili waweze kujifunza vizuri. Katika kutekeleza mpango huo, jumla ya walimu 300 walijengewa uwezo wa namna ya kuziimarisha afya na mbinu mbali mbali za kufundisha madarasa ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ilifanya ziara za ufuatiliaji wa mafunzo yenye mikakati ya kumaliza Malaria Zanzibar kwa skuli 18 za Wilaya za Kati na Magharibi. Pia, yalitolewa mafunzo kwa skuli 54 juu ya maradhi ya kichaa cha mbwa. Aidha, Idara imefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wakuu 90 wapya (55 Unguja na 35 Pemba) na wale ambao hawajapata mafunzo ya uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeendelea kutoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kwa Maafisa wa elimu wa Wilaya na Mikoa na Maofisa wa Idara ili kuongeza uwezo na kuleta ufanisi zaidi katika kazi za ufuatiliaji wa kila siku. Pia, Idara imetoa mafunzo kwa walimu wakuu, Kamati za skuli na walimu washauri juu ya namna ya kudhibiti utoro katika skuli hasa kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Vile vile, Idara imetayarisha muongozo wa kumlinda mtoto ambao utatumika kwa skuli na taasisi nyengine za elimu. Hatua za kuchapisha muongozo huo, zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itaendelea kuzifanyia kazi changamoto mbali mbali zilizopo katika elimu kwa kuhakikisha msongamano wa wanafunzi madarasani unapungua, kupatikana kwa walimu wa kutosha na vifaa vya kufundishia kwa kadiri ya hali ya upatikanaji wa fedha itakavyoruhusu. Pia, Idara itaendelea kuhamasisha jamii kuwapeleka watoto wao katika skuli za maandalizi na msingi, kuendelea kuzisaidia skuli zilizoko katika mazingira magumu ya kiuchumi kwa kuzipatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 23,880,000,000/= kwa Unguja na Tsh. 6,622,694,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

Idara ya Elimu ya Sekondari:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Sekondari ina majukumu ya kusimamia utekelezaji kazi za ufundishaji kwa ujumla na ufuatiliaji wa utendaji kazi katika skuli, kupanga walimu katika skuli zote za serikali za sekondari na kuwapangia skuli wanafunzi waliofaulu katika ngazi mbali mbali za elimu, kufanya shughuli za uzalishaji mali na uwekaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi ya skuli, kufuatilia utendaji wa serikali za wanafunzi na huduma za dakhalia.

Idara ya Elimu ya Sekondari:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Sekondari ina majukumu ya kusimamia utekelezaji kazi za ufundishaji kwa ujumla na ufuatiliaji wa utendaji kazi katika skuli, kupanga walimu katika skuli zote za

serikali za sekondari na kuwapangia skuli wanafunzi waliofaulu katika ngazi mbali mbali za elimu, kufanya shughuli za uzalishaji mali na uwekaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi ya skuli, kufuatilia utendaji wa serikali za wanafunzi na huduma za dakhalia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/ 2014, elimu ya sekondari ilikuwa inatolewa katika skuli 256, kati ya hizo skuli 211 ni za serikali na 45 ni za binafsi. Skuli hizo zilikuwa na wanafunzi 81,757 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Kati yao wanaume ni 37,152 na wanawake ni 44,605. Katika ngazi ya Elimu ya Lazima (*F1-FII*) walikuwepo wanafunzi 52,183 ambao ni asilimia 71.1 ya watoto wenye umri wa miaka 14-15 wanaotarajiwa kuwepo skuli. Kwa upande wa kidato cha 3-6 walikuwepo wanafunzi 29,696 na michepuo, kidatu cha 1-4 walikuwepo wanafunzi 4,981. Jadweli Nam.19, 20 na 22 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Elimu ya Sekondari imetoa mafunzo ya miiko na maadili katika kazi ya ualimu, mafunzo ya uongozi kwa walimu wakuu na wasaidizi walimu wakuu wapya wa skuli 32 za Unguja. Aidha, Idara imetoa mafunzo ya ukutubi kwa walimu wa skuli 44 za Unguja na 40 za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya elimu ya sekondari imekusudia kutoa mafunzo kwa walimu wapya watakaoajiriwa. Pia, itatoa mafunzo ya uongozi kwa walimu wakuu wapya pamoja na wasaidizi walimu wakuu. Vile vile, Idara inakusudia kuendelea kutoa mafunzo zaidi kwa walimu ya *panel* za masomo ya Kiengereza, Hisabati na Sayansi, pamoja na utumiaji na utunzaji wa vifaa vya maabara kwa walimu wa masomo ya sayansi. Aidha, Idara itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa sayansi wa skuli 212 za sekondari ya awali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Elimu ya Sekondari inakusudia kuendelea kufuatilia shughuli za ufundishaji katika skuli na kuzipatia skuli vifaa mbali mbali vya kufundishia. Idara itanunua Kompyuta 20 kwa skuli za sekondari mbili zinazosomesha mchepuo wa Sayansi ya Kompyuta. Pia, itanunua vifaa vya maabara kwa ajili ya mazoezi katika masomo ya sayansi kwa skuli 100 za Unguja na Pemba. Aidha, Idara italipa gharama za Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na Sita kwa wanafunzi wote wa Skuli za Serikali, watakaofanya mitihani katika mwaka wa masomo 2014/2015.

Kazi za Ujasiriamali:

Mhe, Spika, Katika mwaka wa fedha 2013/2014, shughuli za Ujasiriamali zimeendelezwa katika skuli zetu. Skuli zetu nyingi zimekusanya mapato kutokana na miradi iliyobuniwa ambapo fedha zinazopatikana husaidia katika kutatua matatizo madogo madogo yanayozikabili skuli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itaendelea kutoa mafunzo ya Ujasiriamali katika skuli zetu ili kuzisaidia skuli kuongeza mapato na pia kuwajengea uwezo wanafunzi waweze kujiajiri wenyewe baada ya kumaliza masomo yao.Idara itaendelea kuzisaidia skuli kubuni miradi ambayo itasaidia skuli hizo kuweza kujitegemea.

Serikali za Wanafunzi:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, mafunzo yametolewa kwa viongozi wa serikali za wanafunzi kwa skuli 18 za Unguja.Serikali za wanafunzi katika skuli zimetekeleza majukumu yake kwa kiwango kinachoridhisha.Serikali hizo zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuwasaidia walimu kusimamia kazi za usafi wa skuli, kudumisha nidhamu za wanafunzi na kuwaandaa wanafunzi katika kazi za uongozi baada ya kumaliza skuli.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara itaendelea kuandaa mafunzo kwa viongozi wa serikali za wanafunzi kwa skuli za serikali na binafsi ili kukuza uwelewa wao.

Huduma za Dakhalia:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, idadi ya wanafunzi walioishi dahalia ilifikia 1,944 ambapo wanaume ni 1,123 na wanawake ni 821. Katika kuimarisha dahalia zetu, Idara imeandaa mikakati ya kuziendesha dahalia kwa ubora ili kuwawezesha wanafunzi waishi katika mazingira bora na salama. Mikakati hio ni pamoja na kupaka rangi dahalia ya wanawake Mazizini, kulipia deni la umeme na kununua vifaa vya usafi. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wazazi wa wanafunzi wanaoishi dahalia kwa kuendelea kuwahudumia watoto wao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inakusudia kuimarisha huduma za afya za wanafunzi wanaoishi dahalia kwa kuweka visanduku vya huduma ya kwanza na kuboresha mazingira ya dahalia hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 18,160,000,000/= kwa Unguja na Tsh. 7,805,270,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu ina jukumu la kusimamia matumizi sahihi ya *TEHAMA* katika kujifunza na kufundishia katika ngazi mbali mbali za elimu, kuimarisha huduma ya mawasiliano na usalama wa taarifa, kuratibu na kutoa mafunzo ya *TEHAMA* kwa walimu na watumishi wengine wa Wizara na kuandaa programu mbali mbali za kompyuta ambazo zitaongeza ufanisi wa shughuli za Wizara.

Sera ya *TEHAMA* katika Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Idara imekamilisha mikutano ya kujadili Rasimu ya sera ya *TEHAMA* katika elimu na wadau wa elimu na ya Washirika wa Maendeleo. Uandishi wa Rasimu ya tatu ya sera hiyo umekamilika na hatimae itawasilishwa katika ngazi mbali mbali za serikali kwa ajili ya kuthibitishwa kabla ya kutumika rasmi.

Utekelezaji wa Mradi wa (TZ -21):

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 elimu ya msingi imeendelea kuimarishwa kupitia *TEHAMA* chini ya mradi wa "TZ-21 *Century Basic Education*" kwa utunzi wa vitabu vya kuwashajihisha watoto kupenda kusoma. Jumla ya vitabu 5 vyenye maudhui mbali mbali vimetungwa na walimu wetu, jambo linaloonesha ukomavu na kupungua utegemezi kutoka nje.

Kuimarisha matumizi ya *TEHAMA* katika kujifunza na kufundishia:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, jumla ya walimu 1,097 wamepatiwa mafunzo ya awali ya kompyuta, kati yao 516 wanawake na 581 wanaume. Kwa upande wa watendaji wa Wizara, watumishi 55 wakiwemo wanawake 27 na wanaume 28 wamepatiwa mafunzo kwa mujibu wa shuguli zao za kila siku.Pia, Idara imefanya ukaguzi wa vifaa na matumizi ya *TEHAMA* katika skuli za Unguja na Pemba. Jumla ya skuli 80 Unguja na 141 Pemba zilikaguliwa ili kujua uelewa wa walimu katika fani ya *TEHAMA*, vifaa viliopo na kama vinatumika ipasavyo katika kujifunza na kufundishia.

Mhe. Mwenyekiti, Idara iliendelea na kazi ya kutayarisha vipindi vya elimu kwa njia ya redio vijulikanavyo kama "Tucheze Tujifunze" (*TUTU*) kwa kuzingatia mihutasari mipya ya elimu ya maandalizi. Jumla ya vipindi 21 vya *TUTU* na 21 vya darasa la kwanza na la pili vimerushwa kupitia *ZBC*. Vile vile, jumla ya vituo vipya 50 vya "Tucheze Tujifunze" vimeanzishwa, 25 katika Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja na 25 Wilaya ya Mkoani kwa Pemba. Kutokana na kuanzishwa kwa vituo hivyo, hivi sasa vipo vituo 230 vyenye wanafunzi 7,265. Pia, wasaidizi 100 wapya watakaoviendesha vituo hivyo wamepatiwa mafunzo.

Kuimarisha njia za Mawasiliano na Usambazaji wa Taarifa kupitia *TEHAMA:*

Mhe.Spika, Wizara imeanza kutumia mkonga wa Taifa kwa mawasiliano katika Makao Makuu ya Wizara Unguja na hatua za ufungaji kwa upande wa Ofisi Kuu ya Elimu Pemba zinaendelea. Pia, baadhi ya Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu ikiwemo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo cha Kiislamu, Mazizini Unguja na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia zimeanza kufungiwa vifaa hivyo. Lengo ni kuhakikisha kuwa taasisi zote za elimu Unguja na Pemba zinatumia huduma hii kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itaandaa Mpango Mkakati wa Sera ya *TEHAMA* katika elimu, itaendelea kuziunganisha taasisi za elimu na mkonga wa Taifa, kutoa mafunzo ya *TEHAMA* kwa walimu 50 na watendaji wengine 20 wa Wizara, kuendeleza elimu ya maandalizi kwa njia ya *TEHAMA*, kutayarisha programu mbali mbali za kompyuta kwa mashirikianao na Idara husika ili kuimarisha utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 350,600,000/= kwa Unguja na Tsh. 115,511,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kuondoa tatizo la kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wananchi, kuwapatia elimu mbadala vijana walioacha masomo njiani na wale ambao hawakubahatika kuandikishwa kabisa pamoja na kuwaendeleza kielimu wale wote wenye nia ya kufanya hivyo.

Kisomo:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, juhudi za kuhamasisha wananchi ambao hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu, kufungua na kujiunga na madarasa ya kisomo pamoja na kuyaendeleza yale yaliopo zimefanyika na kufanikiwa. Idara ina jumla ya wanakisomo 8,438 kati yao 6,607 wamefanyiwa upimaji katika hatua zote nne. Katika upimaji huo wanakisomo waliofaulu ni 5,290. Kati ya hao, wanakisomo wa hatua ya nne 586 (wanawake 491 na wanaume 95) wamekombolewa, yaani wamemaliza na kufaulu katika hatua ya mwisho. Jumla ya madarasa 7 mapya yakiwa na wanakisomo 108 kati ya hao wanawake ni 101 na wanaume 7 yamefunguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara itaendelea kushajihisha na kuhamasisha wananchi ambao hawajui kusoma na kuandika kufungua na kujiunga katika madarasa ya kisomo.Pia, itafungua na kuziendeleza maktaba za kisomo kwa kuzipatia nyenzo stahiki zikiwemo vitabu na wakutubi wenye sifa.

Elimu Mbadala:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, elimu mbadala imetolewa katika madarasa 30 (Unguja 19 na Pemba 11) yenye jumla ya wanafunzi 678 (Pemba 288 na Unguja 390), kati ya wanafunzi hawa wanawake ni 189 na wanaume ni 489.

Mhe. Mwenyekiti, kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo, kina jumla ya vijana 305 wanawake 73 na waume 232, wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22. Vijana hawa wanasoma masomo ya kawaida. Pia, wanafundishwa masomo ya fani mbali mbali zikiwemo ushoni, upishi, umeme, uchongaji, mafunzo ya kompyuta na utunzaji nyumba.Vile vile, kituo kimetumika kwa shughuli mbali mbali za semina na warsha mbali mbali kuhusiana na maradhi ya malaria, uzazi wa mpango, unyanyasaji wa kijinsia, *VVU* na UKIMWI na shughuli nyengine za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo kimeshatoa wahitimu wa fani mbali mbali 3,095 tokea kuanzishwa kwake wakiwemo wanaume 2,158 na wanawake 937 ambao wametunukiwa vyeti. Fani zitolewazo katika kituo bado zina nafasi katika soko la ajira, wengi wa vijana hawa wameweza kuajiriwa katika taasisi mbali mbali binafsi na wengine wamejiajiri wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara inakusudia kupanua wigo mpana zaidi wa uhamasishaji mjini na vijijini ili kuweza kuongeza idadi ya vijana kujiunga na madarasa ya elimu mbadala katika skuli za msingi na pia kuongeza wanafunzi katika kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo.

Vituo vya Kujiendeleza:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, jumla ya wanafunzi 3,032 (wanawake 1,524 na wanaume 1,508) wamesajiliwa katika vituo mbali mbali vya kujiendeleza Unguja na Pemba.Wanafunzi 1,344 wamefanya mtihani wa faragha wa Kidato cha Nne na wanafunzi 734 wamefaulu sawa na asilimia 54.61 ya watahiniwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara inakusudia kufungua vituo vingi zaidi vya kujiendeleza katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu na itahamasisha vijana walioshindwa mitihani yao ya Kidato cha Pili na Nne wajiendeleze. Pia, Idara imeanzisha mpango maalum wa majaribio katika Wilaya ya Mjini wa kuwawezesha vijana kimaisha unaojulikana kwa jina la "*Youth Empowerment of Life Program*" (*YELP*). Vijana hawa ni wale waliomaliza Kidato cha Pili na cha Nne na hawana shughuli maalumu za kufanya. Vijana hawa wamepatiwa mafunzo ya lugha ya Kiengereza, Ujasiriamali, Fani ya umeme na Utunzaji wa nyumba. Vijana 109 (wanawake ni 53 na wanaume 56) wamemaliza na kufaulu mafunzo yao.

Programu za Wanawake:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ina jumla ya vikundi 55 vya ushirika vya akina mama.Vikundi hivi vinajishughulisha na shughuli mbali mbali za uzalishaji mali ikiwemo kilimo, ufugaji, ususi, biashara ndogo ndogo na ufinyazi. Vikundi 12 vimepatiwa msaada wa vyerehani vinne na mafunzo juu ya mbinu za Ujasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inakusudia kuendelea kuviimarisha zaidi vikundi hivyo kwa kuvipatia mafunzo, nyenzo na vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kuvizawadia vikundi ambavyo vitafanya vizuri zaidi.Pia, itayashajihisha madarasa ya kisomo ambayo bado hayajafungua vikundi vya programu za wanawake kufanya hivyo.

Vyombo vya Habari:
Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/ 2014, Idara imeweza kurusha hewani vipindi 20 vya redio.Vipindi hivyo vilikuwa na maudhui ya kuhamasisha wanajamii ambao hawajui kusoma na kuandika ili kujiunga na madarasa ya kisomo, kuhamasisha vijana walioacha masomo na wale ambao hawakuandikishwa kujiunga na madarasa ya elimu mbadala. Vipindi hivi pia vinahamasisha vijana waliomaliza elimu ya lazima kujiunga na madarasa ya kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara itaendelea kuwaelimisha wananchi na wanakisomo kwa kutumia vyombo vya habari, vipeperushi, makala, majarida, makongamano na michezo katika sherehe za Juma la Elimu ya Watu Wazima, pamoja na kuzitumia maktaba zilizopo mjini na vijijini ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tshs. 671,000,000/= kwa Unguja na Tsh. 185,501,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

Idara ya Mafunzo ya Ualimu:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kusimamia mafunzo ya ualimu vyuoni na mafunzo ya ualimu kazini. Mafunzo ya ualimu hutolewa katika vyuo vya ualimu vitatu ambavyo ni Chuo cha Kiislamu Mazizini, Chuo cha Kiislamu Kiuyu na Chuo cha Benjamin William Mkapa Pemba. Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Sanaa Sekondari, Stashahada ya Sayansi Sekondari, Stashahada ya Ualimu Msingi, Stashahada ya somo la Dini na Kiarabu na Cheti cha Ualimu wa Elimu Mjumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, vyuo vya ualimu vilikuwa na jumla ya wanafunzi 775 (wanaume 201 na wanawake 574). Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 71 (wanawake 66 na wanaume 5) ni wa mafunzo ya Cheti cha Ualimu wa Elimu Mjumuisho katika Chuo cha Kiislamu Mazizini. Jadweli Nam. 29 (A)-(C) zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo wa kitaalamu wakufunzi wa vyuo vya ualimu, Idara iliwapeleka wakufunzi wawili katika Taasisi ya Elimu Tanzania *TIE* kwa lengo la kujifunza mbinu za kufundisha kwa kutumia mitaala ya umahiri *Competence Based Curriculum*. Pia, *FAWE* Zanzibar iliwadhamini wakufunzi watatu kushiriki mafunzo mafupi juu ya mbinu za kufundisha kwa kuzingatia jinsia *Gender Responsive Pedagogy* nchini Kenya. Wakufunzi hao watawafundisha wakufunzi wenzao mbinu walizojifunza ili zitumike katika mafunzo ya ualimu.

Mhe. Mwenyekiti, Ujenzi wa Kituo cha Utamaduni wa Kiislamu, unaogharimiwa na Serikali ya Oman umeanza katika eneo la Chuo cha Kiislamu Unguja hapo Mazizini. Kituo hicho kitakuwa na msikiti, nyumba ya Imamu, jengo la maktaba, maabara ya lugha na kompyuta na vyumba vya semina. Pia, Chuo kimepokea msaada wa shillingi milioni 50 kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa msingi wa jengo la ukumbi wa mitihani. Aidha, Chuo kimeanzisha mkahawa ambao unatoa huduma kwa wanafunzi na walimu na kuwapunguzia shida ya kufuata huduma hiyo nje ya chuo.

Vituo vya Walimu:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara imeendesha mafunzo ya ualimu kwa njia ya elimu masafa katika vituo tisa vya walimu vya Unguja na Pemba. Jumla ya walimu 501 (wanaume 56) na (wanawake 445) wamesajiliwa kwa mafunzo ya cheti daraja la *IIIB* katika mkupuo huu. Huu ni mkupuo wa nne unaotegemewa kuwamaliza walimu wote waliokuwa hawajasomea ualimu.

Mafunzo Kazini:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara imekamilisha Rasimu ya kwanza ya Sera ya Mafunzo ya Ualimu Kazini. Idara pia imeendesha mafunzo kazini kwa walimu wa masomo mbali mbali ikiwemo Sayansi ambapo walimu 1,039 walishiriki, walimu 2,000 wa lugha ya Kiengereza wa ngazi ya msingi na walimu 150 wa sekondari. Pia, walimu 16 walipatiwa mafunzo ya lugha ya Kiengereza na mbinu za kufundisha kwa njia ya mtandao (*Online study*) yaliyosimamiwa na Ubalozi wa Marekani.Vile vile, walimu saba na mkaguzi mmoja wa elimu walishiriki mafunzo ya ufundishaji wa masomo ya Sayansi yaliyotolewa na *SMASSE* huko Nairobi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/15, Idara itaendesha mafunzo kuhusu mpango bora wa kuendesha skuli *Whole School Development Planning* kwa walimu wakuu wa skuli za msingi na sekondari. Idara pia itashirikiana na Idara ya *ICT* kuendesha mafunzo ya elimu ya maandalizi kwa walimu wa msingi wataosomesha madarasa ya maandalizi. Jumla ya walimu 250 watahusika na mpango huu.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wafanyakazi watatu wamepelekwa masomoni. Wafanyakazi 2 wamejiunga na Chuo cha Utumishi wa Umma kwa mafunzo ya cheti na mmoja amejiunga na masomo ya cheti cha ukutubi katika Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/15, Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 1,058,160,000/= kwa Unguja na Tsh. 761,790,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ina jukumu la kuzikagua skuli zote za Serikali na binafsi za Zanzibar, kuwakagua walimu mmoja mmoja wa masomo na kuwapa ushauri na maelekezo walimu hao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ilipanga kuzikagua skuli 342 zikiwemo skuli 255 za Serikali na 87 za binafsi, kati ya hizo, 239 za Unguja na 103 za

Pemba. Jumla ya skuli zilizokaguliwa ni 293 sawa na asilimia 86. Kiwango hiki kinatokana na kupatikana usafiri wa uhakika na nyenzo nyengine za ofisini.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu ilipata wakaguzi wanane wapya. Pia, ilinunua vespa 20 chini ya ufadhili wa Sida, kati ya vespa hizo 8 zilipelekwa Pemba na 12 zilibakia Unguja. Katika kujiendeleza kielimu wakaguzi wawili wanaendelea na mafunzo ya Diploma, watatu wanaendelea na mafunzo katika ngazi ya Shahada, saba katika Shahada ya Uzamilii na wawili na watatu wanakusudia kujiunga na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu. Pia, mfanyakazi mmoja anahudhuria mafunzo ya Stashahada ya "*Record management*".

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu imepanga kuzikagua skuli 376. Miongoni mwa skuli hizo 163 ni za Pemba na 213 za Unguja. Vile vile, kati ya hizo skuli 96 ni za binafsi na 280 ni za Serikali. Pia, Ofisi itakamilisha mchakato wa kupata sheria ya kuanzishwa kwake. Pamoja na hayo, Ofisi inakusudia kuwaelimisha wasaidizi walimu wakuu 200 ili waweze kuelewa na kutumia kwa ufanisi viwango sanifu vya elimu katika kazi zao. Pia, itanunua samani, kompyuta na kupitia vitini (*tools*) ambavyo hutumika katika ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 86,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Taasisi ya Elimu Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Zanzibar ina majukumu ya kutayarisha mitaala, mihutasari, utungaji na uchapishaji wa vitabu na usanifu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Taasisi ya Elimu Zanzibar, iliandaa viwango vya kujifunza kwa elimu ya msingi kwa madarasa ya 5 na 6. Vile vile, ilifanya utafiti wa uchambuzi wa mahitaji ya kuandaa mtaala wa cheti kwa walimu wa maandalizi. Pia, Taasisi iliandaa muongozo wa mtaala wa mafunzo kazini ya wasaidizi wa maabara wa skuli za sekondari. Aidha, ilifanya utafiti juu ya sababu za matokeo mabaya ya mitihani kwa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa skuli za msingi. Pia, Taasisi iliratibu uandishi wa uchapishaji wa vitabu vya elimu ya msingi kwa madarasa ya 1-4 vya masomo ya Kiswahili, Sayansi Jamii, Kiengereza na Hisabati. Baadhi ya sababu zilizogundulika katika utafiti huo ni ukosefu wa vitabu na vifaa vya kufundishia, uhaba wa walimu na matumizi ya mbinu zilizowashirikisha wanafunzi katika kujifunza.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Taasisi imepanga kuendesha mafunzo kwa walimu wa sekondari wa sayansi namna ya kutumia vifaa katika kufundisha masomo ya Sayansi.Vile vile, itafuatilia na kusimamia matumizi ya vifaa katika ufundishaji na uendeshaji wa maabara katika skuli za sekondari.Aidha, itafanya utafiti juu ya sababu za matokeo mabaya ya mitihani kwa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa skuli za sekondari

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Taasisi, itakamilisha uandishi wa sheria ya kuanzishwa kwake na itaandaa mpango mkakati. Pia, itatayarisha vifaa vya kufundishia masomo ya Sayansi, Hisabati, Sayansi Jamii, Kiswahili na Kiengereza kwa madarasa ya 1 - 4. Pia, itatayarisha vitabu vya masomo ya Dini, Kiarabu na Michezo kwa madarasa ya 1 - 4, pamoja na vifaa vya kufundishia masomo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Taasisi itatayarisha mtaala wa mafunzo ya walimu wa maandalizi kwa ngazi ya cheti. Vile vile, utaratibu uandishi na uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili, Kiengereza, Jiografia, Uraia, Historia, Hisabati, Sayansi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Michezo, Dini, Kiarabu na Mafunzo ya Amali kwa madarasa ya 5 na 6. Aidha, Taasisi itahariri na kuchapisha vitabu vya Kiswahili, Hisabati na Sayansi kwa watoto wa skuli za maandalizi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi imepangiwa ruzuku ya Tsh. 94,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali:

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inaendelea na kuendeleza majukumu yake yote kusimamia na kuratibu shughuli zote za Elimu na Mafunzo ya Amali hapa Zanzibar. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya wanafunzi 580 wanapatiwa mafunzo ya amali katika vituo vitatu vya Serikali vya Mkokotoni, Mwanakwerekwe na Vitongoji. Kati yao 183 ni wanawake na 397 ni wanaume.Vituo hivyo vinatoa mafunzo ya fani mbali mbali za ufundi zikiwemo Useremala, Ushoni, Uhunzi, Upishi, Uchoraji na Uandishi wa alama,Uashi,Ufundi Bomba, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Huduma za Chakula na Vinywaji, Elektroniki, Ufundi Magari, Umeme na Ufundi Mafriji na Viyoyozi. Jadweli Namba 37 (a) linatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka itaratibu Mitihani ya Taifa ya uhasibu na biashara (*NABE*), mitihani ya ufundi stadi "*Trade Test*" na "*Competency Based Education and Training" (CBET)* ya Tanzania Bara. Jumla ya vijana 850 walifanya mitihani hiyo. Kati yao vijana 601 walifaulu ikiwa sawa na asilimia 70.7.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014, Mamlaka imeendelea kusajili vituo vinavyotoa mafunzo ya amali vya Zanzibar vya umma na binafsi. Jumla ya vituo vya amali 25 vimekaguliwa na 10 kati yao vimesajiliwa. Jadweli namba 37 (b) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka itaendelea kuvisajili vituo vinavyotoa Mafunzo ya Amali, kuajiri wafanyakazi wa vituo, walimu na Maafisa ufuatiliaji na tathmini pamoja na kununua vitendea kazi vya divisheni mpya ya Ufuatiliaji na Tathmini. Mamlaka pia itasimamia na kutoa elimu juu ya taratibu za upatikanaji wa mikopo kwa wahitimu na mafunzo ya ujasiri amali. Mamlaka inakusudia kujenga uzio katika vituo vya Mwanakwerekwe na Mkokotoni, kuongeza mashirikiano baina ya Vituo vya Zanzibar na nje ya Zanzibar na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Mwaka 2005 na sheria namba (8) ya mafunzo ya Amali ya mwaka 2006 kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 11 ya 2007.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imepangiwa ruzuku ya Tsh. 1,1750,000,000/=

Taasisi za Elimu ya Juu:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, zilikuwepo jumla ya taasisi nne za elimu ya juu. Kati ya hizo, mbili zinamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Taasisi ya Karume na Sayansi na Teknolojia. Pia, zipo taasisi binafsi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani na Chuo Kikuu cha Zanzibar.

Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kimetimiza miaka 12 tangu kuanzishwa kwake na kina jumla ya wanafunzi 2,078 na kinafundisha programu 23, kati ya hizo 3 za Cheti, 8 za Stashahada, 9 za Shahada ya kwanza, 2 za Shahada ya Uzamili na 1 ya Shahada ya Uzamivu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2013/2014, Chuo kimeanzisha Skuli ya Tiba na Sayansi ya Afya ambayo imeandikisha wanafunzi 34.Vile vile, chuo kimeanzisha Stashahada ya Utalii na Mambo ya Kale, Stashahada ya Ukutubi, Shahada ya kwanza ya Historia, Shahada ya Teknohama na Menejimenti. Pia, Chuo kimeanzisha Shahada ya Uzamili ya Kemia na Shahada ya Uzamili ya Afya ya Mazingira. Jadweli namba 25 (a) linatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, skuli ya Kiswahili na lugha za Kigeni ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar imeanzisha kozi ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) ya lugha ya Kiswahili na wanafunzi 8 wamejiunga na kozi hiyo. Pia, kwa mwaka wa masomo 2013/2014 jumla ya wanafunzi wageni 163 (wanaume 105 na wanawake 58) wamejiunga na masomo ya Kiswahili kwa wageni.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kilifanya mahafali ya 9 tarehe 28 Disemba 2013. Katika mahafali hayo Mkuu wa Chuo ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein aliwatunuku Shahada, Stashahada na vyeti wahitimu 749, kati yao wanaume 331 na wanawake 418 katika fani mbali mbali. Miongoni mwao, wanafunzi 224 walitunukiwa Shahada ya Sanaa ya Elimu, wanafunzi 30 walitunukiwa Shahada ya Sayansi ya Elimu, wanafunzi 11 walitunukiwa Shahada ya Sayansi ya Kompyuta. Vile vile, wanafunzi 272 walitunukiwa Stashahada ya lugha na elimu, wanafunzi 15 walitunukiwa Stashahada ya Sayansi ya Kompyuta na wanafunzi 22 walitunukiwa Stashahada ya Teknolojia ya Habari na wanafunzi 30 walitunukiwa Stashahada ya Uongozi wa Elimu na Utawala.Aidha, wanafunzi 55 walitunukiwa vyeti vya ukutubi na 60 vyeti vya Teknolojia ya Kompyuta.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Chuo kulishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuandaa siku ya Utafii na ubunifu. Vile vile, Chuo kilishiriki katika maonesho ya taasisi za Serikali yaliyofanyika katika Kampasi ya Chuo huko Nkrumah. Aidha, Chuo kilishiriki katika mdahalo wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu na kiliandaa vipindi vya *TV* na makala katika magazeti. Chuo kiliandaa mkutano wa kwanza wa Bodi ya washauri wa *SUZA* ambapo mbali ya shughuli nyenginezo zilizopangwa Bodi ilimchagua Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilal kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015,Chuo kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuimarisha shughuli za kitafiti na machapisho kwa kuwajengea uwezo wanataaluma;
- Kuboresha elimu kwa vitendo kwa wanafunzi kwa kuwaandalia mihadhara ya watu maarufu wenye uzoefu katika taaluma husika;
- Kuimarisha majengo ya Kampasi ya Tunguu kwa kuweka vipoza hewa, kutengeneza kituo cha afya, kukarabati mkahawa na kuweka kituo cha polisi;
- Kukarabati majengo ya kampasi za Vuga na Nkrumah kwa kuimarisha miundombinu yake na kuweka vipoza hewa;
- Kuendelea kuwapatia mafunzo ya ndani wafanyakazi wake;
- Kuendelea na kuunganisha *SUZA* na taasisi za Chuo cha Sayansi za Afya, Chuo cha Uongozi wa Fedha na Chuo cha Utalii;
- Kujenga uwezo na kuimarisha matumizi ya Teknohama kwa kufanyia kazi za wanafunzi;
- Kuendelea kuchukua wanafunzi wapya katika fani na viwango mbali mbali;
- Kuanzisha programu mpya za Shahada ya Utalii, Shahada ya Uzamili ya Kiswahili, Shahada ya "*Mobile Computing and Web Design"*,Shahada ya Mawasiliano na mitandao, Shahada ya Sayansi na Teknolojia ya Habari na Ualimu. Vile vile, *SUZA* kwa kushirikiana na Chuo cha *ESAMI* kitatoa Shahada ya Uzamili ya Biashara (*MBA*); na
- Kuongeza masomo ya taaluma ya muda mfupi kama vile masomo yanayohusika na mafuta na gesi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimetengewa ruzuku ya Tsh 5,050,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia:

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ni Taasisi inayotoa huduma za kielimu za uhandisi katika ngazi ya Stashahada (NTA4 – NTA6). Taasisi ina jukumu la kuendeleza na kuikuza elimu ya uhandisi, sayansi na teknolojia hapa Zanzibar. Mafunzo ya uhandisi yanayotolewa ni Uhandisi mitambo, Uhandisi magari,Uhandisi ujenzi na usafirishaji, Uhandisi Mawasiliano ya anga, Elektroniki na kompyuta na Uhandisi umeme.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi ina jumla ya wafanyakazi 100, kati yao 79 ni wa kudumu. Pia, kuna wafanyakazi ambao si wa kudumu wakiwemo wakufunzi 6 wa muda, wafanyakazi 13 wa mkataba na 2 kutoka Wizara ya Fedha. Taasisi ya Karume ina jumla ya wanafunzi 1,308 (wanawake 250, wanaume 1,058). Kati ya wanafunzi hao, 277 (64

wanawake, 213 wanaume) ni wa ngazi ya NTA 4 – NTA 6, 70 (23 wanawake, 47 wanaume) ni wa Stashahada ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na 961 (163 wanawake na 798 wanaume) ni wa mafunzo ya amali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi ya Karume ilikamilisha malengo yafuatayo :-

- Idara 6 za taaluma ziliimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kufundishia;
- Mihutasari ya Idara zote ilipitiwa na kuombewa kibali cha usajili wa Idara hizo kutoka NACTE;
- Mpango kazi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo 2014/2018 ulipitiwa upya;
- Kukamilisha zoezi la uhakiki wa thamani kwa mali zake; na
- Kupunguza gharama za matumizi ya umeme kwa kufunga na kutumia nishati ya umeme wa jua.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Taasisi imejiwekea kutekeleza malengo makuu sita ili kufikia malengo ya mpango kazi wa miaka mitano. Malengo hayo ni kama yafuatayo :-

- Uendelezaji wa ukarabati majengo yake;
- Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia;
- Kuongeza mashirikiano na taasisi rafiki za elimu;
- Kuanzisha mafunzo mapya ya kuiendeleza kutumia Taasisi na yale ya kuisaidia jamii kwa Sayansi na Teknolojia;
- Kuanzisha shughuli za utafiti;
- Kuendeleza wakufunzi na wafanyakazi wa Taasisi ya Karume;
- Kuanzisha mafunzo ya Cheti na Stashahada ya walimu wa ufundi; na
- Kuanzisha mafunzo ya Ujasiriamali kwa wahitimu kutoka katika vyuo mbali mbali (*business incubator*) ili waweze kujiajiri mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi hii imetengewa ruzuku ya Tsh 1,056,600,000/= kwa kazi za kawaida.

Chuo Kikuu Cha Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Chuo Kikuu cha Zanzibar kilikuwa na jumla ya wanafunzi 2,584 kati yao wanaume ni 1,196 na wanawake 1,388. Kati ya hao wanafunzi 53 wanasoma Shahada ya Uzamili ya Sheria na Shari‘a, 140 wanasoma Shahada ya Uzamili ya Biashara, 27 Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Umma na wanafunzi 39 wanasoma Shahada ya Uzamili ya Uchumi.

Aidha, wanafunzi 1,821 wanasoma katika Shahada za kwanza katika fani za Biashara na Fedha, Masoko, Teknolojia ya Mawasiliano ya Kibiashara, Manunuzi, Sheria na Shari’a, Uchumi, Utawala wa Umma, Huduma za Jamii, Teknolojia ya Mawasiliano na Elimu, Benki ya Kiislamu, Lugha na Elimu, Uhandisi wa Simu, Uhandisi wa Kompyuta na Teknolojia na Uuguzi.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wanafunzi 504 wanasoma katika ngazi za Stashahada na Cheti katika fani za benki ya Kiislamu na Fedha, Uhandisi wa Habari na Mawasiliano, Teknolojia ya Mawasiliano, Uhusiano wa Kimataifa, Haki ya Mtoto, Upangaji na Uendeshaji wa Miradi na Teknolojia ya Mawasiliano ya Kibiashara Jadweli Na 27. linatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kina jumla ya wahadhiri 47 wazalendo na 9 kutoka nje ya Tanzania. Wahadhiri watatu wamemaliza masomo yao ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) na wengine watatu bado wanaendelea na masomo yao ya Shahada ya Uzamivu katika nchi za nje, wakati wanne wanaendelea na masomo katika ngazi hiyo hapa hapa nchini. Lengo likiwa ni kupata wahadhiri wa kutosha wenye sifa za juu kuweza kusomesha katika ngazi mbali mbali na kupunguza utegemezi wa wahadhiri kutoka nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo Kikuu cha Zanzibar kinatarajia kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la Hosteli ya wanawake ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya huduma za dahalia. Pia, chuo kitaanza ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la utawala ili kuendana sambamba na maelekezo ya Kamisheni ya Vyuo

Vikuu vya Tanzania. Aidha, chuo kinatarajia kuongeza uwezo wa maabara zake za kompyuta kulingana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi.

Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Chukwani:

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Zanzibar kimeimarika zaidi katika kukuza taaluma kwa kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi na wafanyakazi wake. Katika mwaka 2013/2014, Chuo kina jumla ya wanafunzi 1,880 wakiwemo wanawake 1,173 na wanaume 707. Wanafunzi 1,696 wanasomea Shahada ya kwanza ya ualimu na 184 wapo katika mafunzo ya matayarisho ya kujiunga na Shahada ya kwanza katika mwaka 2014/2015. Jadweli Nam. 26 inatoa ufafanunizi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2013/2014, Chuo kimekamilisha ununuzi wa kompyuta na ujenzi wa nyumba za kuishi wafanyakazi. Aidha, Chuo kimeifanyia matengenezo maktaba yake na kuibadilisha ili itoe huduma kwa njia ya *"Electronic".* Ukumbi huo mpya utachukua wanafunzi 50 kwa wakati mmoja na chumba kimoja kidogo kimetengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa masomo 2013/2014, jumla ya wanafunzi 265 wakiwemo wanawake 134 na wanaume 131 walihitimu masomo yao katika fani mbali mbali.Katika kuwaendeleza wahadhiri wake, Chuo kimeandaa mipango mbali mbali ya mafunzo, Wahadhiri wawili wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu katika masomo ya Sayansi, mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam na mwengine nchini Uturuki. Pia, Chuo kimeandaa mipango ya kuwaendeleza wahadhiri wake walio na sifa za Shahada ya kwanza ili wapate Shahada ya pili na wale wenye Shahada ya pili waendelee na masomo ya Shahada ya Uzamivu (*Ph.D*).

Mhe. Mwenyekiti, mipango ya kuwajengea uwezo wahadhiri wa Chuo inakwenda sambamba na malengo ya Chuo ya kuwa Chuo Kikuu kamili badala ya kuwa Chuo Kikuu kishiriki. Chuo kimeshakamilisha taratibu za kuwa Chuo Kamili chini ya mwongozo wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*) na inatarajia kupata kibali cha kukifanya Chuo hiki kiwe Chuo Kikuu kinachojitegemea kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa masomo 2014/2015, Chuo kinatarajia kusajili wanafunzi 700 wa fani mbali mbali za Shahada ya mwanzo. Pia, Chuo kinatarajia kuanzisha masomo ya ngazi ya Cheti na Diploma ya Ualimu. Chuo pia kitaanzisha mradi wa upatikanaji wa maji safi na salama, programu ya Shahada ya uzamili Kiarabu (Sheria ya Dini ya Kiislam) na utayarishaji wa michoro ya jengo jipya la kiwanda cha uchapaji.Vile vile, Chuo kitaendelea kuwasaidia walimu na wanafunzi wa Sayansi katika Skuli ya Sekondari ya Chukwani na skuli ya Sekondari ya Al-Ihsani. Aidha, Chuo kitaendelea kudumisha uhusiano mwema kati ya viongozi na wananchi wa Chukwani pamoja na maeneo ya jirani.

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu:

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni chombo kilichopewa jukumu la kuwapatia mikopo ya gharama za elimu wanafunzi na wafanyakazi wanaojiunga na masomo katika vyuo vya elimu ya juu. Aidha, Bodi hiyo pia imepewa jukumu la kukusanya madeni kuanzia mwaka 2006 kutoka kwa wanafunzi waliohitimu masomo yao na kuanza kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Bodi iliwapatia mikopo wanafunzi wapya 1,410, kati ya hao 1,028 wamejiunga na masomo katika vyuo vya ndani ya Zanzibar, 370 vyuo vya Tanzania bara na 12 ni vyuo vya nje ya Tanzania. Pia, Bodi imewalipia ada ya masomo na posho la kujikimu wanafunzi 153 wanaoendelea na masomo katika vyuo vya nje ya Tanzania, wanafunzi 906 wanaoendelea na masomo kwa vyuo vya ndani ya Zanzibar na 354 kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo Tanzania Bara. Jumla ya wanafunzi waliohudumiwa na Bodi ya Mikopo kwa mwaka 2013/2014 ni 2,823. Jadweli namba 24 (a) na 24 (b) zinatoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2014/2015, Bodi inakusudia kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya 1,000. Idadi hiyo ni ndogo ukilinganisha na wanafunzi 1,410 waliolipiwa mwaka 2013/2014. Kiwango hicho kimetokana na ruzuku inayopatiwa Bodi ya Mikopo kupungua.Vijana 354 wanatarajiwa kumaliza masomo yao mwaka huu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeendelea na kazi ya ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kutoka kwa wahitimu wa Taasisi za Elimu ya juu waliopatiwa mikopo. Hadi kufika tarehe 30 Mei, 2014, jumla ya T.Sh. 166,500,000/= zimekusanywa kutoka kwa wanafunzi 361 waliohitimu masomo yao na kuajiriwa katika sekta mbali mbali za serikali na binafsi. Kiwango hicho ni kikubwa ukilinganisha na makusanyo ya T.Sh. 105,167,000/= kilichofikiwa katika mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Bodi inakusudia kuongeza kasi ya ukusanyaji wa marejesho ya madeni hadi kufikia lengo la makusanyo ya Tsh. 350,000,000/=. Baadhi ya mbinu zitakazotumika ni pamoja na kuzitaka Wizara na Taasisi za Serikali kutowaruhusu wafanyakazi wao wenye madeni kwenda masomoni katika ngazi ya juu mpaka wahakikiwe na Bodi ya Mikopo na kuwataka wadhamini wa waliopewa mikopo kurejesha mikopo ya waliowachukulia dhamana ambao hadi sasa wameshindwa kurejesha mikopo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Bodi imepangiwa ruzuku ya T.Sh 8,792,400,000/= kwa ajili ya udhamini wa wanafunzi wapya na wanaoendelea pamoja na gharama za uendeshaji.

Baraza la Mitihani la Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mitihani lina jukumu la kusimamia shughuli zinazohusu mitihani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo utungaji, uchapishaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya elimu ya msingi na Stashahada ya Dini na Kiarabu. Baraza pia lina jukumu la kutathmini mwenendo mzima wa malengo ya utoaji elimu na mwenendo wa mitihani hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14, jumla ya wanafunzi 25,385 walifanya mtihani wa Darasa la Saba kutoka skuli za msingi 241 (147 Unguja na 94 Pemba). Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 91 waliteuliwa kujiunga na madarasa ya vipawa vya juu, ambao ni sawa na asilimia 0.35 na wanafunzi 1,347 sawa na asilimia 5.3 walifaulu na kuchaguliwa kuingia madarasa ya michepuo katika skuli mbali mbali za Zanzibar. Wanafunzi waliobakia wameendelea na masomo ya kidato cha kwanza katika skuli za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wanafunzi 19,322 kutoka skuli 194 (120 Unguja na 74 Pemba) walifanya Mtihani wa Kidato cha Pili. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 11,483 sawa na asillimia 59.4 walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu. Kiwango hiki cha ufaulu kimepanda kwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2012 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa 56.9. Jadweli namba 6(a) (i) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, wanafunzi 12,443 wa skuli za Serikali na binafsi walifanya mtihani huo. Kati ya yao, wanafunzi 8,110 wamefaulu ikiwa ni sawa na asilimia 66.5. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa wa Kidato cha Nne kimepanda kwa asilimia 13.4 ikilinganishwa na matokeo ya 2012 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa 53.1. Aidha, kati ya wanafunzi waliofaulu, 2,598 (wanawake 1,382 na wanaume 1,215) wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika skuli za Serikali mwaka 2014/2015, wakiwemo 2,057 kutoka skuli za Serikali, 243 wa skuli za binafsi na 298 wanafunzi wa faragha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mitihani ya Ualimu, walimu wanafunzi 260 walifanya mtihani wa Stashahada ya Ualimu wa masomo ya Dini na Kiarabu na Stashahada ya Elimu ya Msingi katika Chuo cha Kiislamu Mazizini, Chuo cha Kiislamu Kiuyu na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa, Mchanga Mdogo. Kati ya hao, walimu wanafunzi 196 sawa na asilimia 75.4 walifaulu na 60 ambao ni sawa na asilimia 23.1 watarudia mitihani yao.

Mhe. Mwenyekiti, Mitihani ya Taifa ya kidato cha sita imefanyika tarehe 04 – 16 Mei 2014. Jumla ya wanafunzi 1,288 wa skuli za Serikali na binafsi wameandikishwa kufanya mtihani. Matokeo ya mtihani huu yatatolewa baada ya taratibu za kusahihisha na kutayarisha matokeo kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Mitihani lilitoa taaluma kwa walimu, wanafunzi, wasimamizi, watungaji na wachapishaji mitihani kwa lengo la kudhibiti uvujaji na udanganyifu unaoweza kutokea kabla na baada ya kufanya mitihani. Hali hii ilipelekea kupungua kwa kesi za udanganyifu. Utaratibu huu utaendelea ili kupata mitihani yenye viwango na inayokubalika kuwapima wanafunzi.Baraza linapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wale wote walioshirikiana na watendaji wake katika kufanikisha shughuli zote za uendeshaji wa mitihani mwaka 2013.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2014, Baraza litaandaa Mtihani wa Kidato cha Pili wa pamoja kwa watahiniwa wote wa Kidato cha Pili wa skuli za sekondari za Serikali na za binafsi. Kabla ya hapo Baraza lilikuwa likiendesha mitihani kwa watahiniwa wa skuli za serikali tu na wanafunzi wa skuli za binafsi walikuwa wakifanya mitihani kwa kuzingatia ratiba ya skuli husika. Kwa mwaka huu 2014/2015 usajili wa wanafunzi utafanyika kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Baraza limeamua kutumia mfumo huu ili kusajili wanafunzi kwa usahihi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha misingi ya ufanisi wa uendeshaji mitihani, Baraza limekusudia kuajiri washauri wa masomo 11 watakaosaidiana na watendaji wa Baraza katika kuhakikisha maswali yanatungwa kwa kuzingatia mitaala inayofundishwa na yana uwiano na kiwango cha elimu cha watahiniwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza limekusudia kuendelea kuimarisha taratibu za usimamizi wa mitihani ya SMZ, ikiwemo kuweka kumbukumbu zote za wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mtihani katika mfumo wa kompyuta na kuongeza udhibiti wa mitihani hiyo. Aidha, Baraza litaendelea kuandaa mpango mkakati utakaosaidia kukuza ufanisi wa shughuli zake za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza limetengewa ruzuku ya Tsh. 1,590,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Bodi ya Huduma za Maktaba:

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba ina jukumu la kuanzisha, kusimamia na kusambaza huduma za Maktaba katika sehemu zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika limeendelea na juhudi mbali mbali za kufikisha huduma za maktaba katika skuli mbali mbali. Jitihada hizo zimepelekea kuongezeka kwa idadi ya skuli zilizomo katika mradi wa maktaba za sanduku kutoka skuli 35 mwaka 2012/2013 na kufikia 45 mwaka 2013/14. Pia, Shirika linaendelea na programu maalum ya watoto ndani ya Maktaba Kuu Unguja na Pemba.Aidha, kwa mwaka 2013/2014, Shirika limeandaa utaratibu wa kuwafuata watoto katika skuli zao, hali ambayo imesaidia sana kujenga hamasa ya kupenda kusoma vitabu na machapisho mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika limeandaa mpango wa kuziimarisha maktaba za skuli. Lengo kuu la mpango huo ni kuwapatia taaluma sahihi walimu juu ya namna bora ya kutoa huduma za maktaba kupitia maktaba za skuli, lakini pia, kuziimarisha maktaba za skuli ili kuwa muhimili imara katika kukuza maendeleo ya elimu nchini. Aidha, jumla ya walimu 160 kutoka skuli za Wilaya za Kaskazini ‘A’ Kusini, Chake Chake na Mkoani walipatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa maktaba.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika pia limeanzisha utoaji wa huduma za maktaba kwa kupitia njia ya mtandao ili kuwawezesha wanachama hususan wanataaluma kupata taarifa mbali mbali zinazohusiana na taaluma zao. Aidha, kwa kushirikiana na Ubalozi wa Marekani, Shirika limeanzisha huduma ya *‘‘American Corner’’* katika Ofisi kuu ya maktaba Unguja ambapo huduma za mtandao zimeimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Shirika linatarajia kupanua huduma zake zaidi sehemu za mjini na vijijini. Ili kufikia lengo hilo, Shirika limekusudia kuendesha programu za *‘‘Mobile library’’* na *‘‘Reading tents’’*, kuongeza skuli 10 katika mradi wa maktaba za sanduku katika Wilaya ya Wete Pemba. Pia, inakusudia kuendelea kuishajihisha jamii kujenga tabia za kujisomea na kupenda kutumia huduma za maktaba kwa watoto nchini kote. Vile vile, itaendelea kuihamasisha jamii kwa njia za mijadala ya wazi, makongamano, semina, mikutano na warsha mbali mbali ili kuweza kuielewesha juu ya haja ya kutumia huduma za maktaba kwa lengo la kuinua jamii na kujitambua kupitia machapisho mbali mbali. Aidha, Shirika litatayarisha Rasimu ya Sera ya Maktaba nchini.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Shirika la Huduma za Maktaba limetengewa jumla ya Tsh. 380, 000,000/= kwa kazi za kawaida.

Kitengo Cha Uhasibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Kitengo kimesimamia ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na malipo ya huduma mbali mbali wanazostahiki wafanyakazi ikiwemo nauli za walimu na huduma za likizo.Kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kimesimamia ulipaji wa fedha za wakandarasi na wazabuni wa ujenzi na wazabuni wa vifaa na huduma mbali mbali.Kitengo kimekuwa na mashirikiano na Wizara ya Fedha katika matumizi ya mtambo wa *IFMS* ambao husaidia kwa kiwango kikubwa usimamizi wa matumizi kwa mujibu wa bajeti ya Wizara na hivyo, kuimarisha udhibiti wa fedha za umma. Pia, Kitengo kimeweka kumbukumbu za matumizi ya fedha kwa utaratibu uliokubaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kitengo kitaendelea kusimamia matumizi yote ya fedha za kawaida na fedha za maendeleo kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa. Aidha, Kitengo kinakusudia kuimarisha kazi za utayarishaji wa ripoti za fedha za robo mwaka pamoja na ufungaji wa hesabu za Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, Kitengo kitawasilisha ripoti ya hesabu hizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya 45,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2013/14, Kitengo hiki kiliendelea na majukumu yake ya kuratibu shughuli za utoaji wa habari sahihi za elimu na kuendeleza mawasiliano na vifaa mbali mbali. Maelezo zaidi yatapatikana katika ibara ya 163 mpaka 164.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kitengo kimetengewa kutumia jumla ya shilingi milioni 45,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Kitengo cha Ununuzi na Ugavi:

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo hiki ndio Sekretarieti ya Bodi ya Zabuni ya Wizara. Katika kutekeleza kazi zake, Kitengo kiliendelea kushirikiana na Bodi ya Zabuni katika kutayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini Zabuni mbali mbali zilizotangazwa. Jumla ya Zabuni 35 za wizara na manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi zenye thamani ya jumla ya shilingi milioni 11,708,096,953/= zilitangazwa na kufanyiwa tathmini.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/15, Kitengo kinakusudia kutayarisha, kutangaza na kuzitathmini Zabuni za washauri elekezi, wakandarasi wa ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa mbali mbali. Pia, Kitengo kitatangaza Zabuni za kutafuta watoa huduma wengine kwa kazi mbali mbali za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Kitengo kinatarajia kutumia jumla ya Tshs.45,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani:

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kuu la Kitengo hiki ni kukagua mapato na matumizi ya hesabu zote za Wizara, Idara na Taasisi zake zikiwemo skuli. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kitengo kilikuwa na lengo la kukagua skuli 200 za Unguja na Pemba kwa. Hata hivyo, Kitengo kiliweza kukagua jumla ya skuli 103 (62 Unguja na 41 kwa Pemba) sawa na asilimia 52 ya malengo. Kitengo pia kimekagua hesabu za fedha za matumizi ya kawaida na zile za maendeleo kwa asilimia 50.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kitengo kitaendelea kufanya ukaguzi wa mahesabu ya Taasisi na Idara zote za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Katika kuongeza ufanisi, Kitengo kitaendelea na utaratibu wake wa kutoa mafunzo ya uwekaji wa kumbukumbu za hesabu na uwekaji wa rekodi za vitabu kwa Wenyeviti wa Kamati za skuli, walimu wakuu na washika fedha wa skuli. Lengo ni kuwajengea uelewa kuhusiana na kazi zao. Pia, Kitengo kimejipangia kukagua skuli 220 kati ya hizo skuli 140 kwa Unguja na 80 kwa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kimepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 45,000,000/= kwa ajili ya kazi zake za kawaida.

Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu:

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kina jukumu la kuratibu maendeleo ya elimu ya juu na kuwa na mashirikiano ya karibu na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania, vyuo vikuu vya Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na Taasisi nyengine za elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa 2013/2014, Kitengo kimeendelea na kazi zake za kawaida za uratibu ikiwa ni pamoja na kufuatilia uendeshaji wa vyuo na kutangaza nafasi za masomo zinazotolewa na nchi au Mashirika mbali mbali duniani ikiwemo Misri, Cuba, China, Indonesia, India, Algeria, Srilanka, Korea, Australia, Brunei na Jumuiya ya Madola. Fani zilizotangazwa ni Udaktari, Kilimo, Uongozi wa Elimu, Sayansi ya Mazingira, Kemia, *Cardiology*, Uongozi wa Fedha, Mabadiliko ya Mazingira na Maendeleo ya Kimataifa, Sheria na Sayansi ya Bahari. Waombaji 176 waliwasilisha maombi yao kwa fani na nchi tofauti, jumla ya waombaji 36 walifanikiwa kupata nafasi za masomo. Wanafunzi 09 nchini Algeria, 02 Cuba, 23 China na 02 Jumuiya ya Madola.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Kitengo kinaendelea na uwekaji wa kumbukumbu za wahitimu wanaorejea nchini. Hadi Aprili, 2014, Kitengo kimepokea wahitimu 431, (222 wanaume na 209 wanawake) ambao walikuwa hawajaajiriwa. Wahitimu hao wamepatiwa barua za utambulisho katika Ofisi inayohusika na Utumishi wa Umma kwa ajili ya taratibu za ajira. Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 171 hadi 174.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, Kitengo kitaendelea kuratibu utoaji wa elimu ya juu kulingana na mahitaji ya nchi kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika na elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 45,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi Za Maisha:

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata haki yao ya msingi ya elimu wakiwemo watoto wenye mahitaji maalumu. Aidha, kitengo kina dhamana ya kuwapatia Stadi za maisha walimu, wakufunzi na wanafunzi ikiwemo ushauri nasaha, elimu juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI na madawa ya kulevya, pamoja na kuwapa taaluma juu ya masuala ya jinsia ili wawe raia wema katika jamii.

Elimu Mjumuisho:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, kitengo kimefanya ufuatiliaji wa skuli 31 Unguja na Pemba (22 za Serikali na 9 za binafsi) zinazotekeleza progamu ya Elimu Mjumuisho kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake. Aidha, kitengo kilitoa mafunzo mbali mbali kwa walimu wa skuli ili waweze kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum katika madarasa ya kawaida kwa ufanisi. Miongoni mwa mafunzo hayo ni mafunzo ya maandishi ya nukta nundu, mafunzo ya lugha ya alama na mbinu mbali za urekebishaji wa tabia za wanafunzi. Jumla ya walimu 626 (468 wanawake na 158 wanaume) kwa Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo hayo. Pia, Kitengo kilitoa mafunzo ya lugha ya alama na nukta nundu kwa wanafunzi 176 (104 wanawake na wanaume 72) wa Unguja na Pemba ili kuwajengea uwezo wa kuwasaidia wanafunzi wenzao viziwi na wasioona katika kujifunza. Maelezo zaidi yanapatikana Ibara ya 177 hadi 184.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kilisimamia upimaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.Wanafunzi waliogunduliwa na matatizo walipatiwa tiba na wanafunzi 22 (12 wanawake na 10 wanaume) walipewa rufaa ya kwenda katika Hospitali tofauti kwa uchunguzi na matibabu zaidi (4 walipelekwa *KCMC*, Moshi, 1 Muhimbili na 19 Mnazi Mmoja). Vile Vile, kitengo kimenunua jumla ya miwani 353 na kuwapatia wanafunzi waliogundulika na matatizo ya uoni katika skuli za Unguja na Pemba. Aidha, Kitengo kimenunua vifaa vya kukuza maandishi, fimbo nyeupe, "*puzzles*" mashine za *Braille* na programu ya *NVDA*.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha taaluma ya elimu mjumuisho, wafanyakazi wamepatiwa nafasi za mafunzo ili kuwajengea uwezo zaidi katika utendaji wa kazi zao. Jumla ya walimu 16 na watendaji 4 wa kitengo wanaendelea na masomo ya Shahada ya kwanza katika fani ya elimu maalum katika vyuo vikuu mbali mbali vya Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kilishirikiana na Taasisi ya Elimu, Zanzibar katika kukifanyia majaribio kivunge (*toolkit*) kilichoandaliwa na *UNESCO* kwa wakufunzi 29 (6 wanawake na 23 wanaume) wa vyuo vya ualimu Unguja na

Pemba ili kuangalia iwapo maudhui na njia za ufundishaji katika kivunge hicho yanaendana na mazingira halisi ya Zanzibar pamoja na kuangalia endapo kitasaidia katika kuandaa mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, katika kuhamasisha jamii juu ya suala zima la Elimu Mjumuisho, vipindi viwili vya redio vilirushwa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar ambapo wananchi walipata fursa ya kuchangia na kuuliza maswali kuhusu utekelezaji wa Elimu Mjumuisho katika skuli na vyuo.

Ushauri Nasaha:

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kilifanya mkutano na maafisa 10 wa Elimu Wilaya pamoja na Waratibu 10 wa vituo vya walimu Unguja na Pemba ili kujua umuhimu wa kuwepo walimu washauri na kufanya kazi nao kwa karibu ili kulifikia vyema lengo la ufundishaji na ujifunzaji. Idadi ya walimu washauri wote ni 770 (432 wanawake na 338 wanaume) kati ya walimu hao waliopata mafunzo ya ushauri ni 234 (134 wanawake na 100 wanaume). Kitengo pia kilifanya ufuatiliaji katika skuli saba za dahalia za Pemba na kuwapatia ushauri nasaha walimu na wanafunzi wa skuli hizo kufuatia kesi nyingi zinazojitokeza za unyanyasaji wa wanafunzi wapya wanapowasili katika dakhalia hizo.

Mapambano Dhidi ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya:

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kilitoa mafunzo ya Stadi za maisha kwa walimu 30 (18 wanawake na 12 wanaume) wanaofundisha Kidato cha Nne kwa masomo ya Kiengereza na Biolojia Unguja ili kuwawezesha kuchanganya Stadi za maisha na masomo wanayofundisha na kuweza kuwajengea wanafunzi uelewa katika Stadi za maisha.

Mhe. Mwenyekiti, katika mapambano dhidi ya UKIMWI na madawa ya kulevya, kitengo kimetoa mafunzo ya Stadi za maisha kwa wanafunzi viongozi wa klabu za afya katika skuli 18 za Unguja (Mkoa wa Mjini Magharibi na Kusini), jumla ya wanafunzi 72 walishiriki katika mafunzo hayo (wanawake 40 na wanaume 32). Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha kuishi katika mazingira salama.

Masuala ya Jinsia:

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kilitoa mafunzo juu ya udhalilishwaji wa kijinsia kwa wazazi 42 (13 wanaume na wanawake 29), walimu pamoja na wahudumu 18 (wanaume 7 na wanawake 11) wa vitengo vya wanafunzi wenye ulemavu wa akili Unguja. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha walimu na wazazi kuwafundisha na kuwakinga wanafunzi hawa kudhalilishwa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, kitengo kitaendelea kutoa mafunzo ya mbinu za ufundishaji masuala ya Elimu Mjumuisho kwa walimu zaidi, kuhamasisha jamii kuhusu haki ya elimu kwa watoto wote hasa wale wenye mahitaji maalum, kutoa mafunzo ya Stadi za maisha kwa walimu washauri na wanafunzi ili waweze kupambana na changamoto mbali mbali pamoja na kufanya utafiti juu ya idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu katika skuli zilizobakia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 75,000,000/= za kazi za kawaida.

Kitengo cha Urajis:

Baraza la Elimu:

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Urajis kina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa sheria ya elimu nchini, ikiwemo vikao vya Mabaraza ya elimu, usajili wa skuli, maombi ya leseni za walimu, masuala ya mimba na ndoa za wanafunzi.

Leseni za Walimu:

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya walimu 1,260 walipatiwa leseni za kusomeshea. Kati ya walimu hao 1,059 waliosomea na 201 wasiosomea. Pia, maofisa wa kitengo walitembelea skuli 17 za binafsi kukagua leseni za walimu. Katika

mwaka 2014/2015, maofisa wa Kitengo cha Mrajis wa Elimu wataendelea kukagua leseni za walimu wa skuli za Serikali na binafsi. Maelezo zaidi yanapatikana Ibara ya 188 hadi ibara ya 189.

Maombi ya Usajili wa Skuli:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 wizara ilisajili skuli 24 za Serikali.Pia, kitengo kilifanya mkutano na walimu wakuu kuelezea sheria mbali mbali zinazohusu uendeshaji na usimamizi wa skuli za binafsi. Katika mwaka 2014/2015, Ofisi ya Mrajis wa Elimu itaendelea kupokea na kushughulika maombi ya usajili kwa skuli zote za serikali na binafsi.

Kesi za Ujauzito na Ndoa za Wanafunzi:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014 jumla ya kesi 12 za ujauzito wa wanafunzi ziliripotiwa ambapo kesi 2 zilikuwa za wanafunzi kwa wanafunzi. Kesi 5 kati ya hizo zilijadiliwa na wanafunzi 4 walikubali kuendelea na masomo. Katika kipindi hiki kesi 9 za ndoa za wanafunzi ziliripotiwa na kati ya kesi hizi 4 zilikua baina ya wanafunzi kwa wanafunzi. Kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 6 ya mwaka 1982 kifungu cha 20 (3) wanafunzi 9 wa kike na wanafunzi 4 wa kiume walifukuzwa skuli. Katika mwaka 2014/2015, Kitengo cha Urajis kitaendelea kushughulikia kesi za ujauzito na ndoa za wanafunzi na pia kuwapatia elimu juu ya umuhimu wa kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2-015, kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 50,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Kitengo cha Michezo na Utamaduni:

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Michezo na Utamaduni kimeundwa ili kusaidia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Michezo Zanzibar ndani ya skuli na kukuza vipaji vya watoto ili kupata wanamichezo bora.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kimeendelea na juhudi za kuimarisha michezo kwa kujenga mashirikiano ya karibu zaidi na Taasisi zinazojishughulisha na michezo ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Katika mwaka 2013/14, Kitengo kwa kushirikiana na *British Council* kimetoa mafunzo ya mchezo wa riadha kwa walimu 25 ili kukuza ujuzi wa walimu hao katika mchezo huo. Shirika pia limedhamini mafunzo kwa wanafunzi 35 ya usimamizi na uamuzi wa mpira wa miguu, riadha na mpira wa wavu. Mafunzo hayo yamelenga kuinua ushiriki wa vijana kiuchezaji, usimamizi na uamuzi wa michezo.

Mhe. Mwenyekiti, katika shamrashamra za kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi, kitengo kiliandaa mashindano ya timu mchanganyiko za wanafunzi kutoka katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Wilaya nane zilishiriki katika michezo ya mpira wa miguu, Netiboli, mpira wa Wavu, mpira wa Meza na Bao. Aidha, wanafunzi wetu walipata fursa ya kushiriki katika mashindano ya skuli za Sekondari Afrika Mashariki (*FEASSSA*) yaliyofanyika Lira Uganda. Timu zilizoshiriki ni mpira wa miguu wanaume iliyofika robo fainali na mpira wa mikono wanaume iliyoshika nafasi ya tatu. Aidha, maandalizi ya mashindano ya michezo ya *UMISSETA* yameanza.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kuwepo kwa mihutasari wa somo la michezo katika elimu ya msingi, Kitengo kilitoa mafunzo ya michezo kwa walimu wanaofundisha somo la michezo wa darasa la kwanza na la pili. Pia, Kitengo kilifanya mikutano ya uhamasishaji kwa kupenda michezo na kuunda klabu za michezo kwa walimu wakuu na walimu wengine wa skuli za Wilaya ya Kusini, Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Chake Chake Pemba. Kitengo kiliandaa mashindano ya riadha ya mbio za nyika zinazojulikana kama "*Elimu Cross Country*" kwa wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari. Kwa mwaka 2014 jumla ya wakimbiaji 497 walishiriki, ambapo wanafunzi kumi walitoka skuli *ya Filbert Bayi* ya Kibaha. Mashindano haya yanasaidia kuibua hamasa ya kupenda michezo na kukuza ushirikiano kwa wanafunzi. Maelezo zaidi kuhusu kitengo cha michezo na utamaduni yanatolewa katika Ibara ya 195 hadi 197.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania kilitoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha somo la michezo katika skuli za msingi juu ya matumizi ya kadi za michezo kwa ajili ya kufundishia. Jumla ya walimu 35 kutoka skuli za Mkoa wa Mjini/Magharibi walishiriki katika awamu ya kwanza. Mafunzo hayo yataandaliwa kwa skuli za Pemba na yatashirikisha walimu 574 (352 kwa Unguja na 222) wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, kitengo kwa kushirikiana na taasisi nyengine za michezo ndani na nje ya nchi yetu kina lengo la kuendelea kutoa taaluma ya michezo kwa fani mbali mbali kwa walimu wa michezo katika skuli za Unguja na Pemba. Aidha, kwa kushirikiana na taasisi nyengine za elimu nchini, Kitengo kitaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa skuli za msingi wanaotarajiwa kuifundisha mihutasari ya somo la michezo. Halikadhalika, kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki ya Tanzania kupitia kituo chake cha *Olympafrica*, Kitengo kitaendesha mafunzo ya michezo mbali mbali ikiwemo ya asili katika maeneo ya vijijini. Aidha, "*British Council*" kwa kushirikiana na Kitengo na Kamisheni ya Michezo na Utamaduni kupitia mradi wake wa"*International Inspiration*" utaendelea na mpango wake wa mafunzo kwa walimu mbali mbali wa michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo pia kitaendelea na utaratibu wake wa kufanya tathmini ya kila mwaka ya michezo kupitia sherehe za Tamasha la Elimu bila Malipo kuanzia ngazi ya skuli, kanda, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Pia, kuendelea kutoa ushindani katika michezo itakayoandaliwa na Umoja wa Michezo na Sanaa Skuli za Sekondari Tanzania (*UMISSETA*) na Shirikisho la Michezo ya Skuli za Sekondari Afrika ya Mashariki (*FEASSSA*) inayofanyika kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kitaendelea kuwahamasisha walimu wa skuli wa ngazi mbali mbali kurejesha hali ya michezo kama ilivyokuwa zamani katika skuli zetu kwa kuanzisha na kuziendeleza "*Houses*" za wanafunzi ndani ya kila skuli. Mbio za "*Elimu Cross Country*" zinatarajiwa kuendelea kila mwaka na kujumuisha skuli zaidi kutoka nje ya Zanzibar ili kuleta hamasa kubwa zaidi katika michezo. Aidha, kitengo kwa kushirikiana na Taasisi nyengine kimedhamiria kuandaa tamasha kubwa la michezo na sanaa katika sherehe za Maadhimisho ya Miaka 50 ya Elimu Bila ya Malipo.

Mhe.Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 100,000,000/= kwa Unguja na shilingi milioni 70,000,000/= kwa Pemba kwa kutekeleza kazi zake za kawaida.

MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 15,000,000/= kutoka vianzio vya ada ya leseni za walimu pamoja na uandikishaji wa skuli binafsi. Hadi kufikia Mei 2014, jumla ya shilingi milioni 29,432,500/= zilikusanywa na kuwasilishwa Hazina ikiwa sawa na asilimia 196 ya makadirio. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara inakusudia kukusanya jumla ya shilingi millioni 30.0 ikiwa ni mapato ya usajili wa skuli za binafsi na leseni za walimu na kuziwasilisha Hazina Jadweli Nam. 46 inatoa ufafanuzi.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wote wa sekta ya elimu wakiwemo wananchi, Washirika wa Maendeleo na mashirika ya misaada ya Kimataifa kwa kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza elimu.Napenda kutoa shukurani zetu za pekee kwa Serikali ya Oman, Serikali ya Marekani, Sweden na Serikali ya Watu wa China, India na Misri.Pia, napenda kuyashukuru mashirika mbali mbali yakiwemo, *Sida, USAID, UNESCO, UNICEF, VSO, OPEC Fund* na *Partnership for Child Development* kupitia kwa *Imperial College of Science and Technology (UK).*Pia, shukurani zetu ziende kwa *Aga-Khan Foundation*, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Pia, napenda kuyashukuru mashirika yasio ya kiserikali ya *ZAYADESA, FAWE, Save the Children Fund, Book Aid International* na *ZAPDD*.

Jumla ya Gharama za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa ufanisi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 103,633,950,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 86,201,500,000/= ni kwa matumizi ya kawaida shilingi 3,300,000,000/= za SMZ na shilingi 24,132,450,000/= za washirika wa maendeleo kwa matumizi ya miradi ya maendeleo.Jadweli Nam. 44 na 45 zinatoa uchambuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, napenda kutoa hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii adhimu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kustahiki kila aina ya shukurani na sifa njema kuwa na uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako hili na kutoa maoni ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, pili, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka kama Kanuni ya 112(e) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2012) inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imefanya kazi ya kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mnamo tarehe 09/05/2014 ambayo iliwasilishwa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kamati ilijadili utekelezaji wa kazi za wizara kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 na matarajio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.Katika majadiliano na uchambuzi wa mapendekezo ya bajeti ya wizara hii, Kamati imebaini kuwa baadhi ya maeneo ya wizara bado yanakabiliwa na changamoto mbali mbali zinazoendelea kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba niwasilishe maoni ya Kamati kwa kuangalia maeneo mbali mbali ya wizara ambayo Kamati imeona kwa umuhimu wake kuyatolea maelezo na kutoa ushauri unaofaa kwa Wizara na Serikali.

Kuhusu Utekelezaji wa Kazi za Maendeleo:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Kazi za Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 ambapo katika taarifa ya utekelezaji, ilieleza kuwa utekelezaji wa Kazi za Maendeleo hutekelezwa kwa kupitia Miradi inayoanzishwa na wizara kwa kushirikiana na Serikali, Wananchi na Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa ya utekelezaji wa Kazi za Maendeleo, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ilitekeleza Miradi tisa ya Maendeleo ambapo Jumla ya fedha zilizotengwa za serikali katika miradi hiyo ni shilingi bilioni 5,350,000,000/= na kwa upande wa ruzuku kutoka kwa washirika mbali mbali wa Maendeleo ni shilingi bilioni Tshs 8,779,632,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa kuwa, mpaka kufikia tarehe 30 April, fedha zilizopatikana kutoka serikalini ni shilingi bilioni 1,137,000,000/= sawa na asilimia 21 na kwa upande wa washirika wa Maendeleo fedha zilizopatikana ni shilingi bilioni 6,059,603,156/= sawa na asilimia 68.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imefanya tathmini ya fedha zilizopatikana za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kuzingatia mchango wa Serikali na mchango wa Washirika wa Maendeleo na imebaini kuwa, bado serikali inatoa mchango mdogo wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo hali inayopelekea kuzorota na kutokukamilika kwa utekelezaji wa miradi kwa muda uliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya utekelezaji wa Miradi usio wa ufanisi umejitokeza katika Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi ambapo fedha zilizotengwa kutoka serikalini ni shilingi milioni 150,000,000/= na fedha zilizopatikana ni shilingi milioni 19,000,000/= sawa na asilimia 13 tu za fedha zote zilizotolewa na serikali. Aidha, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi na Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu ilishindwa kutekelezwa na Wizara kutokana na kukosekana kwa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi hata kidogo na uingizwaji mdogo wa fedha za miradi kutoka serikalini, kwani unazorotesha sana utekelezaji wa miradi iliyopangwa na Wizara. Hivyo, Kamati inaitaka serikali kuipa

kipaumbele ya kibajeti Wizara hii, kwa kuhakikisha kuwa inaipatia fedha za miradi kwa wakati. Kufanya hivyo, kutaiwezesha Wizara kufanya kazi zake kwa ufanisi na kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2013/2014.

Kuhusu Uhaba wa Fedha kwa Ajili ya Utekelezaji wa Kazi za Kawaida

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inasikitishwa sana na uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida katika wizara hii hali inayopelekea utekelezaji wa majukumu ya wizara kutotekelezwa katika kiwango kinachostahiki. Kamati imebaini kuwa uhaba wa fedha umepelekea wizara kushindwa kuzipatia baadhi ya skuli zake vitabu vya kutosha, na kupelekea kuwepo kwa upungufu wa vitabu katika skuli hasa skuli za msingi, uhaba wa madarasa na vikalio unaotokana na ongezeko kubwa la wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipokuwa inapitia bajeti ya matumizi ya kazi za kawaida imebaini kuwa, katika mwaka huu wa fedha wa 2014/2015 kumekuwa na punguzo la fedha za ruzuku kwa baadhi ya ofisi na vitengo vya wizara, ambapo punguzo hilo limejitokeza katika Baraza la Elimu, Chuo cha Kiislamu, Taasisi ya Karume, Sayansi na Teknolojia, Bodi ya Mikopo, Taasisi ya Elimu na kadhalika, hali inayoashiria kuwa bado wizara itaendelea kushindwa kutekeleza kazi zake za kawaida kwa ufanisi kwa vile bado haijatengewa fedha za kutosha.

Ni dhahiri kuwa punguzo la fedha za ruzuku linaashiria kuzorota kwa huduma zinazotolewa na ofisi, vitengo na taasisi za wizara. Kwa mfano, katika Taasisi ya Karume, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 ilipangiwa ruzuku kwa ajili ya uendeshaji ya Shilingi 393,968,000/= na katika mwaka huu wa fedha wa 2014/2015 fedha za ruzuku zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji ni Shilingi 26,600,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, ukilinganisha baina ya mwaka wa fedha uliotangulia na mwaka huu wa fedha, utagundua kuwa kiwango cha ruzuku katika taasisi hii kimekuwa ni kidogo sana na itapelekea kurudisha nyuma maendeleo ya taasisi, kwani kiwango hicho hakitokidhi haja hata kuweza kutekeleza kazi za kawaida za taasisi, hivyo itakuwa ni vigumu kwa taasisi hii kuweza kutekeleza shughuli walizojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaiomba serikali kutafuta vianzio vyengine vya fedha ambavyo vitaweza kusaidia kukuza bajeti ya wizara hii na kupunguza changamoto za utekelezaji wa majukumu ya wizara kupitia ofisi na vitengo vyake. Aidha, kwa upande wa kamati inatoa rai ya kuanzishwa Mfuko wa Elimu kisheria ili mfuko huo utumike katika kuchangia gharama za elimu katika ofisi, vitengo na taasisi mbali mbali za wizara na kuweza kukuza sekta ya elimu nchini.

Kuhusu Usimamizi wa Majengo ya Wizara

Mhe Mwenyekiti, kamati inaipongeza serikali, wizara na Washirika wa Maendeleo kwa mashirikiano yao ya pamoja na kuweza kujenga skuli mpya za kisasa Unguja na Pemba ambazo zinatoa fursa kwa wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri. Pamoja na pongezi hizo, kamati inaitaka Wizara kuandaa utaratibu maalumu wa kusimamia majengo yake ikiwemo majengo ya skuli mpya, skuli kongwe na majengo mengine, ili yaweze kutumika kwa kipindi kirefu.

Kamati imebaini kuwa baadhi ya skuli mpya zilizojengwa na wizara zimekosa ubora na zimeanza kubomoka kwa kipindi kifupi sana, tokea wizara kukabidhi majengo hayo kwa skuli husika. Hali hiyo imejitokeza katika Skuli ya Faraja ambapo ngazi inayotumika kwa watu wenye ulemavu imevunjika. Aidha, katika Skuli ya Uzini sakafu kwa baadhi ya madarasa zimeanza kubomoka.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imepata wasi wasi mkubwa juu ya ubovu wa skuli hizo na inaishauri wizara kuwa makini katika ujenzi wa majengo yake ya skuli na ihakikishe kuwa inawatumia wataalamu wake katika kusimamia ujenzi unaofanyika ili uwe na viwango vinavyostahiki pamoja na kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu hao katika hatua zote za ujenzi.

Kuhusu Gharama za Uendeshaji wa Skuli za Serikali

Kwa Kipindi kirefu sasa skuli zetu za serikali zimekuwa zinajiendesha wenyewe bila ya kupatiwa rukuzu kutoka serikalini, lakini kutokana na mabadiliko mbali mbali yanayojitokeza katika skuli hizo, ikiwemo ujenzi wa majengo

ya kisasa, matumizi ya computa kwa baadhi ya skuli na ongezeko la idadi ya wanafunzi kumepelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji ikiwemo gharama za umeme na gharama za ununuzi wa madawati ambayo mahitaji yake yamekuwa yakizidi kila leo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaitaka serikali kuenda sambamba na mabadiliko yanayojitokeza katika skuli zetu; kwa kubuni mbinu mpya za uendeshaji wa skuli kwani uendeshaji wa skuli unaotumika sasa, unategemea sana fedha za michango ya wanafunzi na vianzio vyengine vitakavyobuniwa na uongozi wa skuli. Kuhusiana na gharama za umeme, Kamati inaitaka Wizara iwe makini katika kusimamia gharama za umeme ili kuepusha malimbikizo ya madeni yanayoweza kujitokeza kwa kukosa umakini na inaishauri wizara kutumia nishati ya umeme wa jua katika skuli zake ili kuepuka kutumia umeme wa kawaida ambao gharama yake ni kubwa na hakuna bajeti maalum iliyotengwa na Wizara kwa ajili ya kulipia gharama hizo isipokuwa skuli hutumia fedha za michango ya wanafunzi katika kulipia gharama za umeme.

Uvamizi na Uharibifu wa Mazingira katika Maeneo ya Skuli

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwa, kuna baadhi ya wananchi ambao wanakaa karibu na maeneo ya skuli au hata wale walioko maeneo ya mbali wamekuwa na tabia ya kufanya uharibifu mkubwa katika maeneo ya skuli kwa kuchimba mchanga hali inayoleta athari kwa skuli zetu. Miongoni mwa skuli ambazo vitendo hivyo vinaendelea kufanyika ni Skuli ya Mwanakwerekwe “A”, Regeza Mwendo, Potoa Sekondari, Mwanakwerekwe “C” na Skuli ya Kilimahewa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasikitishwa sana na hali hiyo na inashauri jamii kuwa walinzi wa skuli ambazo zitakuwa zinawazunguka na pia srikali ipange mpango wa muda mrefu ambao utakuwa na lengo la kuweka uzio kwa skuli zote za serikali ili kuepusha matatizo yanayojitokeza.

Kwa upande wa uvamizi wa maeneo ya skuli, kamati imegundua kuwa kuna baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kuyageuza maeneo ya Skuli kuwa yao binafsi na kupelekea usumbufu mkubwa katika maeneo hayo kwani sehemu hizo baada ya kuvamiwa na wananchi hao, huzitumia kwa matumizi mengine yasiyofanana na matumizi ya skuli kama vile kugeuza sehemu hizo kuwa makazi ya watu kama ilivyojitokeza hali hiyo katika Skuli ya Regeze Mwendo.

Kamati inaishauri wizara kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia idara yake ya ardhi na usajili, katika kusimamia upatikanaji wa Hatimiliki kwa maeneo yao ili iwe njia moja wapo ya kuyadhibiti maeneo ya skuli na maeneo mengine ya 1izara.

Kuhusu Hali ya Michezo Maskulini

Mhe Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa kiwango cha michezo maskulini kimekuwa kinaporomoka kwa kiasi kikubwa kutokana na kukosa mashirikiano mazuri baina ya wanafunzi, walimu na wazee, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wazee kuwakataza watoto wao kutoshiriki katika michezo maskulini kutokana na kuwa na uelewa mdogo juu ya masuala ya michezo. Wazee walio wengi wanaamini kuwa; kushiriki watoto katika michezo kutapelekea watoto wao kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao.

Kupitia kamati hii naomba kuiambia jamii kuwa, michezo ni sehemu ya mafunzo wanayotakiwa kupatiwa wanafunzi kwani inachangamsha na kukuza akili zao. Hivyo kamati yetu inaiomba jamii kuwashajihisha watoto wao kushiriki katika michezo ambayo itazingatia mila na desturi zetu za kizanzibari.

Kamati inatoa pongezi za dhati kwa wizara kwa jitihada zake za kukuza michezo maskulini, licha ya kukosa ushirikiano mzuri kwa baadhi ya wazee, Wizara bado imekuwa inaendelea kuchukua jitihada hizo na imefanikiwa kuanzisha mashindano ya mbio za nyika ambayo yanajumuisha washiriki kutoka Zanzibar na Tanzania bara.

Kamati inaunga mkono jitihada za Wizara za kuendeleza michezo maskulini na inaishauri Wizara hii kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo katika kuiendeleza michezo maskulini ili iweze kuimarika kama ilivyokuwa katika kipindi cha nyuma.

Kuhusu Mpango wa Upatikanaji wa Chakula Maskulini

Kamati inaipongeza wizara na Washirika wa Maendeleo, kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, kuweza kubuni mpango wa upatikanaji wa chakula maskulini ambao utasaidia kuwapatia chakula wanafunzi wa skuli za Msingi. Katika mpango huo, Kamati iliarifiwa kuwa, utaanza kutekelezwa Pemba katika Wilaya ya Kaskazini "A" ambapo katika utekelezaji wake utawashirikisha na wananchi waliopo karibu na maeneo ya skuli hizo katika namna ya upatikanaji wa chakula na hata uandaaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaitaka jamii, pindi mpango huo utakapoanza katika maeneo yao, kuupokea kwa moyo mkunjufu pamoja na kuwapa mashirikiano wizara pindi watakapohitajia kwani bila ya mashirikiano yao, wizara itashindwa kufanikisha mpango huo.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumalizia hotuba hii kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha maoni pamoja na mashirikiano uliyokuwa unatupa pindi tunapohitaji ushauri kutoka kwako. Aidha, namshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya licha ya kuwa na ufinyu wa fedha za bajeti katika utekelezaji wa kazi za kila siku.

Pia natoa pongezi zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa busara zao na umakini katika kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi tulichokuwa tunafanya uchambuzi wa bajeti ya wizara. Baada ya shukrani hizo sasa naomba kuwatambua kwa kuwataja majina Wwajumbe wa Kamati kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hassan Hamad Omar	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	Mjumbe
5.	Mhe. Farida Amour Mohamed	Mjumbe
6.	Mhe. Mohamed Mbwana Hamad	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaid Kassim Mussa	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru makatibu wetu wa Kamati ambao kwa kipindi chote cha kazi zetu wamekuwa wakitupa msaada mkubwa wa kitaalamu na kuweza kufanikisha shughuli zetu kwa ufanisi mkubwa na kwa muda uliopangwa na kwa umahiri unaofaa nao ni:-

1. Ndg. Asha Said Mohamed; na
2. Ndg. Maryam Rashid Ali

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja hii mimi binafsi na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. Na mwisho kabisa nawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu waweze kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja ili wizara ipate kufanya shughuli zake vizuri kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya ripoti hii ya kamati naomba na mimi nitoe mchango wangu ijapokuwa kimuhutasari kama Mwakilishi wa Jimbo la Chambani. Kwa ruhusa yako naomba uniruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi utakuwa ni mfupi sana, kwanza nichangie katika ukurasa wa 13 Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima. Katika ukurasa huu wa 13 kuna kifungu (iii) kiachosema, "Kuchonga na kusambaza thamani katika skuli za sekondari zilizokamilishwa kujengwa".

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri lakini kuna swali tu nataka nimuulize Mhe. Waziri, kuna mchango wa wasafiri ambao tulisema kwamba kila msafiri katika Kisiwa cha Unguja na Pemba atozwe katika tiketi yake shilingi 1,000 kwa ajili ya kupunguza tatizo hili la madawati ambalo limekuwa ni tatizo kubwa. Je, Mhe. Waziri ana utaratibu gani

wa mapato ya fedha hizi kutoka Wizara ya Fedha au kutoka pale Bandari, na tokea tulipopitisha sheria hii ni fedha ngapi ambazo amezipata na ni madawati mangapi ambayo yashachongwa kupitia fedha hizi?

Nikiendelea kifungu kidogo cha (v) hapa inasema,

"Kukamilika ujenzi wa skuli za sekondari za Paje/Mtule, Dimani na Tunguu na kujenga ukuta wa kuzunguka skuli mbili mpya za sekondari katika skuli 16 zilizojengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia".

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitakuwa nina swali moja tu, hizi skuli mbili ambazo zitajengwa uzio ni zipi? Kwa sababu hazikutajwa. Vile vile kuna skuli hii ya Paje/Mtule na Dimani zimekaa muda mrefu sana, skuli nyingi zilizojengwa katika mradi huu zimeshafunguliwa lakini skuli hizi bado zinasuasua.

Mhe. Waziri ni lini anatarajia skuli hizi kuzikabidhi kwa wananchi ili na wao wapate kufaidika na skuli hizi. Lakini kama tulivyoeleza katika ripoti hii ambayo nimeisoma hivi punde, skuli hizi zinajengwa chini ya kiwango, naiomba serikali iwe makini sana katika kusimamia ujenzi wa skuli hizi kwa sababu tumetaja skuli chache tu, lakini nyingi zao hivi sasa zimekuwa zinavuja nyengine tiles pia zinazuka. Kwa hivyo, naiomba serikali iwe makini sana katika hili ili tunapotoa mradi huu wa ujenzi basi tupate wajengaji ambao wanafuata vigezo vinavyofaa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 17 unaozungumza Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi. Kwa kweli naipongeza sana serikali kupitia Wizara ya Elimu kuziangalia skuli hizi za maandalizi na kuziimarisha. Kwa kuwa skuli za maandalizi sasa hivi imekuwa ni miongoni mwa elimu ya lazima, naiomba serikali suala hili ilipe kipaumbele sana. Naipongeza serikali kwamba katika ukurasa wa 17(ii) hapa Kukamilisha ujenzi wa skuli za maandalizi za Kajengwa na Chambani na kuchonga thamani zake.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuliona hili jengo la Skuli ya Chambani pahala ambapo pana wanafunzi wengi wa maandalizi lakini walikuwa wanakaa chini ya miembe, mikwaju kwa sababu ya kukosa pahala na wananchi wa Chambani walisimama kidete katika kulijenga jengo hili mpaka sasa hivi *Alhamdulillah* wizara imelichukua ni matumaini yangu kwamba wizara italimaliza jengo hili kama walivyoahidi ndani ya bajeti hii ambayo tunayo leo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika mchango wa Maslahi ya Walimu. Jamani walimu ni watu muhimu sana katika nchi na wanahitaji waangaliwe kwa jicho la huruma. Kwa sababu mwalimu baada ya kazi yake ya ualimu hana muda tena wa kuangalia hapa na pale kupata angalau chochote. Naomba maslahi ya walimu yaangaliwe vizuri na ikiwezekana wapewe kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, kuna walimu ambao wanafundisha skuli za mbali na wanapokaa, kuna malalamiko mengi kwamba hawapewi nauli. Naiomba wizara hili ilifanyie uhakiki kila anayestahiki kulipwa nauli alipwe, yasitoke haya malalamiko ambayo si ya lazima.

Mhe. Mwenyekiti, pia miongoni mwa maslahi ya walimu ni huduma zao za likizo. Walimu wengine wanakaa miaka mitano, sita hawajapata huduma ya likizo. Hili liangaliwe vizuri ili walimu kila unapofika wakati wa kupewa likizo basi huduma yake iende sambamba kwa mujibu wa miaka yake.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika upungufu wa walimu hasa katika skuli za msingi. Mhe. Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa wa walimu sekondari na msingi. Lakini msingi nasema ni wengi zaidi. Kwa sababu ukiangalia walimu wengi wa skuli za msingi wameajiriwa miaka ya 70 na 80 mwanzo, wamefikia umri mkubwa wa kazi wanaanza kustaafu mmoja mmoja na wengine wanajiendeleza na kusoma. Anapojiendeleza mwalimu kusoma akirudi kuchukua *degree* au *masters* harudi tena msingi anapangiwa skuli ya sekondari. Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kuweza kudhibiti upungufu wa walimu katika skuli za msingi wakati ambapo zinakabiliwa na changamoto ya kustaafu walimu kwa wingi, na vile vile walimu wanaoajiriwa sasa ni wale ambao wanatoka vyuo vikuu wanapangiwa katika skuli za sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika Kitengo cha Ukaguzi. Mhe. Mwenyekiti, bila ya ukaguzi hakuna kinachokuwa. Katika Wizara ya Elimu Kitengo cha Ukaguzi ni kitengo muhimu sana, lakini inaonekana kwamba bajeti katika kitengo hichi imekuwa ni ndogo mno. Sasa ningeomba Serikali suala hili iliangalie vizuri.

Halafu wakaguzi wetu hivi sasa wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo hata ofisi zao. Pale Pemba ofisi ya ukaguzi kwa kweli ukenda wewe mwenyewe utaona huruma. Pia miongoni mwa changamoto ambazo zinawakabili wakaguzi ni pamoja na kuwa hawana vipandio vya kutosha. Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu iwaangalie wakaguzi wetu ili waweze kufanya kazi vizuri zenye tija na yenye ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo mdogo nakushukuru kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani na kwa niaba ya Kamati yangu tunaiunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, bajeti hii tunapaswa kuichangia kwa muda wa siku moja na nusu kwa mujibu wa makubaliano yetu tulivyopangiwa. Na tunatakiwa kuchangia kuanzia sasa hivi, jioni na baadhi kama watabakia watu asubuhi, ili mchana wake tufanye majumuisho. Jioni tuendelee na bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Lakini wakati tunayazungumza hayo tumekwisha kupitwa na muda. Kwa utaratibu huo, imetakiwa nitangaze kwamba siku ya Jumamosi inayofuata na Jumamosi inayofuata tena zitaendelea kuwa ni siku za kazi katika Baraza hili.

Baada ya maelekezo hayo, kwa sasa nina wachangiaji watatu. Naomba kama kuna wengine walete maombi yao ili tuweze kwenda kwa mujibu wa taratibu tulizokuwa tumejiwekea.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametuwezesha kwa siku ya leo kuwa katika afya njema ili kuweza kusaidia mambo yetu ya taifa hili kwa mustakabali wa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwapongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao wametuletea ripoti hii kwa ajili ya kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo kwanza niipongeze sana wizara hii kwa jinsi ya kujenga skuli nzuri tu za sekondari. Hata hivyo nitahadharishe kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tatizo letu linalotukuta katika mambo yetu ambayo tunayajenga mwisho wake huwa hatuna mbaya. Sasa niiombe tu wizara hii kwamba yale majengo ambayo tumeyajenga, kwa hivyo ni vyema tukakaa tukatafakari suala la utunzaji. Maana tatizo letu utunzaji kwetu sisi tunaliona ni jambo dogo, lakini ni jambo kubwa kwa sababu kutokutunza kitu baadae tunakosa mtoto na maji ya moto.

Kwa hivyo, niiombe sana wizara yale majengo ambayo tumeyajenga pamoja na matatizo yake ya hapa na pale lakini na utunzaji nao ni mzuri. Nikitilia mkazo hapo hapo hatimiliki nayo naomba itiliwe mkazo kwamba ni muhimu sana katika majengo yetu haya.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 26 Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mimi nitamuomba Mhe. Waziri anapokuja hapa kwa sababu idara hii ni idara muhimu ambayo inachukua mambo mengi katika wizara. Sasa nitamuomba Mhe. Waziri kwa sababu najua tu wanaosafiri kwenda nje, kusafiri kwenda ndani kupata mafunzo ni Wakurugenzi na baadhi ya watu ambao wana nyadhifa mbali mbali. Lakini nitamuuliza Mhe. Waziri. Je, hawa madereva wanapata mafunzo. Hasa nimuulize yeye mwenyewe dereva wake, pamoja na dereva wa Naibu Waziri kwa sababu tunaanza vichwa kwanza, pamoja na madereva wote ambao tunao katika wizara.

Mhe. Mwenyekiti, hili silisemei Wizara ya Elimu tu, nimekusudia hii Wizara ya Elimu kama ni mfano. Lakini nasemea wizara zote kwa sababu madereva wetu bado nidhamu zao si nzuri. Lakini wakipata mafunzo watakuwa na nidhamu nzuri baadhi ya madereva. Kwa sababu dereva unatakiwa ukae kwenye gari yako ile ndio ofisi yako. Sasa kama mtu hukumpa mafunzo mambo mengine hayajui. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa sababu nimetizama kifungu hapa cha mafunzo kina shilingi 53,750,000/= kama hivi. Sasa kipindi hiki nitamuomba Mhe. Waziri pesa hizi wapelekwe madereva mafunzoni ili na wao wapate fursa ya kujua kazi yao ni nini. Akija hapa Mhe. Waziri aje anieleze vizuri au fungu hili silipitishi. Niambiwe ni madereva wangapi kwa kipindi cha mwaka huu watapelekwa kwenye mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika ukurasa wa 49 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, hii itakuwa ni bajeti ya tatu nadhani kuzungumzia suala la Mamlaka hii ya Mafunzo ya Amali. Nadhani kulikuwa na mradi huu unataka kupelekwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ambao kidogo ulikuwa na mvutano kwamba ile skuli ijengwe wapi. Lakini baadae ikaamuliwa kwamba ijengwe sehemu ya Bagamoyo Mtambwe. Sasa naona humu

hamkuandikwa chochote. Je, nauliza ule mradi umekufa, au umefikia njiani, au kulikoni. Mhe. Waziri uje unieleze kwa kina hapa kwa sababu mradi ule ulikuwa umeshakuwepo katika mtiririko mzuri, sasa naona hapakutajwa chochote. Ile skuli sasa ya amali itajengwa vipi, itajengwa wapi, na ilikuwa kuwaje ikawa mradi huo haukuingizwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 76 Kitengo cha Michezo na Utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sasa hivi umefika wakati tubadilike katika kitengo hiki. Na hasa kubadilika kwake huyu mtu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo yeye atokee kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa sababu Wizara ya Elimu tunasema "Udongo upate ulimaji".

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie tu kwamba enzi yetu sisi tumechezeshwa michezo yote ikiwemo *football*. Mimi Skuli ya Utaani nimesoma, tumeanzishwa michezo yote Mungu amuweke Bi Maryam Said ndie aliyekuwa mwalimu wangu wa michezo wa darasa. Lakini michezo yote tulikuwa tunachezeshwa, na tulikuwa *very smart*, tulikuwa na *good health*, tulikuwa na kila kitu. Pia watoto wanakuwa akili zinachanuka. Lakini leo tumetia tu humu Kitengo cha Michezo na Utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, pia skuli tulikuwa tunafundishwa utamaduni wetu, tunaimbishwa ngoma mbali mbali, msewe, ngoma za utamaduni wa Mzanzibari. Lakini sasa hivi niseme tu jambo hili hatulitilii mkazo kwa nini, na hapa Zanzibar michezo ilikuwa ndio kitovu. Tulikuwa tunaleta makombe hapa, tunaleta kila kitu. Hasa riadha ilikuwa kwa kweli Zanzibar hawatupati. Pamoja na wenzetu na milima huko lakini riadha ilikuwa tunashinda vizuri sana Zanzibar. Kwa hivyo, niiombe Serikali kwa makusudi kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo washirikiane vizuri ili michezo hii irejeshwe kama zamani, ili tuweze kupata watu ambao wana vipaji vya michezo vya aina mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikija hapo hapo kwa mambo ambayo yalitusaidia sisi enzi yetu niseme Mhe. Waziri hebu nakuomba kila nikisimama hapa nikichangia wizara hii mimi nasema *domestic science* ni muhimu maskulini. Kwa sababu kwa ulimwengu tulionao leo unamchukua mwanafunzi hajui hata kupika chai; ile chai anaichukua sufuria na maji baridi anatia majani ikisha ndio anaweka kwenye moto. Hajui hata kutia kifungo chashati lake la skuli. Naiomba sana Serikali na mimi natoa wito hasa kama kuna mtu ambae ataweka kitengo hiki kwa makusudi kama ni biashara moja wapo. Kwa sababu watoto wetu sasa hivi kila mmoja anajitia hamnazo, hawataki kukaa jikoni.

Leo anaolewa mtoto hata kupika chakula hajui. Hawezi chochote kwa sababu anajifanya anasoma mara leo *tuition*, mara leo nini, hana kimoja anachokiweza. Naiomba Wizara ya Elimu, Utamaduni, Utalii na Michezo na Serikali kwa jumla kwamba kitengo hiki cha *domestic science* kirejee upya ili watoto wajue namna gani ya kujifunza.

Maana yake hiyo *domestic science* imejigawa nyanja mbali mbali. Unajua namna ya kulea mtoto, unajua namna ya kushona, kufuma mashuka, kufanya kila kitu. Maana yake mapishi yote unayajua hapo. Mimi sikufundishwa upishi na mama yangu, mimi upishi nimefundishwa nilipokuwa skuli. *Domestic science* imenilea vizuri kwa hivyo pamoja na nilivyo hivi lakini hakuna hata kitu kimoja kinachonishinda kwa mapishi. Kwa hivyo, kitengo hiki cha *Domestic Science* ni muhimu. Naiomba sana Serikali irudishe kitengo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika mishahara ya walimu. Najua sana kwamba Serikali pamoja na yote inajitahidi lakini bado mwalimu ni mtu muhimu katika taifa lolote. Maana sisi sote humu tusingefika hapa kama hatukupata walimu waliotusomesha. Kwa hivyo, mazingira yetu yalivyo naomba sana wizara, hasa Serikali, pamoja na mishahara kuongezwa lakini bado walimu wana kazi kubwa sana.

Wewe tizama mwanao tu kwenye nyumba ambae hashindi hata nyumbani, kutwa anashinda skuli, akiwa mdogo na akiwa mkubwa. Basi tujue kwamba mwalimu ana kazi kubwa sana. Pamoja na maposho na vyenginevyo, lakini bado naiomba Serikali iwajali sana walimu kuwaongezea maposho na mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba naiunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Na nawaomba Wajumbe wenzangu kwamba hii ni wizara muhimu ambayo ndio wizara mama, ndio wizara ufunguo wa kutuonesha njia ya kwenda popote pale. Basi waiunge mkono wizara hii isipokuwa wachangie yale ambayo waliyonayo, ili kuweza kuboresha baadhi ya mambo. Ahsante sana.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kwa heshima na taadhima kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kutupa pumzi tukaendelea na vikao vyetu hivi. *Inshaallah* kwa uwezo wake atupe uhai na uzima. Kama tunavyojua *we are all in transit*!

Mhe. Mwenyekiti, lengo kubwa la Baraza kwa ufahamu wangu mimi, maana yake mshamba si kuzaliwa shamba, kutokufahamu mambo tu wakati mwengine. Lakini kwa ufahamu wangu mimi tumekuja kuwatumikia wananchi katika Baraza lako hili.

Mhe. Mwenyekiti, ili nisipoteze muda labda nijitambulishe tu kwamba mimi ni mdau mkubwa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Na sikuanza leo katika masuala ya kuchangia wizara hii. Najua Serikali yetu inataka mashirikiano na inataka kusaidiana ndio maana nazipongeza nchi za *donors* hizi walioweza kutuunga mkono. Mhe. Mwenyekiti. Labda nirejee tu kwa nini nikasema mimi ni mdau mkubwa halafu nije na majumuisho hapa, moja kuona jinsi gani tunaweza kusaidiana.

Mhe. Mwenyekiti, miaka 20 iliyopita aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Makadara Mhe. Taimour Saleh Juma jengo liko pale. Katika kuisaidia Wizara ya Elimu na kuisaidia nchi yangu, nina uchungu na nchi yangu, naipenda nchi yangu ya Zanzibar. Kwa hivyo, nikajenga Skuli ya Makadara ambayo ipo mpaka leo, *Alhamdulillah* imetunzwa.

Mhe. Mwenyekiti, sifiki hapo tu, nilipopata wageni kutoka Pemba Sheikh Ahmed bin Breik na Mama Lutfiya wale ni wazaliwa wa Chake Chake Jimbo la Wawi. Nilipokwenda kule wakakuta madarasa yanataka kuboreshwa wanataka kusaidiwa. Wakaamua wakaniambia mimi Raza mtafute mkandarasi madarasa yote Skuli ya Furaha. Mhe. Saleh Nassor Juma shahidi wangu, tukajenga madarasa mapya yote na tukatia vikalio. Karibu *over 200 millions* zilitumika. Huo ulikuwa ni msaada kama ni mdau mkubwa. Na mgeni wa heshima wakati ule alikuwa Rais Mstaafu Mhe. Ali Hassan Mwinyi, pamoja na aliyekuwa Waziri wa Elimu Mhe. Haroun Ali Suleiman, pamoja na Waziri Kiongozi Mstaafu Dkt. Mohammed Gharib Bilal, pamoja na viongozi mbali mbali wa Chama na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya kujaaliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini kwa sababu naipenda elimu, kwa hivyo nikaamua mwaka 2012 tarehe 18 Julai nilijaaliwa kwenda skuli ya Pagali pale. Pagali walikuwa na jengo ambalo walitumia nguvu, walitakiwa kuezeka. Sasa waliponiita mimi nikawaambia aah! Mimi ninakuja na alama yangu kama Zanzibar kama Mwakilishi, niweke majani nijenge madarasa mapya kuanzia chini mpaka juu. *Alhamdulillah* tukatengeneza madarasa hayo ya kisasa na kwa bahati nzuri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikwenda kuyafungua madarasa yale tarehe 18/Jula/2012, saa 10.00 jioni. (*Makofi*)

Ninashukuru siku ile ninafikiri Mhe. Waziri alidharurika na Naibu Waziri alidharurika jioni, Katibu Mkuu alidharurika, Naibu Katibu Mkuu alidharurika. Waliokuja ni wakurugenzi tu wale, makamishna wa elimu. Kwa sababu walikuwa na shughuli nyingi lakini Rais kwa bahati alikuwepo, Balozi wa Oman, China, India, Mama Asha Balozi na viongozi wa chama na serikali. (*Makofi*)

Ninashukuru lakini kwa bahati siku hiyo kulikuwa ndio ile ya kutia linta. Mhe. Rais akaahidi siku ile kwamba hii iliyokuwa kazi ya Wizara ya Elimu basi nitawambia na nitatoa *order* Wizara ya Elimu waje waezeke kwa sababu wananchi wameshafikisha nguvu zao kwa kufika kwenye linta.

Ninashukuru ilikuwa mwaka 2012. Kwa bahati nzuri mwaka 2013 kama kawaida yangu Tawi la Miwani Uzini, nilibahatika vile vile kulikuwa na kilio cha wanafunzi, nikenda kujenga madarasa mawili pale ya kisasa. Kwa bahati nzuri tarehe 26/06/2013, siku ya Jumatano ilikuwa asubuhi saa tano, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Seif Iddi alikuja kufungua skuli ile. (*Makofi*)

Kwa bahati mbaya vile vile Waziri, Naibu Waziri walidharurika. Ninashukuru Katibu Mkuu alikuwepo, lakini Naibu Katibu Mkuu naye alidharurika.

Mwaka huu tarehe 26 mfunguo tano mwaka 2014, kwa bahati nzuri Skuli ya Mgenihaji, unajua serikali yetu lazima tushirkiane pamoja tumefanya mengi. Walikuwa na upungufu wa vikalio madarasa mawili. Kwa bahati nikamtafuta mfadhili kutoka Dubai akaja akakabidhi vikalio kwa niaba ya huyu mfanyabiashara kutoka Dubai-Muhoma. Kwa hivyo aliyehudhuria ni Mama Shein na kwa bahati nzuri, Waziri, Naibu Waziri walidharurika, Katibu Mkuu alipatikana na Naibu Katibu Mkuu hakuwepo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, haya ninayazungumza *documents* zote ninazo na leo ningeliomba baada ya kusema yote haya nitayakabidhi mbele yako na kaseti na nini. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka mambo mawili. La kwanza tamko la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu haya majengo ambayo wanayoambiwa wananchi muyaezeke, serikali kupitia Wizara ya Elimu itamaliza.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka Waziri atoe tamko. Je, serikali iendelee kuwadanganya wananchi wafanye hivyo, halafu kila miaka mitano, sita iendelee kukaa kimya au ni sera ya Wizara ya Elimu kuwadanganya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, hiki kitabu mimi sikiungi mkono hata asilimia moja. Vile vile sitokubali na nitatoa shilingi yangu mpaka niridhishwe na matokeo yaliyotokea, wala siyaungi mkono bajeti ya Wizara ya Elimu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Rais kutoa agizo tarehe 9 mfunguo nane mwaka 2012, Katibu Mkuu aliandikiwa barua ambazo zote nitaziwasilisha. Aliandikiwa Skuli ya Pagali kukumbushwa kwamba ahadi ya Rais kupitia Wizara ya Elimu. Hapakuwa na majibu. Barua ya pili, tarehe 9 mfunguo nane 2012, Katibu Mkuu aliandikiwa tena barua. Barua mbili hizi, kuna barua samahani kulikuwa kuna barua ya tarehe 20 na kuna barua ya tarehe 22 mwezi tano.

Kuna barua ya tatu sasa. Katibu Mkuu anaandikiwa barua ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini kukumbusha ahadi ya Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu umalizaji wa jengo aliyotoa wakati wa Skuli ya Pagali kuezekwa kupitia Wizara ya Elimu. Mkuu wa Mkoa kamuandikia Waziri wa Elimu tarehe 22, baada ya mwaka mmoja. Hapakuwa na majibu vile vile, yote hayo barua zipo hapa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninataka kuuliza mimi ninavyomfahamu ninamtambua Rais mmoja tu katika nchi yetu hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein. Je, kuna mtu ana uwezo kuliko Dkt. Shein nchi hii, awe mkubwa au hii ni dharau kwa Rais ambae anatoa kauli mbele ya wananchi, mbele ya umma ya wananchi, halafu hapajatekelezwa hata jambo moja. Hizi ni *evidence*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe hayo kulikuwa na Skuli ya Kiboje, hii picha muione, yule mende huwezi kumfuga kwenye darasa. Hizi hapa, seuze ng'ombe, mende huwezi kumuweka madarasa ya Skuli ya Kiboje, ndio sekondari hapa. Nimetembea mimi haya. Nitampelekea Spika yote hizi, mende huwezi kumuweka ambapo skuli hii imefunguliwa na Kamandoo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Mapinduzi wakati ule Dkt. Salmin Amour Juma, leo Rais Mstaafu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuwadhalilisha viongozi wa kitaifa haliwezi kukubalika, *we can not compromise* katika nchi hii. Dkt. Salmin Amour Juma ameitumikia nchi hii, alikuwa kiongozi. Leo jengo hili limeekwa kama ni *show* ya kuonekana kudhalilishwa Rais Mstaafu Dkt. Salmin Amour Juma, yaani mende humu huwezi kumueka.

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, ninataka kumwambia Mhe. Waziri anajua hiyo Kiboje au kafika huo mtaa wa Kiboje kwenye skuli ya sekondari. Hivyo ndivyo walivyokusudia kuwafanyia viongozi hawa. Sasa ninachotaka Mhe. Mwenyekiti, aniambie Mhe. Waziri, kwanza akaliondoshe hili bango la aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, maana yake Skuli ya Kiboje ukiingia tu, ndio madarasa haya ambayo mende hawezi kukaa. Halafu madarasa mengine yaliyobakia hata yule ng'ombe huwezi kumtia mule ndani.

Mhe. Mwenyekiti, haya mambo, mama nitakuletea zote hizi nitampa, zipo nyingi tu...

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 5 za ziada.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, mbali na barua hii. Leo Wizara ya Elimu imenunua *furniture* milioni mia saba sitini na tisa kutoka Dar es Salaam. *Furniture* yenyewe ni ya sehemu moja tu ya *State University of Zanzibar*. Wanadaiwa milioni mia moja na thamanini na tano. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Unguja na Pemba majengo yao, serikali imetoa ahadi ya kumaliza, leo Wizara ya Elimu inakwenda kununua *furniture* kwa sehemu moja milioni mia saba na sitini na tisa, mia sita hamsini na tisa na bado wanadaiwa milioni mia moja na thamanini na tano, mia tisa sabini na mbili.

Mhe. Mwenyekiti, hizi pesa zingeliweza kumaliza hawa wananchi waliokuwa wameambiwa wafanye jitihada, halafu serikali itakuja kumaliza. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, huu ni udhalilishaji, huu ni ufisadi, huu ni kuumiza wananchi wasiokuwa na hatia katika nchi yetu. Hii hapa. (*Makofi*)

Sasa ninataka aje Mhe. Waziri aniambie, nani aliyekubali mkataba. Maana yake Mhe. Waziri hii Skuli ya Kiboje nilipotaka mimi kujenga na Wizara ya Elimu waliniambia, mwanzo walinikubalia tutashirikiana, tutatoa nusu *bin* nusu, mimi niendeleze. Hii barua yao Wizara ya Elimu. Siku ya pili Wizara ya Elimu imeniletea barua hii hapa serikali kwamba nakala Waziri, kwamba bwana sisi hatuwezi kushirikiana jambo hili Mohamedraza Hassanali Mohamedali kama tulivyoamua kwa sababu mpaka tupate kibali kutoka serikalini, Wizara ya Fedha. Yaani mimi ninataka kuwasaidia wananchi kumaliza ile Skuli ya Kiboje, hapa imeandikwa barua na serikali haiwezekani lakini wizara hii hii imekwenda kununua *furniture* Dar es Salaam kwa milioni zaidi ya milioni saba kwa mkono kwa maslahi ya sehemu moja, wakati mimi ninafanya maslahi ya wananchi walionituma, *with people's power*.

Sasa kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ninasema lazima tupate Kamati Teule na wajumbe wenzangu tumekuja hapa kwa sababu ya uchungu wa nchi. Haya mambo Mhe. Mwenyekiti, ni jambo ambalo na ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri aje aseme hapa basi hatuwezi kuwadanganya wananchi. Mwanzo kuna majengo mengi hayakumalizwa, wananchi munaendelea munawaambia jengeni. Tujenge suala kama hili linalokuja. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninachokuomba kuiomba wizara, mimi ninaishauri wizara irudi na bajeti hii ikalete tafsiri maalum isije kutudanganya tu hapa. Tumemaliza hii, kuna maskuli hayajamalizika na munaendelea kuwadanganya wananchi, munawaambia wananchi endeleeni. Hizo za miaka mitano hamukufanya. (*Makofi*)

Mhe.Mwenyekiti, ninasema hii serikali yetu, tunaijua lakini lazima tuwaambie wananchi ukweli. Kwa hivyo ni tamko la Serikali ya Mapinduzi iseme kwamba serikali wacha waendelee wadanganywe, waendelee kutengeneza linta, sisi tuendelee kuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo ninataka tamko la serikali au tamko la Wizara ya Elimu. Ninatamka kwamba hata hizi *furniture* kutoka Dar es Salaam tunao ndugu zetu hapa Zanzibar mafundi mbali mbali wangeliweza kutengeneza hizi *furniture*. Lakini *furniture* inatoka Dar es Salaam milioni mia saba, inakaribia bilioni. Hizi zingeliweza kumaliza matatizo yote ya skuli za Unguja na Pemba kwa majimbo mbali mbali. Mimi ninaamini Wajumbe wenzangu kama tutasimama kwenye *suratul mustaqim,* kila mjumbe mmoja kwenye jimbo lake hajamaliziwa jengo.

Labda waniambie tu kwamba kuweka jambo ambalo sio. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoomba kwamba wizara hii ukarudi, irudi na kama kuna uwezekano nitataka Kamati Teule hizi pesa serikali ilitiliana na mkataba na hii Skuli ya Kiboje, tamko la Wizara ya Elimu na mimi ninataka muende hata saa hivi, tamko la Wizara ya Elimu Skuli hii ya Kiboje, madarasa yale itolewe lile jengo, bango litolewe la Dkt. Salmin Amour Juma. Hatuwezi kuwadhalilisha viongozi.

Vile vile katika skuli hiyo hiyo ya Kiboje wananchi wameambiwa jengeni haikuezekwa mpaka leo, zaidi ya mwaka na barua hii walionipa *estimates*, baadae wakaniambia bwana haiwezekani na *estimates* walinileta hiyo. Tukakubaliana sote.

Mhe. Mwenyekiti: Muda wako umemalizika.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti,mimi niendelee kushukuru na naomba hizi kaseti zilizofunguliwa skuli mbali mbali zote, hii ya Mama Shein na ahadi walizozitoa Marais, *documents* zote hizi za *furniture* milioni mia saba, barua za Wizara ya Elimu naomba nikukabidhi zote mbele yako. Kama nilivyokwambia Mhe. Mwenyekiti, mimi tokea nimeingia Barazani, nina ushahidi wa jambo lolote, chochote kile.

Mhe. Mwenyekiti: Muda wako umemalizika.

Mhe. Mohamedrasa Hasssanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, hivyo ninashukuru sana siungi mkono. Ninatoa shilingi, sikubaliani naye mpaka nipate maelezo ya kutosha. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi simameni katika suala la nchi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nikukabidhi Mhe. Mwenyekiti, hizi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa ni nafasi ya Mhe. Mussa Ali Hassan na baadae kama muda ungalipo ataendelea Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wizara hii inajitahidi sana kuweza kushughulikia mambo mengi ya elimu na hasa miaka hii ya sasa kwamba vijana wetu wengi wanafaulu. Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri ili kuweza kutusaidia katika maskuli yetu hasa katika Jimbo la Koani, kwa kweli tuna ukosefu wa walimu wa sayansi kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo naomba Mhe. Waziri mwaka huu wa fedha atakapotumia ahakikishe kwamba walimu wa sayansi wanapatikana katika skuli zetu za Jimbo la Koani. Kwa kweli tuna ukosefu mkubwa sana na watoto wetu hivi sasa kupasi kwao sio kama hapo, kwa sababu mwanzo walikuwepo walimu wengi wa sayansi lakini wengi wameondolewa kupata *transfer* kupelekwa katika maskuli mengine. Hivyo ninamuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba anatupatia tena walimu hawa ili kuendeleza masomo katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna matatizo kwenye skuli zetu, tuliahidiana na Mhe. Waziri ili tukizianza yeye atamaliza kututilia bati katika skuli zetu. Ninashukuru Skuli yetu ya hivi sasa Bungi tumefanikiwa lakini tulikwenda sambamba na skuli ya Koani kwenye *shell,* ina muda mrefu sana na pale hatuna mabanda mengi. Tuna mabanda mawili tu ambayo yanasaidia watoto. Watoto ni wengi hivyo hawana sehemu ya kusomea hasa itakapofika kwenye mwezi wa Januari ya mwaka huu. Mhe. Waziri tunaomba lile banda letu Mhe. Waziri atusaidie, ili atumalizie kama tulivyokubaliana kuhusu kupata bati katika Skuli yetu ile ya Koani.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo kubwa kwenye nchi yetu ya Zanzibar. Hivi sasa tuna matatizo ya vijana wetu wamekosa masomo muhimu sana ambayo yalikuwa yanatusaidia sana, wanafunzi wote wa Zanzibar ili kuwa na historia ya nchi yetu. Hivi sasa nchi ya Zanzibar kwa kweli hakuna historia. Hili suala ninamtaka Mhe. Waziri akija anieleze kwa nini somo hili limeondoshwa katika skuli zetu za *Primaries* hadi *Secondaries*.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Waziri akija kama si yeye aliyeondoa, anihakikishie ni nani aliweza kuondoa historia ya Zanzibar, na kwa nini wanafunzi wawe hawafahamu historia ya nchi yao. Je, Mhe. Waziri kuna nchi yoyote ambayo hakuna historia ya nchi yake. Kuna nchi yoyote ambayo haisomeshi historia wanafunzi wao, historia ya nchi yao. (*Makofi*)

Kwa kweli Mhe. Waziri kama hakunihakikishia suala hili nitaondoa shilingi yangu katika kuchangia bajeti hii. Kwa hivi sasa wanadanganywa sana kwamba hawaijui historia ya nchi yao, unalowaambia lolote hata ukiwaambia embe ni chungwa wanakubaliana na hilo kwa sababu hawana historia wa wazazi wao, enzi na enzi ilivyoanza historia ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tuna matatizo mengi ya skuli zetu na vyuo vya Kiislamu. Walimu wanajitahidi sana kusomesha vyuo hivi vya Kiislamu. Lakini utakuta kwa kweli hazihudumiwi hasa na serikali kama vyuo vyengine. Utakuta vyuo vingi vya Kiislamu mabanda yake ni ya makuti, vumbi chini, hakuna saruji na watoto wake wanakwenda nguo mbovu mbovu tupu. (*Makofi*)

Kwa kweli Mhe. Waziri avipitie vyuo hivi vya Kiislamu ili navyo viweze kushughulikiwa kuweza kusomeshwa katika mahala bora na walimu wake wawe bora, pamoja na walimu kusaidiwa angalau kupata posho, sio wajitegemee. (*Makofi*)

Wengi wanaosoma katika vyuo vya Kiislamu hawapati shahada zao za kumaliza angalau wanapomaliza misahafu, angalau kupata shahada kwamba huyu mtu amefikia lengo kwamba amehitimu chuo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri tunaomba katika skuli zetu ahakikishe na mabanda ya chekechea yanapatiwa ufumbuzi kwamba kila skuli ina banda lake la chekechea angalau iwe mwanzo mzuri wa wanafunzi kuweza kusoma chekechea, halafu waende *primary* kwa wakati mzuri. (*Makofi*)

Kwa hivyo mimi ninafikiri nisiwe na mchango mwingi ila tu Mhe.Waziri akija atuhakikishie kwamba ameweza kutupatia yote ambayo tumeyahitaji upande wa sekondari na *primary* na upande wa vyuo na upande wa chekechea, ili skuli zetu ziwe bora na ziwe za kisasa katika maendeleo na vile vile katika skuli nyingi hivi sasa zinahatarisha sana amani za wanafunzi. Nafikiri wizara wanawekwa wakaguzi wa skuli, wakipita skuli waangalie usalama wa

wanafunzi, magari yanapita karibu na skuli kwa mbio nyingi na utakuta Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikuwa ni kazi yake kuweka matuta kwa ajili ya wanafunzi. Lakini kwa vile wao sio wenye watoto basi utakuta skuli nyingi hazina matuta kwa sababu usalama ule Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano sio kazi yao.

Kwa hivyo, tunawaomba wakaguzi wanapopita basi wahakikishe kwamba kila skuli ina usalama wa wanafunzi, angalau kupata matuta mawili au matatu na hasa ukitizama katika jimbo langu kuna skuli ya pale Bungi kwa kweli kunahatarisha sana wanafunzi; gari zinakimbia na hakuna *cross*, na ukisikia ajali kubwa zinazotokea pale Bungi. Ni hatari sana hazipungui kuuwa watu kuanzia 10 na kuendelea. Kwa hivyo, naomba akija Mhe. Waziri skuli ile anihakikishie wakaguzi wake wataweka matuta.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naiomba skuli ya Nyerere hapa Mjini, pale ni hatari sana, kutwa wanakaa askari jamii kuweza kuwavuasha watoto, hakuna tuta kwenye sehemu ile. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa usalama wa wanafunzi wakienda wakaguzi basi wahakikishe kwamba skuli ile wanaipatia matuta. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa mchango wangu huo, naomba Mhe. Waziri akija yote yale ambayo tumeyaomba ayatolee ufumbuzi na mpango mzima wa kuweza kufanikiwa mahitaji yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa kujali muda. Sasa ni nafasi ya Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadaye Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Tuzingatie muda.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata fursa ya kutoa machache kuhusu wizara hii muhimu ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa leo kuendelea na kazi zetu za kawaida.

Vile vile nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na nimpongeze Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa dhati, kwa namna alivyoiwasilisha hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nianze kidogo na hii dhana ya elimu bila malipo; dhana hii ilitangazwa mara tu baada ya Mapinduzi kwa wanafunzi wa Zanzibar watasoma bila malipo. Lakini jinsi tunavyoendelea dhana hii pole pole inafifia, ingawaje serikali inasema hatulipi tunachangia. Ningetaka Mhe. Mwenyekiti, wizara inifafanulie kulipa ni vipi na kuchangia ni vipi, ili nipate maana na tofauti ya mambo haya mawili. Kwa sababu kulipa unatoa pesa na kuchangia unatoa pesa, kwa hivyo nataka nijuwe tofauti yake ni ipi katika mambo mawili haya.

Mhe. Mwenyekiti, elimu Zanzibar inakuwa, lakini kuna majengo ambayo mimi nilipokuwa mwalimu, kuna jengo moja hivi sasa ni taasisi ya Chuo Kikuu, mimi niliwahi kufanya *practice* ikiwa ni skuli ya msingi. Lakini jengo lile lile leo limepata hadhi ya Chuo Kikuu, elimu imepanda lakini tunatumia jengo lile lile. Hili jengo wakati wangu mimi lilikuwa linaitwa Kidutani B, liko pale *Majestic* kwenye taasisi ya Chuo Kikuu. Mimi nilikwenda pale *Teaching Practise* kwenye jengo lile ambalo lilikuwa likiitwa Skuli ya Kidutani B na nilikwenda pale kufundisha darasa la sita. Mhe. Mwenyekiti, leo jengo lile lile limetiwa rangi tu lina hadhi ya Chuo Kikuu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa ile kuweka saini na Serikali ya Oman juu ya ujenzi wa Kituo cha Utamaduni pale Chuo cha Kiislamu cha Mazizini. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili ni zuri na hotuba imeonesha humu kuwa ujenzi huo umeanza. Kwa kweli kuwepo kwa utamaduni wa Kiislamu utatusaidia kuweza kujua dini yetu na hadhi yake. Kwa kuwa jengo lile ndani yake kutakuwa na Msikiti ambao utakuwa unafanyiwa ibada na kutolewa mawaidha mbali mbali ya Kiislamu ni jambo zuri. Kwa hivyo, niipongeze serikali kwa kukubali kujenga hilo jengo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na uzuri huo ningeiomba serikali isimamie vizuri ujenzi huu ili uendane na hali halisi.

Pia hapa palizungumziwa ufaulu wa wanafunzi kuwa umeongezeka. Lakini hapa mimi nitazungumzia ufaulu wa wanafunzi wa darasa la kumi na mbili yaani *Form Four*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mtizamo wangu mimi ufaulu unapungua kwa sababu niliposoma mimi viwango vya kupasi vilikuwa ni vya daraja 5, ya tano ni ya ku-*fail*. Ilikuwa kuanzia sifuri hadi 34 unapata F ume-*fail*. Lakini nadhani hii sifuri hadi 34 imegaiwa na mtu anapata *marks* ndani ya lengo hili anapewa E kuwa ka-*pass*. Kwa kweli huku ni kuidumisha elimu, huwezi *marks* za mtu ambae alikuwa ana-*fail* ukazitengeneza kidogo na kuzifanya kuwa ni za mtu ambae kafaulu, kwa kiwango cha *Form Four*. Hapa elimu tunaidumaza badala ya kuikuza, tunapata watoto

wengi tunasema wame-*pass* kumbe kama wangesoma na mimi ingekuwa wame-*fail*. Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa ni kuidumaza elimu, kwa hivyo hii mimi siikubali kuwa elimu kiwango chake cha kufaulu kimepanda, hakikupanda hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu Idara ya Sera, Mipango na Utafiti kwenye mradi wa ujenzi wa Chuo cha Kiislamu ambayo hii nadhani nitaikuta kwenye ukurasa wa 10 na wa 11. Mhe. Mwenyekiti, hapa ilizungumziwa kuhusu kuendeleza ukarabati wa majengo ya Chuo cha Kiislamu kiliopo Micheweni. Lakini hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2014 hakuna fedha za SMZ zilizotolewa na hivyo hakuna kazi zilizotekelezwa. Kwa hivyo, hakuna kilichofanyika kwa upande huu wa Chuo hiki cha Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti, chuo hiki ni muhimu na kina haja ya kuendelezwa, lakini serikali hakuna fedha iliyoingizwa. Kwa hivyo, ningeomba nijuwe kwa nini kisiingiziwe fedha hata kidogo. Mhe. Mwenyekiti, niende sasa kwenye viambatanisho katika ukurasa wa 106, kiambatanisho hiki kinazungumzia mabanda ya madarasa yaliyofikia hatua ya kuezekwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika jimbo langu katika kijiji cha Mahudusi, mwaka jana banda hili lilikuwa katika mabada ambayo yaliingizwa kuwa yataezekwa na yalitajwa banda moja, mbili na hili likawa ni banda la tatu. Lakini licha ya bati hata kuti serikali haikuleta. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Mwenyekiti, mimi sio mpigaji buti na hata hili sitolipigia buti, lakini nataka anipe maelezo ya kunitosha, kwa nini hili banda ambalo ni la vyumba vinne tu ofisi na vyoo halikufanyiwa hatua yoyote na tayari limekabidhiwa kwa serikali na mwaka huu limetolewa tena kwa Wilaya ya Mkoani limetajwa katika nambari moja.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Mwenyekiti, serikali mwaka jana haikutekeleza, hivyo mwaka huu ningeomba hili banda limalizike ili kuwaondolea watoto usumbufu wa kufuata skuli mbali, ama waende Kengeja au Mtambile ambako ni masafa marefu sana. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala hili serikali ni lazima iwe makini, inapoahidi kuwa itafanya kitu fulani basi ni lazima kitu hicho kitekelezwe. Kwa sababu hii ahadi mnayoitoa kwa wananchi, tena kwa kupitia chombo hiki ambacho kinasimamia hiyo serikali, sasa serikali inapokuwa haijatekeleza na bila ya kutoa maelezo yoyote kwetu, kwa kweli hatujisikii vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuliposoma ni kweli elimu ilikuwa bila ya malipo, mimi mwaka nilioingia *Form One*, jioni ya siku niliyofika pale skuli mwalimu wa zamu, kulikuwa hakuna *baser Fidel Castro*, alitukusanya wanafunzi wapya na kutuita mwanafunzi jina mmoja mmoja. Kwa mfano zamu yangu aliniita Mohammed Haji Khalid nikakabidhiwa chandarua, sikuambiwa niende na mbanjo kama wanavyokwenda navyo wanafunzi wa sasa. Vile vile nikakabidhiwa *blanket*, shuka na vyombo vyote, mpaka sabuni ya kuogea, sabuni ya kufulia na kibati cha *blue band* nitumie. Mimi nilisoma bila ya malipo, lakini mwanangu ninayemsomesha hivi sasa, mimi binafsi pamoja na uwakilishi wangu lakini maji yamenifika ya shingo. Nina wanangu wanasoma kiasi watatu katika vyuo, hawana mikopo. Itazameni hiyo hali niliyokuwanayo nawasomesha watoto watatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Kwa hivyo, hii hali Mhe. Mwenyekiti, ningeomba serikali izidi kuongeza hii bajeti ya mikopo ili wanafunzi wengi waweze kusaidia kuondoa matatizo kwa wazazi wao, kwa sababu elimu ni muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kidogo na kwa sababu mimi nilikuwa mwalimu. Nije kwenye maslahi ya walimu ni lazima yaangaliwe. Mhe. Mwenyekiti, walimu wanaostaafu hivi sasa waliofanyakazi kwa muda mrefu wako hatarini sana, kwa sababu maslahi yao ni madogo na wanastaafu, kwa hivyo hicho watakachojaaliwa pia kitakuwa ni kidogo cha kuweza kumudu maisha yao.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, hao walimu wa zamani angalau wapewe *promotion* ya mishahara, ingwaje wao sio wanaoajiri siku hizi ili wakiondoka angalau viinua mgongo vyao viwe vimetononoka.

Halikadhalika hii sera ya serikali ya kuwa mtu anapokwenda likizo anapewa shilingi 100,000 ni vipi, mbona wakati wetu sisi ilikuwa, kwanza mtu yeyote katika nchi za Afrika ya Mashariki alikuwa anapangiwa kulingana na kule anakokwenda. Maana yake maana ya likizo ni mtu anakwenda kupumzika, leo kama mtu hana mtoto shilingi

100,000, kama ana watoto sita shilingi 100,000, ana wake wanne shilingi 100,000. *Formula* hii hasa serikali imeipata wapi.

Mhe. Mwenyekiti, yako mambo mabaya ya Kikoloni yawacheni, lakini yale mambo mazuri ya Kikoloni yachukuweni. Ilikuwa mfanyakazi anapokwenda likizo ana hadhi zake maalum kulingana na pale anapokwenda kutumia likizo na watu ambao atafuatana nao, awe ni mkewe, mumewe na watoto wanne. Pia watu wanatofautiana kulingana na pahala anapokwenda kutumia likizo yake, sijui huu mfumo sisi tumeupata wapi maskini! Mfumo ambao hauna mfumo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kuwa tunaimarisha masomo ya dini ya Kiislamu, nashukuru sana. Hivi karibuni tuna Masheikh wetu ambao ni Wahadhiri wa dini yetu, ambao walipata mitihani na hatimae wameachiliwa kwa dhamana, lakini hata mawaidha ya mule ndani ya Msikiti nasikia wamezuiliwa kutoa. Kwenye hadhara sio sawa, lakini na iwe hivyo wazuiliwe wasitowe, lakini hata wanapokwenda kusali kutoa mawaidha mule nayo ni makosa, je, hapo si kubana uhuru wa kuabudu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hapa jambo hili sio zuri, kwa sababu Uislamu unataka kuendelezwa, kuimarishwa na hasa vile ambavyo umeingiliwa na tamaduni za Kimagharibi. Leo kama wale watu ambao wana uwezo wa kutuelekeza hata ndani ya Msikiti anaambiwa usitowe maelekezo. Hii kwa kweli sio haki na pia ni kukiuka haki za kuabudu na uhuru wake mtu, hasa pale ambapo havunji wala hakiuki sheria na taratibu za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache ningemuomba Mhe. Waziri aje anieleze vizuri kwa tungo, kwa nini mwaka jana hili banda la Mahudusi halikuezekwa na mara hii kalitaja tena kuwa litaezekwa. Kwa hivyo, anihakikishie vyenginevyo nitakuja kupiga buti, ingawa sio mpigaji wa buti. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Ahsante sana, anayefuata Mhe Hussein Ibrahim Makungu na kama muda utakuwepo Mhe. Saleh Nassor Juma jitayarishe.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukawa katika hali ya uzima na afya njema.

Pia nakushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Vile vile nimpongeze waziri Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kwa hotuba yake nzuri na imetufahamisha mambo mengi kabisa katika elimu ambayo ni kitu muhimu sana katika nchi hasa kwa watoto wetu hawa wanaosoma sasa hivi.

Pia niwapongeze sana niwapongeze sana wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kazi yao nzuri tena kubwa chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mgeni Hassan Juma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 3 kifungu cha 10. Katika ukurasa huu ninaipongeza sana serikali kwa mafanikio yaliopatikana kwa mwaka 2013/2014 kuhusu ujenzi wa skuli tatu mpya za sekondari za ghorofa kwa Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa kweli katika hili ninaipongeza sana serikali yetu pamoja na uhaba wa fedha na uchumi wetu mdogo, lakini imeweza kujenga skuli tatu za ghorofa na hilo ni jambo kubwa na la kupigiwa mfano katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Naomba niseme, kwamba tunajenga skuli za ghorofa za kisasa tena zina uwezo, lakini suala la kuzishughulikia skuli hizi inakuwa ni tatizo. Kwa mfano, tunaweza kujenga ghorofa, lakini zile skuli zetu za zamani zilizojengwa miaka ya nyuma ziko katika hali mbaya na zinatumika wananchi wetu kusoma, kwani skuli bado ni kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Skuli ya Kengeja ambayo iko Pemba kama Mhe. Mjumbe aliyemalizia hivi sasa Mhe. Mohammed Haji Khalid tulikwenda katika Jimbo lake la Mtambile Kengeja. Kwa bahati tulikwenda kuangalia skuli, kwa kweli skuli inatia huruma na wananchi wanapata tabu sana na Mhe. Mwenyekiti na wewe ulikuwa shahidi ulikwenda na Kamati yako ya Mawasiliano na Ujenzi, tukaiona ile skuli hali yake ilivyo. Watoto wanakaa chini na hapo chini penyewe hata ile sakafu haipo, kuna mawe, yaani wanakaa juu ya mawe, skuli inavuja na madarasa yote mabati mabovu.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba iangalie skuli kama hizi kwanza, kwa sababu tunajenga majengo mapya lakini na skuli hizi zifanyiwe marekebisho kwani hawa watoto wanakuwa wanasoma kwenye hali ngumu na hata ile elimu yenyewe sidhani kama itakuwa wanafahamu vizuri, kwa sababu skuli ina joto sana na ikinyesha mvua inavuja.

Vile vile, nije kwenye Skuli ya Sekondari ya Bububu, ambayo iko ndani ya jimbo langu. Kwa kweli skuli hii iko katika hali mbaya, watoto wengi wanasoma katika darasa wanafika 120 mpaka 130, pia hivi sasa skuli inavuja mabati mabovu pamoja na Skuli ya Msingi ya Bububu pia inavuja mabati mabovu.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia suala la uzio katika skuli ile. Skuli ile ni nzuri na wala haina uzio na watu wanakuja tofauti na kukaa kwenye eneo lile wanauza madawa ya kulevya na kupelekea kuwaharibu wanafunzi akili zao. Kwa hivyo, naiomba sana wizara iangalie sana suala la uzio kwa skuli ile, kwa sababu itawajengea mazingira mazuri wanafunzi wale na waweze kusoma na kuwa raia wema katika nchi hii.

Jambo jengine, ni suala la wizi ambalo limekuwa ni tatizo, yaani wanafunzi wanaibiwa na mpaka walimu wakiweka vifaa vyao vinaibiwa na hali hiyo inapelekea kukosekana kwa amani na usalama. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, alingalie suala hili la uzio kwa Skuli ya Bububu.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwamba skuli ile tayari inayo hatimiliki na eneo lipo kubwa. Vile vile ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata hizi skuli mpya tunazojenga za kisasa kwa kupitia wizara yako, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aangalie eneo la Bububu Skuli ambalo ni eneo zuri tena liko pwani kabisa na linatosha kujenga skuli ya ghorofa pale.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, kuna skuli Sharifumsaa imejengwa na wananchi kwa muda mrefu imefikia hatua ya karibu kuweka *linter* na mpaka leo ile skuli imekaa. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aliangalie na hilo kwa kupitia sisi Wawakilsihi na Wabunge pamoja na wizara tusaidiane, kwamba ile skuli tuiezeke, ili watoto waweze kusoma kwa sababu skuli ile itasaidia watoto wengi wa eneo lile kupunguza kuja mjini kwa ajili ya kusoma; kwa kweli wanafunzi wanapata usafiri na mambo mengine.

Ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aiangalie skuli hii ambayo iko Sharifumsaa juu bado haijesha na hii imejengwa kwa nguvu za wananchi pamoja na kupitia wafadhili mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa kweli elimu ni muhimu na watoto wanakabiliwa na changamoto kubwa sana, ili waweze kupasi. Sasa nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba watoto wanataka kusoma na uwezo wa kusoma wanao lakini mambo mengi yanawakwaza kama vile maisha yao ni duni, usafiri pamoja na vifaa vyengine mbali mbali inakuwa shida kweli.

Naomba kutoa mfano, mdogo tena ni mzuri kabisa mwaka juzi wanafunzi wote wali-*fail* skuli nzima kidato cha nne (*Form IV*). Mhe. Mwenyekiti, nilisikitika sana kuona kwamba wale vijana wali-*fail* wote nikaona sijambo jema bora niende nikawasikilize, lakini kabla sijenda nilipita kwa Mhe. Makamu wetu wa Pili wa Rais na kunipa ushauri mmoja mzuri sana ninamshukuru na ushauri huo niliuchukuwa na yeye alifanya kwenye jimbo lake Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Kwa bahati nilipokwenda skuli na kuzungumza na wanafunzi wale, kwa kweli wanafunzi wanavyo vipaji tena wazuri na wao uwelewa mzuri wa kusoma, lakini wanataka *motivation* kama vile kuahidiwa vitu au kupatiwa vitu, ili wapate nguvu ya kusoma. Kutokana na hali hiyo, niliwaahidi mwanafunzi mmoja akipasi nitampa shilingi 100,000/= kwa vile mwaka jana hakupasi hata mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, ninawashukuru pamoja na kuwapongeza wanafunzi wale kwa mwaka huu uliokwisha mwaka 2013/2014 wamepasi wanafunzi 53, kwa kweli nilifarajika sana na niliwapa zawadi ile wanafunzi wale na walifurahi pamoja na wazee wao. Kwa hivyo, ninaomba utratibu kama huo Mhe. Mwenyekiti, kwamba wanafunzi wanataka wapate *motivation*, ili waweze kusoma na kupasi vizuri na baadae wawe raia wema na kupata ajira zenye heshima na zenye kufuata maadili pamoja na mila zetu.

Naomba nimalizie suala la upungufu wa walimu. Kwa mfano, Skuli ya Bububu mwalimu huyo anasomesha *Science, Geography, Mathematics*. Kwa kweli walimu hawawezi na wakati mwengine wanasukuma tu. Mhe. Waziri namuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba sisi tulipokuwa tunasoma nakumbuka Mwalimu wangu alikuwa Sanya wa *Geography*, yaani yeye alikuwa akitoka darasa moja kwenda jengine somo lake ni *Geography*.

Kwa hiyo, ninamshukuru mwalimu wangu Sanya ambae hivi sasa ni Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe amenisomesha *Geography*, lakini alikuwa mwalimu mwenye kuelewa kazi yake tena wakati akisomesha unafahamu kile anachokisomesha. Kwa kweli ninampongeza sana mwalimu wangu huyu kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba walimu wengine pia waangalie wawe na hali kama hii ya walimu wa zamani, yaani wapate kazi ndogo ndogo sio mwalimu mmoja anasomesha masomo 6. Kwa hivyo, naomba utamaduni huo uondoke na tujitahidi mwalimu mmoja kwa somo moja.

Hata hivyo, kuhusu suala la maslahi ya walimu ni madogo. Mhe. Mwenyekiti, tunao walimu wazuri lakini wanashindwa. Kwa mfano, mzuri Mbunge wa Mji Mkongwe mwalimu mzuri wa *Geography* lakini ameacha kusomesha amekwenda kwenye ubunge, kwa ajili ya kufuata maslahi mazuri zaidi. Lakini kama mwalimu yule angekuwa analipwa vizuri asingehama mpaka leo angebakia kuwa mwalimu mzuri na angesomesha wanafunzi tofauti na kuweza kutoa vipaji vizuri pamoja na wataalamu wazuri kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, walimu wanaacha ualimu na kwenda kwenye kutafuta maslahi binafsi na kuacha ile fani ya ualimu, kwa sababu mshahara ni mdogo sana Mhe. Waziri, hivyo tuangalie. Kwa mfano, unafika skuli unaona mwalimu anauza biashara anakuja na kachori au badiya ama malai na wakati mwengine anakopesha wanafunzi, kwa ajili ya kuongeza kipato yule mwalimu.

Mhe. Waziri ninamuomba sana kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, walimu waangaliwe sana mishahara yao, nyumba zao wanazoishi, usafiri wao wa kwenda skuli inakuwa ni matatizo makubwa, wakati mwengine wanaomba *lift* daladala zinakuwa shida.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuangalie suala la walimu wetu kuhusu usafiri wao uwe wa uhakika pamoja na kuwaandalia mambo maalum walimu. Kwa kweli sidhani serikali kama inashindwa kuwaandalia mazingira mazuri hawa walimu wetu, inawezekana kabisa tukiamua tu, ili waache kufanya biashara ndogo ndogo na washughulike na masomo, kwa ajili ya kuwasomesha wanafunzi wetu kwa lengo la kuwa raia wema pamoja na kusoma vizuri na kupasi.

Nizungumze kuhusu suala la michezo kwenye skuli zetu limepungua sana. Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka zamani nilipokuwa nikisoma kwa kweli michezo ilikuwa iko juu. Kwa mfano, Skuli ya *Haile Sela Sie* tulikuwa tukisoma pale kulikuwa na mchezaji mmoja akiitwa Dua Said, kipaji chake kizuri cha michezo, yule mchezaji akaweza kununuliwa *Small* Simba, baadae akaenda Simba na hata kufika kwenda kuchezea Falme za Kiarabu ambazo ni kubwa kubwa.

Sasa kipaji kile kimemsaidia sana na akapata kama ajira na hata kusoma aliacha. Mhe. Mwenyekiti, vipaji vipo kwenye skuli zetu vingi sana, lakini vinashindwa kuonekana vipaji hivi. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aliangalie sana suala la michezo kwa watoto wetu. vile vile suala la michezo ya kuigiza hivi sasa imekufa sana katika skuli.

Kwa hiyo, naomba michezo hiyo irudi kama zamani, kwani wataalamu pamoja na wazoefu wapo na michezo ya kuigiza hivi sasa kama tunavyoona *films* tofauti na watu wanapata ajira kupitia njia hizi za utamaduni bila ya kutegemea serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla michezo ya aina tofauti tuzingatie sana na pia ukiwemo mchezo wa riyadha na Mhe. Asha Bakari Makame na mimi napenda kusisitiza tuangalie sana kwenye skuli zetu masuala haya yote.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la gharama za uendeshaji wa skuli za serikali. Mhe. Mwenyekiti, ninasikitika sana kwamba suala hili ninakwenda skuli nakuta umeme umekatwa na ukiuliza unambiwa deni ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati aondoshe haya madeni ya umeme kwa skuli na iwe kama msaada kutoka serikali yetu kwamba suala la umeme kwa skuli zetu iwe ni *free*, kwa sababu skuli zikikosa umeme *computer* wanafunzi hawawezi kutumia.

Kwa kweli hivi sasa kusoma kwetu *technology* imepanda, yaani huwezi kusoma bila ya kuwa na *computer*, wakati tuliposoma sisi ni mabuku na makaratasi, lakini hivi sasa mwanafunzi awe na *computer*. Sasa bila ya umeme wanafunzi wetu tunawapa shida. Mhe. Mwenyekiti, nimeshawaona wanafunzi wengi hivi sasa wanakwenda skuli wakiwa na simu, tena simu hii ina mambo mengi kama vile mambo ya *network*, yaani unapata mambo yote kwenye simu na mtu akifungua anapata mambo mengi ya kusoma kwenye simu na kwenye *computer* ndio hayo hayo.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba skuli zetu kukosa umeme ni tatizo kubwa na linarejesha nyuma wanafunzi wetu katika masuala ya kimasomo yao. Naomba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba asamehe bili za umeme katika skuli zetu, ili tuwape nafuu wanafunzi wetu waweze kusoma vizuri na waondokane na gharama za kuchangia masuala ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *uniform* pamoja na mabuku liangaliwe, wasaidiwe hawa wanafunzi kama tulivyokuwa tunasoma sisi. Kwa kweli tulikuwa tunapewa makubu pamoja na kalamu bure. Kwa hiyo, ninaomba jambo kidogo ninajua serikali yetu ni masikini, lakini inaweza kusaidia japo kwa *motivation* kwa wale watoto waliopasi, yaani wasaidiwe kama hivyo na inatosha na wataweza kusoma vizuri.

Suala la usafiri nalo ni tatizo kubwa kwa wanafunzi wetu na wala sio kwa skuli za Bububu ni skuli zote kufika mjini, kwa kweli wanafunzi wanasumbuliwa na kudhalilishwa wanafunzi kwenye daladala na hasa wanafunzi wa kike. Mhe. Waziri ninamuomba sana kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aangalie sana suala la usafiri kwa wanafunzi wetu. Kwa mfano, juzi niliangalia televisheni na niliiona Skuli ya Kiembesamaki kuna mfadhili ametoa mabasi matatu kwa ajili ya wanafunzi wa Skuli ya Kiembesamaki.

Kwa kweli ninampongeza sana na hawa wafadhili wengine wajitokeze kusaidia skuli nyengine na wala sio skuli moja inayosaidiwa na wafadhili wengine kama vile mabenki zikiwemo *CRDB*, *NMB*, *PBZ* zisaidie skuli zetu katika suala la usafiri kwa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, ninaona hasa kwamba wanafunzi wanapata tabu, kwa sababu ninawachukua wanafunzi wangu kila siku asubuhi, mchana na jioni; *trip* mbili kwa siku na gharama za uendeshaji zote ninatoa mwenyewe, kwa sababu najua gharama ni kubwa mno. Lakini namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie na anipe uwezo, ili niweze kutekeleza suala hili, kwa sababu sio kwa manufaa yangu peke yangu au manufaa ya wananchi wangu, isipokuwa ni mafunaa ya taifa zima. *(Makofi)*

Kwa kweli wale wanafunzi watakaposoma watakuja kusaida taifa hili la Zanzibar na taifa jengine na hata duniani kote. Kwa maana hiyo, na sisi wafadhili wengine mbali mbali nawaomba wasaidie kuhusu suala hili la usafiri kwa ajili ya wanafunzi wetu wasipate tabu, ili wafike skuli kwa wakati na waweze kusoma vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ninaipongeza sana serikali kwa kujenga majengo mapya tena ninawapongeza kwa uwezo pamoja na upeo wao mzuri. Lakini ninasikitika sana Mhe. Mwenyekiti kwa hawa wafadhili wanaojenga hizi skuli ni kwamba wanachukua fedha nyingi, lakini skuli hazina ule uimara wa kudumu kwa miaka mingi baadae kama 10 au 20 mbele.

Kwa mfano, utakuta skuli zinajengwa na wafadhili wanachukua fedha pamoja na serikali inachangia fedha, lakini skuli baada ya miezi 6 skuli inabanduka *tiles* au inavuja, rangi si ya uhakika; miundombinu ya maji na umeme si ya uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri Skuli ya Faraja (Kwamtipura), Skuli ya Uzini zimeshabanduka *tiles*, yaani skuli hizo zimejengwa hivi karibuni na wala hazijafika miaka mingi. Kwa hiyo, tunaomba hawa wakandarasi wanaopewa kujenga hizi skuli waangaliwe ambao wanaoweza kuisaidia nchi yetu kwa nia safi na njema na wala wasiwe matapeli wakaja kuchukua fedha na kuondoka. *(Makofi)*

Nimalizie kwa suala la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali yetu kwa kweli inavunja moyo kwa upande mwengine. Kwa mfano, tukiangalia hata Wizara ya Afya juzi hapa wafadhili wa maendeleo wanatoa fedha

kutusaidia, lakini serikali yetu mchango wake unakuwa mdogo, wafadhili wanarudi nyuma wanaona hawa tunawasaidia, lakini wao wenyewe hawasaidiliki.

Kwa maana hiyo, ninaomba hawa wafadhili wanapochangia Mhe. Mwenyekiti na sisi serikali kupitia wizara tuwasaidie fedha fulani, ili na wao wapate moyo kama wao wakitoa asilimia 50 ya mradi na sisi tujitahidi tutoe angalau asilimia 50, kwa ajili ya kuonesha kwamba na sisi tunao moyo na imani ya kuchangia hizi fedha, kwani wakitoa wao tu hizi fedha watarudi nyuma na kuvunjika moyo kwa miradi mingine.

Niwapongeze sana hawa wafadhili wanaotusaidia na mpaka hivi sasa wametusaidia vitabu hivi kwa miradi mingi ya skuli kama vile *UNESCO, GPA, USAID, SIDA, UNICEF*. Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki kinaonesha wamesaidia karibu bilioni 1 katika miradi mbali mbali, haya mashirika ya maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hapo kwa vile muda ni mdogo na ninaunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala la afya na elimu tutoe kipaumbele sana na kuwaingizia fedha Waheshimiwa Mawaziri, ili waweze kuendeleza haya mambo ambayo waliyoyaandaa humu pamoja na wafadhili wetu, kwa ajili ya kuweza kufanya miradi mingine kwa mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Baada ya hayo, Mhe. Mwenyekiti ninasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, muda tulionano naona ni mdogo sana na wala hautotosha kwa mtu yeyote tutakayempa kwa ajili ya kuchangia. Kwa hivyo, tutawapa nafasi nzuri zaidi wachangiaji, ili wazidi kujipanga vizuri na jioni tutaanza na Mhe. Saleh Nassor Juma, atafuatiwa na Mhe. Raya Suleiman Hamad na baadaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu na atafuatia Mhe. Marina Joel Thomas. Waheshimiwa Wajumbe, tutaanza na watu hao na wengine wataendelea, kwa sababu ninayo orodha ya watu 11. Kwa hivyo, naakhirisha kikao hiki mpaka jioni saa 11:00 leo.

(*Saa 6:56 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka jioni saa 11:00*)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirejea)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, haraka haraka nataka kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na hatimae kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa wazima wa afya na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu tunayoishi hadi hapa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia allah na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru, ama baada ya kumshukuru Mwenyeti Mungu nitumie fursa hii nikushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi. Aidha, nichukue fursa hii haraka haraka kumpa mkono wa pole Naibu Waziri wa Wizara hii Mhe. Zahra kutokana na kufiliwa na mama yake, *inshaalla* Mwenyezi Mungu amlaze marehemu mahala pema peponi nae ampe subra katika kipindi chote hiki cha msiba.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa leo hii tunajadili hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Ali Juma Shamhuna ihusianayo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Elimu kwa kipindi hiki cha mwaka 2014/15.

Kwanza nianze na Wizara hii kiujumla kwamba Wizara ya Elimu ni kati ya Wizara muhimu sana za nchi, wenzetu katika nchi mbali mbali Wizara hii na ya Afya huzipa umuhimu mkubwa katika bajeti zao. Nimefanya utafiti mdogo sana katika hizi nchi za falme za kiarabu Wizara ya Elimu na Maarifa huchukua karibu asilimia 40, imezidiwa na *Royal Guard Brigade* ambayo ndiyo inaongoza kwa kupata bajeti kubwa, lakini hii Wizara ya Elimu na Maarifa inapata karibu asilimia 45 sasa lazima tuone umuhimu wa hii Wizara.

Mhe. Mwenyekiti nalazimika kusema hivi kwa sababu ukiangalia kitaalam wasimamizi wakuu wa Elimu katika nchi, wao ndio wanaotupangia sisi aina ya elimu na utaratibu gani wa kupata elimu hiyo katika nchi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naweza nikaita Wizara ya Elimu ni kama masonara tunawapelekea vito wanatutengenezea mikufu, pete wanatutengenezea kila kitu nakusudia unampeleka mtoto pale si chochote pale, hajui lolote lakini mtoto aliyekuwa hajui lolote wala chochote basi huyo anatengenezwa kuwa *engineer*, anatengenezwa kuwa daktari, anatengenezwa kuwa mtaalam katika masuala ya migodi na mafuta.

Sasa kumtoa mtoto aliyekuwa hajui lolote mpaka utaalam basi kazi hii tunaweza kuifananisha na sonara anayeifanya dhahabu, anayeifanya shaba, anayeifanya lulu kuwa mkufu pete au kidani. Sasa hii ni Wizara muhimu sana na anayeongoza Wizara hii anatakiwa awe makini mno, inasikitisha sana Mheshimiwa Wizara yetu ya Elimu wakati huu haina kipaumbele katika kufanya mambo yake. Waheshimiwa ili mwanafunzi afaulu vizuri anahitaji madaftari, na majengo ya kukaa akasoma ili kupata utulivu wa kujifunza.

Mheshimiwa mimi katika jimbo langu la Wawi kwa kushirikiana na kamati ya maendeleo ya Jimbo, kwa kushirikiana na wananchi waliopo katika jimbo tumemudu kujenga mabanda katika skuli kadhaa za Sekondari na za msingi zilizopo pale, kwa mfano katika Skuli ya Ng'ambwa napenda sana niisifu kamati ya maendeleo ya skuli ya hii ikishirikiana na Diwani wake na Sheha na uongozi mzima wa Shehiya pale wameweza kujenga majengo kadhaa. Karibu hivi sasa kuna mabanda mawili na holi moja limeshafika katika *stage* ya linta yanataka kuezekwa, huu ni mwaka wa pili hayajaezekwa.

Aidha, nichukue nafasi hii kuwasifu kamati ya maendeleo ya Vitongoji pale Skuli ya Vitongoji wana mabanda mawili huu ni mwaka wa tatu, banda moja la Sekondari moja la *Primary* bado hayajaezekwa Mheshimiwa. Sasa mimi nilidhani kipaumbele chetu tungekitupa katika kuezeka majengo, inasikitisha sana mwenzetu katika uasisi anayeishikilia hii Wizara Mzee wangu pale hakutoa kipaumbele katika hili na badala yake ametumia shilingi milioni 69, 729,665,000/= kwa ajili ya kununua fanicha tu tena katika Chuo Kikuu cha *SUZA* huku mabanda ya shule yakiendelea kubaki.

Nashukuru Mhe. Raza pale asubuhi ametoa vielelezo mimi nilibahatika kupata *invoice* ya huo mkataba aliotia baina ya *Quality Furniture Limited* na *State University of Zanzibar* yaani *SUZA* . Hapa Mheshimiwa ukiangalia *contract* hii ilikuwa ya milioni 769,729,655/= mpaka sasa zimelipwa, zimebakia milioni 185,972,965/= hii ni bakaa, sasa nilikuwa nataka akija Waziri anifafanulie vizuri kwa nini akenda kuweka *contract* na *Quality Furniture Limited* ambayo iko Nyerere *Road opposite* na TBC pale Dar es Salaam na badala yake asije kuchukua *furniture* zile hapa Unguja ambapo kuna wajasiriamali kadhaa ambao wanachonga vizuri sana *furniture* , na siku zote tunasisitiza kwamba mambo ya kupunguza umasikini na kuongeza kipato katika nchi yetu.

Leo imepatikana *contract* kama hii inapelekwa Tanganyika wakati hapa Mikunguni vijana wanachonga vizuri mno, wala hatuhitaji safari kwamba tukishachonga tusafirishe aaa! Tukishachonga pale Mikunguni hatuhitaji kuzitia kwenye meli ni kuzichukua tu na kuzipeleka pale Chuo wakatumia. Sasa ni sababu gani ya msingi sababu ya kiuchumi ambayo ameitumia na kwenda kuweka *contract* na *Quality Furniture Limited* kwa Shilingi milioni 769 na kadhalika na asije akafanya hapa Zanzibar ambapo kuna vijana wetu wanaweza kupunguza bei, na hizi fedha zikatumika kwa kuniezekea lile banda langu la Skuli ya Ng'ambwa pamoja na skuli za Vitongoji yale mabanda yangu ya Sekondari na kuna Skuli ya Chaani pale, nimepita lipo banda halijaezekwa akenda akaezeka kwa nini Waziri asifanye hivyo, sasa hapo ndio nataka uje unieleze Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunazungumzia Wizara ya Elimu tulikuwa tunalaumu sana kwamba majengo yetu haya maeneo yetu na hivi viwanja vya shule, viwanja vya vyuo, majengo ya shule, majengo ya vyuo hizi ndio *Public Assets* na zinahitaji hatimiliki ili tusinyang'anywe nyang'anywe tu na watu wasije wakazivamia kwa miaka mingi tunapiga kelele jambo hilo. Kwa bahati mbaya sana hata hapa Chuo cha Mbweni sijui tayari tumeshapata hizi hatimiliki lakini kiwanja hapa eneo la Mbweni eneo la shule linaendelea kumwegwa siku hadi siku.

Sasa Waziri aniambie kwamba ni hatua gani ambazo amechukua ili kuona yale malalamiko yetu tuliyotoa siku za nyuma ya kwamba maeneo yetu ya Serikali ya shule haya kupatiwa hatimiliki, vipi kazi hii imefanywa na kama imefanywa ni kwa kiasi gani cha kusikitisha zaidi kumbe Serikali hainyang'anywi tu na wafanya biashara au wavamizi kumbe nayo pia inanyang'anya.

Nilikuwa na kilio kikubwa sana Mheshimiwa mwaka jana hapa kuhusiana na skuli ya Ndagoni eneo la skuli ya Ndagoni ni tatizo baina ya Wizara ya Elimu na wale wamiliki wa sehemu iliyopo shule, ile shule imeingia katika kiwanja cha bwana Ayoub Suleiman marehemu na mrithi mkuu wa eneo lile ni bwana mmoja anaitwa Suleiman Ayoub Suleiman anaishi Vitongoji Udusini pale, lakini shamba lao lipo Ndagoni, hawa walitakiwa watoe eneo ili iongezwe shule wakenda wakatoa eneo wakatoa bure kwa Wizara na mabanda yakajengwa.

Mhe. Mwenyekiti, ghafla Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Mwalimu Mkuu pale na Sheha wakaanza kuchukua lile shamba la wale warithi wakachukua shamba mpaka makaburi yao wakayatia katika eneo la skuli hii ni dhulma.

Mimi sidhani kama Waziri anayo habari ya hili kwa ninavyomjua Waziri huyu alivyokuwa hapendi kudhulumu, huyu sidhani kama ana habari na kama huna ndio nakupa taarifa Mhe. Waziri.

Mwaka jana alitoka Naibu Wako Waziri alikwenda kule akafanya mazungumzo na warithi pamoja na baadhi ya Wakurugenzi walikwenda pamoja na Naibu Waziri, sasa wakazungumza mazungumzo mengi lakini *ali-mention* mazungumzo yale hadi leo hii bado hayajatekelezwa, kwa hivyo bado ikawa ni tatizo. Nakuomba sana Waziri hili uliangalie shule ya Ndagoni Pemba kuna ugomvi baina ya Familia ya bwana Ayoub Suleiman inayoongozwa na Suleiman Ayoub Suleiman, mkaazi wa Vitongoji Udusini pamoja na shule ile pale Langoni.

Sasa niende moja kwa moja katika elimu ya msingi ukurasa wa 31 ibara ya 55. Mheshimiwa shule za msingi ni muhimu sana kwa ajili ya kutoa taaluma, na mpaka sasa hivi kuna taarifa ambazo Mheshimiwa sijazithibitisha hizi kwamba mwaka 2009 lilitoka azimio la kwamba elimu ya msingi baada ya kuandikisha miaka saba sasa iwe miaka sita, sasa katika hili unapotoa azimio kama hilo Wizara inatakiwa iwe na umakini wa hali ya juu katika kukabiliana na mabadiliko kama hayo, inasikitisha sana kwamba Wizara ya Elimu pamoja na azimio hilo la kuweka elimu ya msingi kwa miaka sita hadi leo hii vitabu vile vya wanafunzi na walimu vinavyokabiliana na badiliko hilo bado havijapatikana.

Pamoja na muongozo wa mwalimu vile vile na inaonekana kwamba Wizara inalazimisha kwamba wasomeshe kupitia muhtasari iliyopelekwa lakini vitabu vya rejea havipatikani je, hapo Mheshimiwa Wanafunzi wetu ambao ni wa msingi wataweza kukabiliana na mabadiliko hayo na kufanya vizuri masomo yao ya sekondari.

Nimalizie hapo kwamba Mheshimiwa nakuomba sana inaonekana kwamba elimu ya msingi wanataka wasome kwa kiswahili kwa miaka minne, na kiingereza kwa miaka miwili sasa miaka miwili wataweza kufahamu lugha ya kiingereza na baadae wakaitumia Sekondari, naomba wataalam wako wakupe jibu uje utueleze katika hili, kuna ukweli wa hilo au ni maneno tu huku uswahilini tunapeyana peyana.

Sasa niende katika suala la maslahi ya walimu; maslahi ya walimu bado ni madogo Mhe. Mwenyekiti ni madogo sana yanatia haya mwalimu ni kioo katika jamii, leo anakwenda mwalimu katika shule kufundisha huku akiwa amevaa yebo yebo wakati mwanafunzi amevaa buti, hiyo siyo aibu? Sasa mimi nashauri tu Mheshimiwa kwamba Serikali iangalie pamoja na haya mabadiliko wanasema wanaboresha lakini wameboresha hawakuangalia hawa walimu wetu wa zamani, ambao hawawezi tena kujiendeleza kwamba elimu yao ni ndogo na mshahara wao ni mdogo na wamefanya kazi miaka mingi.

Mimi nadhani hapo wapaangalie sana ili kuboresha mafao yao, na inasikitisha sana Mheshimiwa kuna tatizo la walimu wa Sayansi katika shule zetu walimu wanapangwa masafa marefu kwenda kusomesha katika maeneo mbali mbali lakini hawana makazi, mimi nadhani Mhe. Waziri kuna haja sasa ya kuandaa utaratibu wa walimu kupatiwa majumba au kama hawana uwezo wa kujenga nyumba basi katika mishahara yao wawekewe *house allowance*, ili waweze kukodi huko uswahilini na kuweza kutusomeshea watoto wetu.

Leo inasikitisha sana katika shule ya Jambiani kule, walimu nyumba ni mbovu wanazokaa pale wanalazimishwa zile nyumba wazifanyie matengenezo walimu wa Jambiani wakati katika mishahara yao mumewawekea pesa za haya matengenezo, kama hamukuwawekea wazipate wapi Mhe. Waziri, mimi nadhani katika hilo muliangalie upya na hawa walimu wetu wa Jambiani muwaone vizuri sana.

Sasa Mheshimiwa kuna haya mafunzo ya amali, kwanza nipongeze kwa kutoa wanafunzi karibu 580 katika kipindi hiki cha mwaka 2013/14. Hili nipongeze kwa kweli hapa mumefanya kazi nzuri na wanafunzi wale wanatoka wapo vizuri, lakini cha kusikitisha Mheshimiwa tuliambiwa hawa watapata kama ruzuku ya kuanzia kujiendeleza katika jamii na karibu *bench* mbili zimetoka hakuna chochote kilichotoka hilo (a). Lakini (b) zile skuli zetu tatu Mheshimiwa ikiwemo ile Skuli ya Mkokotoni na skuli ya Vitongoji zote hazina uzio zile ni tatizo na miaka yote tunapiga kelele kwamba zile shule zijengewe uzio kusudi mali na wanafunzi wetu wawemo salama mle. Kwa hivyo naomba utakapokuja hapa Mhe. Waziri unieleze ni lini skuli zile za mafunzo ya amali iliyopo Mkokotoni, ambayo inatoa mafunzo ya ufundi vizuri sana na ile iliyoko Vitongoji shule zile lini zitawekewa uzio.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa hii shule ya Kiembesamaki. Skuli hii inapokea wanafunzi wenye vipaji kutoka katika Chuo cha Kiislam pale. Wanafunzi wenye vipaji wanachanganywa na wanafunzi wa kawaida katika shule ile ya Kiembesamaki, yaani wanafunzi kutoka Chuo cha Kiislam wanakuja kuchanganywa na wanafunzi wa shule ya

Kiembesamaki. Mimi nilikuwa nafikiri Mhe. Waziri uje utufafanulie kwamba ufanisi katika kupokea mafunzo baina ya wanafunzi wa aina mbili hizi wale wenye vipaji na wale wasio vipaji. Umewachanganya pamoja si tutapoteza upande mmoja huku au tukampa kazi kubwa mwalimu. Nusu wanashika haraka nusu hawashiki vizuri tatizo halitotokea hapo.

Mhe. Waziri mimi nadhani ungeandaliwa utaratibu ikiwezekana kama hili suala ni kweli basi hawa wenye vipaji tuwaweke pembezoni ili waweze kukamata vizuri, na hawa waliokuwa hawana vile vile tuwaweke sehemu yao kusudi mwalimu anapofundisha aweze kujua kwamba hawa *ability* yao ni hii na hawa *ability* yao ni hii, kusudi tusimpe kazi mwalimu ya kufundisha katika darasa lenye vipaji tofauti.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa nitaunga mkono hii hoja pindi Waziri atakapokuja kunieleza kwa kina na kuniletea mkataba wa makubaliano baina ya *quality furniture limited* na SUZA sambamba na atakaponieleza hii kadhia ya Bwana Suleiman Ayoub Suleiman na Wizara ya Elimu kuhusiana na ile Skuli ya Ndagoni. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyetuwezesha kutupa uhai na uwezo wa kufika hapa kuzungumza. Vile vile ninakushukuru na wewe kunipa nafasi kidogo ya kuzungumza. Niishukuru pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake mzuri. Halafu niwapongeze Mawaziri wote kwa jumla waliokuwa wana jukumu kubwa lililowakabili na liko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamshukuru Mhe. Waziri, ninampongeza pamoja na watendaji wake na ninampongeza kwa sababu hii ni Wizara nyeti na Wizara hii inataka iwe na vielelezo na mambo makubwa ya kuweza kuyafanya. Vile vile ninampongeza Waziri aliyepita wa Elimu. Mheshimiwa mimi nilikuwemo katika kamati kipindi kilichopita ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto, na nilikuwa na kilimo kila siku nikikizungumza na akafika Mhe. Haroun kuweza kusema kuwa matatizo haya yataondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia Elimu Mjumuisho. Elimu Mjumuisho inahusisha watu mbali mbali na wanachanganywa na wenzao waliokuwa wako makini ambao si walemavu na kule tuko walemavu wa aina 6. Pengine darasa litakuwa lina walemavu 2.

Kwanza nitazungumzia miundombinu kutokea 2005, niliitumikia hii katika miaka miwili na nusu na nilipita maskuli mbali mbali na nikaziona shida ziliomo, lakini basi hata kukarabati tukaweka miundombinu iliyokuwa ni rafiki na watu wale pia hatuwezi. Tusiwajengee Skuli zao wakati Skuli ndio ile ile lakini iweze kufanyiwa ukarabatu waweze angalau wale watu wenye ulemavu kuweza kufika kwa ulemavu wao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kilio cha watoto walemavu maskulini. Kwanza kutofahamu yanayozungumzwa katika skuli. Ninamtaka Mhe. Waziri aje atueleze ni walimu wangapi wa Elimu Mjumuisho waliokwenda mafunzo na wakaweza kupatikana Unguja na Pemba.

Halafu katika madarasa Mheshimiwa vikalio vilivyokuwa vimo angalau muunde vikalio maalum kwa watu wenye ulemavu; yale madeski wengine hawawezi kukalia. Ukienda kukagua utamkuta mtoto mlemavu aliyekuwa hawezi kukaa pale yuko chini. Kwa kweli ni jambo lililokuwa linatusikitisha. Tunaiomba Serikali, Waziri uwe makini kwa sababu Elimu Mjumuisho imejumuisha mataifa mbali mbali, watu mbali mbali, wote tuko pale na elimu ndio ufunguo wa maisha ya mwanadamu.

Halafu nataka niseme kila siku nasema, hawa walimu wanakwenda sawia na watoto hawa mule tunamosomeshwa, tukenda tunakuta kilio cha kwamba watoto wale hawafahamiki wala wao hawawafahamu walimu wanaowasomesha. Na tukiuliza tunaambiwa kuna watu wanafundishwa, mimi kila skuli ninazokwenda ninakuta mwalimu wa aina hiyo hamna. Sasa mwalimu mmoja kuna mabanda kumi na mbili pengine mna walemavu 10, atawazungukia vipi kupata kuwasomesha. Hapa tuliambiwa na Mhe. Haroun atafanya vikao na walimu jinsi na wale waliopata elimu ile kuweza kupeana ujuzi, ili na wale wajue angalau kuzungumza na wale wapate angalau kuweza kuwajua wale watoto walemavu mahitaji yao. Sasa atakuja kutueleza Mhe. Waziri mafanikio aliyoyapata ya walimu na ni Skuli ngapi aliowapeleka walimu hawa kuweza kufundisha watoto hawa.

Halafu mimi nilikuja hapa mara moja nikachangia, nikasema Skuli kwa Pemba tuna moja tu ya mahitaji maalum iliyopo Chake Chake lakini hata ile Skuli nayo haiboreshwi, ukienda iko vile vile. Kwa sababu hizi Skuli katika kuboreshwa mna vifaa mbali mbali tunavyovihitaji vya kusomea, ukienda utakuta Skuli ina kifaa kimoja lakini pia mwenye kutumia kifaa kile hayupo wa kuweza kufundishia. Kwa hivyo atakuja kutueleza maana Skuli nyingi mara moja vifaa vimepelekwa, lakini mimi Skuli nilizozitembelea nikawahi kuviona niliambiwa kifaa hiki lakini bado hayupo awezae kukitumia ambacho ni cha watu wasioona.

Nije kwenye ada; nilimwambia mara moja Mhe. Haroun kuna watu ambao hawajiwezi ni walemavu na watoto ni walemavu, katika ada akasema nimeiondoa ada kwa mtoto mlemavu. Lakini kwa kila leo ni kilio husaidia mimi ninaowaweza nisiowaweza nikawaacha, anazuia vipi mtoto kuwa asende kusoma na jambo la lazima kwa kuwa hana ada. Mhe. Haoun alitwambia aliyekuwa hana ada hata mtu wa kawaida asizuiwe kusoma ili apeleke kidogo kidogo mpaka ada yake itimie, aje atueleze kilio kimezidi. Akifika yule akiipata ada kwa muda miezi mitatu hajenda au miezi minne ukifika humrudishi nyuma anaendelea walipo wenzake huku nyuma keshakosa. Kwa sababu gani tufanywe hivyo na tushajua mtu wa chini ni maskini, kupata elfu tano kwake ni sawa na kapata laki tano. Mtu ana watoto 6 wote wanataka walipiwe kwa nini asiweze kulipia kwa ule mpango ulioambiwa aweze kupeleka kidogo kidogo mpaka ada yake imalize na watoto hawa waweze kuzuiliwa kwa kuwa hawajatoa ada.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, sare za Skuli, mimi nimeshakwenda kupapatua maskuli mengi sana, mtoto anazuiwa kwa sababu hana sari lakini mtizame mtu wa kijijini kipato chake alichonacho watoto anaosomesha ni 4, kapigana kapata sare ya watoto 2 lakini keshakwenda kumwamia mwalimu na hawa nitajirekebisha watapata. Watoto wale wanasimamishwa kusoma mpaka wende na sare. Sasa wakisimama kwa miezi miwili mitatu wakifika utamuanzisha hapa au utakwenda kumpeleka mbele waliko wenzake, malengo umeshayapoteza.

Tunaiomba Wizara ya Elimu iwe makini kwa sababu sote hatuwezikuwa sawa kipato chetu kwa watoto kuwasomesha, kuna waliokuwa wanaweza kulipa kwa mara moja watoto wake wanne, kuna na wanaoweza kuwa wana watoto 4 akalipia mmoja. Sasa yote hayo tuyaone ni kilio.

Halafu mimi nitasema haya maskuli tunayoyajenga, tunajenga maskuli mengi kuondoa kero lakini kero tunazizidisha, maskuli ukenda hamna vikalio. Hamna kitu chochote tushatembelea Skuli mbali mbali tukenda watoto wanatandikiwa majamvi chini. Unaonaje tukawa na Skuli za kiasi tukiwa tunatataka kujenga ghorofa mwaka huu lakini zile pesa tukatafuta vifaa tukaingiza maskulini. Kwa sababu watu sasa wanakwendea na utandawazi, dunia imepanuka sio tena kusoma chini ya miti au tukasoma chini tukatandika majamvi. Sasa mimi ninamwambia Mhe. Waziri tunajenga kuondoa matatizo lakini na matatizo tunayazidisha. Maskuli ni mengi lakini mahitaji kwenye maskuli hamna.

Nataka nimuulize Mhe. Waziri na atakuja kutueleza, kuna maudhi yaliopo maskulini jinsi ya walimu na watoto wanaowasomesha kufanya nao mapenzi. Atueleze ni Skuli ngapi walimu hawa kawapata na ni adhabu gani aliowapa walimu hawa na watoto waliokuwa wamepata ujauzito ni wangapi kwani katika kitabu sijapata kuona, hili vile vile tujue. Kwa sababu ni kero kubwa hapa aje atueleze.

Kipindi kilichopita tulimwambia Mhe. Haroun na akathibitisha kwamba yeye aliyapata mashtaka kama hayo, tunamuomba Mhe. Waziri awe makini na yakikutwa makosa kama haya waweze kuyapigia vita sana walimu kupata adhabu inayostahiki.

Halafu Mheshimiwa unyanyapaa wa watoto wenye ulemavu katika maskuli; maskuli yetu haya ya elimu mjumuisho. Kila siku tunalipigia debe hili la kuwa unyanyapaa dhidi ya watoto wenye ulemavu upunguzwe, lakini maskulini umo na watoto wale wakipata mambo kama yale huwa wanakimbia Skuli. Kwa sababu ni watu ambao wanajiona kuwa ni dhaifu au vipi wakipata wale wenzao kuwachokoza wao hawendi kule mashuleni. Tunaomba vile vile Mhe. Waziri aweze kuzungumza na walimu kuyakabili mambo kama haya ya unyanyapaaji wa watoto walemavu maskulini.

La mwisho kabisa ninamuomba Mheshimiwa katika maskuli lazima miundombinu iwe rafiki ikiwa mtoto ana kigari chake aweze kuingia na kigari chake na aweze kukaa juu ya kiti chake kuweza kusoma pamoja na wenzake. Na ikiwa mumechongwa madeski mfano akajua kuwa hii Skuli ina watoto wenye mahitaji maalum basi kuwe na viti maalum angalau viwili vitatu aweze kuvichonga viti hivyo vya mtoto mmoja mmoja viweze kuwasaidia mahitaji yao, kwa sababu kwa vile viti tunavyokalia vya maskuli wale huwa vinawapa shinda sana Mheshimiwa.

Kwa hivyo naomba sana serikali wawape kipaumbele na hata hawa walimu wa kuweza kuunda hii mitaala kuwasomesha na wao kingereza.

Kwa hayo machache ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii; hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naomba nimpongeze Waziri kwa hotuba yake hii ambae ametuwasilishia leo na pia niwapongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, Walimu Wakuu wote na watendaji wote wa Wizara hii kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti umeeleza mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2013/2014 na ameeleza mafanikio mbali mbali katika kitabu hiki. Kwanza ninaomba nipongeze kwa dhati kabisa mafanikio yote ambayo yametekelezwa katika Wizara hii kupitia nyanja mbali mbali. Mhe. Waziri ameeleza humu baadhi ya mafanikio; ameeleza ujenzi wa Skuli tatu mpya za Sekondari za ghorofa, wameeleza suala la asilimia ya ufaulu ya watahiniwa wa mitihani kidato cha pili, kidato cha nne, wameeleza Chuo Kikuu cha Taifa Suza kuanzisha *course* ya PHD, wameeleza usambazaji wa vifaa mbali mbali vya mashule. Kwa hivyo ninaipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa mafanikio yote ambayo yameelezwa humu na ninaomba wazidishe jitihada hiyo ili tuendelee mbele katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Katika ukurasa wa 27 katika Idara hii imeeleza kuna wafanyakazi kama 137 wamestaafu katika kipindi cha mwaka 2013/2014. Hapa naomba nipate maelezo tu juu ya wafanyakazi 137 je, wamelipwa haki zao.

Ninakwenda katika mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi kwenye ukurasa wa 8. Mradi huu umeelezwa utekelezaji wake ni mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo. Na wamesema mradi huu umetengewa jumla ya bilioni moja kwa mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo bilioni 7,212,032,000. Na wametaja washirika wa maendeleo wenyewe ni UNICEF, UNESCO, USAID, GPE, SWEDEN, lakini wameweza kufikia Mei mwaka huu SMZ imechangia milioni 175,000,000 na washirika wa maendeleo wametoa bilioni 2,881,271,948. Pia mradi huu malengo yake makuu wameeleza hapa.

La kwanza kukamilisha ujenzi wa madarasa 480 ya Unguja na Pemba. Wakaeleza kufanya ukarabati majengo mbali mbali ya Skuli, wameeleza kuchonga madawati 10,000 na kusambaza katika madarasa mapya na ukiangalia kuna ripoti ya kamati ya Wizara hii ya Elimu imeeleza kuna baadhi ya Skuli ambazo zimejengwa lakini zimekosa ubora na baadhi ya Skuli nyengine zimeanza kubomoka kwa kipindi kifupi ambacho Wizara imekabidhiwa Skuli hizo, na akatoa mfano katika ripoti amesema Skuli ya Faraja, Uzini.

Hapa nilikuwa ninaiomba Wizara kuwa makini katika ujenzi wa majengo ya Skuli na ihakikishe inawatumia wataalam wake kusimamia na kuona kwamba ujenzi huu unajengwa katika kiwango ambacho kinastahiki, sio wanawaaachia tu wajenzi wanafanya wanavyotaka. Matokeo yake tunapata nyumba ambazo hazimo katika ubora ambao unastahiki.

Kwa hivyo naiomba Wizara isimamie kwa dhati kabisa suala hili kuwatumia wataalam wake kwa *stapes by stapes* ujenzi unavyoendelea. Pia katika suala zima la uchongwaji wa madawati ninaiomba Wizara ihakikishe yale madawati yanayochongwa yanatengenezwa kwa kiwango ambacho kizuri sio yanachongwa madawati baada ya muda yanaharibika.

Pia ninaiomba tena Wizara kusimamia fedha hizo za wafadhili kwa sababu hizi fedha za wafadhili Mhe. Mwenyekiti ni fedha za walipa kodi sawa sawa na sisi huku kwetu. Tusichukulie kwamba ni msaada tu tukatumia kinyume na malengo. Kwa hivyo tunaomba tuithamini misaada ya wafadhili ambapo wafadhili hao wanatusaidia kwa moyo ili kuendeleza nchi yetu katika maendeleo